# Nipashe

Jumanne Oktoba 11, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581095

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 70071 LIKE & FOLLOW

JACKPOT BABA LAO!
TZS. 367,741,460
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



RIPOTI MAALUM

**Bwana** harusi alivyouawa kwa risasi akivua samaki mgodini

UKURASA 4



**HARMONIZE: KUENDESHA LEBO SI MCHEZO**

UKURASA 27

# Vikwazo 14 kibiashara Kenya, Tz kuondolewa

• **Samia**, Ruto wasema sasa hakuna majibizano ni ushirikiano... *Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akiagana na Rais wa Jamhuri ya Kenya, Dk. William Ruto, baada ya kuhitimisha ziara yake ya kikazi ya siku mbili jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**MWINYI AZINDUA KIKOSI KAZI KUCHAKATA MAONI**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amezindua kikosi kazi cha kuchakata maoni ya wadau wa siasa Zanzibar baada ya kupokea ripoti ya maoni...

UKURASA WA 5

**UGONJWA SONONA UNAVYOATHIRI WANAWAKE KIAKILI**

WATU milioni 1.5 nchini wanaishi na ugonjwa wa sonona huku wengi wao wakiwa wanawake...

UKURASA WA 8

**LHRC YATAJA SABABU NNE KUPINGA ADHABU YA KUNYONGWA**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimetoa sababu nne za kutaka adhabu ya kifo ifutwe nchini, ambazo...

## Padri atuhumiwa kumbaka mtoto aliyeenda kuungama

UKURASA 3



## Job Ndugai: Hata wabunge hutakiwa kupimwa afya akili

UKURASA 2

**MICHEZO** CHAMA ATOA SIRI KUSHINDA UGENINI UK.32

**KABWELA** UK.7

# Vikwazo 14 kibiashara Kenya, Tz kuondolewa

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan na Rais wa Kenya, William Ruto, wametoa agizo kwa mawaziri wa uwekezaji kuondoa vikwazo 14 vya biashara vilivyosalia baina ya nchi hizo.

Pia wakuu hao wa nchi wamekubaliana kushirikiana katika masuala mbalimbali ya kimkakati ya kuimarisha uhusiano na ushirikiano ikiwamo wa kibiashara.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kufanyika kwa mazungumzo yao, Rais Samia alisema jambo la kwanza walilozungumzia ni namna ya kuweka mazingira mazuri ya kibiashara baina ya Tanzania na Kenya.

Samia alisema wamewaagiza mawaziri wa Sekta ya Biashara na Uwekezaji wa nchi hizo kushughulikia vikwazo 14 visivyo vya kikodi vilivyobaki ili nchi hizo ziwe na uhuru mpana wa kufanya biashara.



"Kazi hii ilianza na Rais mstaafu, Uhuru Kenyatta na tulikubaliana kuvifanyia kazi vikwazo vya kibiashara, kwa ujumla wataalamu walitambua vikwazo 68 ambavyo vilifanyiwa kazi, vikwazo 54 viliondoka visivyo vya kikodi na vimebaki 14," alisema Rais Samia.

Alisema kazi ya kuondoa vikwazo hivyo imekuza biashara kati ya nchi hizo mbili ingawa Tanzania imenufaika zaidi.

Kadhalika, alisema wamezungumzia Mkutano wa Nne wa Tume ya Pamoja ya Ushirikiano ambao ulikuwa ufanyike Agosti, mwaka huu, lakini haukufanyika.

Alisema katika kulitekeleza hilo, wamewaagiza mawaziri wa mambo ya nje wa nchi hizo wakutane na kuzungumzia mambo yaliyoko katika ajenda zao na kuyachukulia hatua kwa haraka.

Walijadili pia namna ya kuimarisha mipaka ya kimataifa ya nchi hizo ili watoto wao ambao ndiyo viongozi wa baadaye waijue imepita wapi.

Rais Samia alisema wamezungumzia bomba la kusafirisha gesi kutoka Dar es Salaam hadi Mombasa, ambao walishasaini makubaliano na Rais mstaafu wa Kenya, Uhuru Kenyatta, utakuwa mradi wa kwanza kusimamiwa na Rais Ruto.

Vile vile, Rais Samia alisema suala lingine waliloteta ni kudhibiti vitendo vya uhalifu vinavyovuka mpaka na kuviagiza vyombo vya ulinzi na usalama kushirikiana kutokomeza vitendo hivyo, ikiwamo dawa za kulevya, usafirishaji haramu wa binadamu, ujangili na uharamia.

"Tumetaka wakae waangalie kwa hizi nchi zetu mbili tutafanya vipi, kwa sababu tumekuwa tunapata sifa mbaya ya human trafficking (usafirishaji haramu wa binadamu) wakati wanaosafirishwa sio Watanzania, sisi tunakamata tu, lakini wakifika kwetu record (takwimu) za dunia zinaiona Tanzania au Kenya," alifafanua Rais Samia.

Pia alisema wamejadili ushirikiano wa kikanda na kimataifa na wamekubaliana kuendeleza ushirikiano mzuri na madhubuti ndani ya Afrika Mashariki, Afrika na Umoja wa Mataifa (AU).

Kwa upande wake, Rais Ruto alisema walizungumzia namna ya kuondoa vizuizi vinavyosababisha biashara ya utalii kwenda taratibu.

Kadhalika, namna ya kurahisisha mawasiliano katika nchi hizo mbili ili wananchi wake waweze kuwasiliana kwa urahisi na gharama nafuu ikiwa ni mpango wa nchi za Afrika Mashariki wa kuwa na mtandao wa mawasiliano mmoja.

Rais Ruto alisema kwa kipindi kimoja cha uongozi wa Rais Samia, usafirishaji wa bidhaa kutoka Kenya kwenda Tanzania umeongezeka kutoka Sh. bilioni 31 hadi Sh. bilioni 45, wakati mauzo ya biashara kutoka Tanzania kwenda Kenya yameongezeka kutoka Sh. bilioni 27 hadi Sh. bilioni 50.

Alisema nchi hizo zimeachana na majibizano yalikuwapo huko nyuma na sasa wanashirikiana kuimarisha uhusiano mwema kwa manufaa ya wananchi wao.

"Ile historia ya zamani kidogo mabishano tumeyaweka nyuma yetu, tunataka kujenga uhusiano mwema, tunataka Watanzania wafaidike na Wakenya wafaidike pia, Wakenya wakifaidika na sisi Tanzania itafaidika," alieleza Rais Ruto.

Rais Ruto aliwasili nchini juzi ikiwa ni ziara yake ya kwanza kikazi katika ukanda wa Afrika Mashariki tangu alipoapishwa kuwa Rais Septemba 13, mwaka huu.

## Ndugai: Hata wabunge hutakiwa kupimwa afya ya akili

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SPIKA mstaafu, Job Ndugai, amesema suala la wabunge na madiwani kupimwa afya ya akili kabla ya kuwania uongozi na katikati ya muhula ni la wananchi kuamua.

Alisema ukosefu wa elimu ya afya ya akili unachangia watu kushindwa kujua dalili za ugonjwa huo mapema.

Ndugai aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza kwenye kilele cha maadhimisho ya Siku ya Afya ya Akili Duniani ambayo hufanyika kila mwaka Oktoba 10.

Maadhimisho hayo yalifanyika Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe, jijini hapo.

"Hata kule bungeni wakati fulani huwa unatolewa wito kwamba wabunge wapimwe akili wapelekwe Mirembe kwanza kabla ya kupata fomu za kuomba ubunge."

"Wanataka tunapochukua fomu za kuomba ubunge tuje kwanza Mirembe tupimwe akili na katikati ya muhula tena tupimwe hiyo pia ni kwa madiwani wakichaguliwa, sasa sijui jambo hilo ni muhimu au sio muhimu, wanasisitiza sana jambo hilo, hilo la wananchi nadhani tuwaachie wenyewe," alisema.

Alisema licha ya kuwa mwana Dodoma, alikuwa hajawahi kufika katika hospitali hiyo.

"Mimi ni mwana Dodoma, lakini ndiyo siku yangu ya kwanza kufika hapa Hospitali ya Mirembe, tunaijua sana, lakini wengi hawajapata nafasi ya kuitembelea nimeachana na mtazamo ule wa zamani ya kuwa ni hospitali ya watu wa matatizo ya afya ya akili."

"Taarifa zilizoko mtaani zinazohusu hospitali hii ni nyingi sana leo sio siku yake ya kuelezea, leo ndiyo tunaanzia huko, lakini nimewakuta mko kawaida tu kama sisi, tofauti na nilivyowafikiria nikiwa huko uraiani," alisema.

Hata hivyo, alisema jamii inashindwa kutambua dalili za ugonjwa huo na kusababisha mtu kujulikana wakati amesha athirika.

"Hata makazini mtu anakuwa 'demoted' (kushushwa cheo) kutokana na kuwa na matatizo ya afya ya akili, kumbe mtu anahitaji msaada wa afya ya akili, ili aweze kuwa sawa na kuendelea na majukumu yake ya kila siku," alisema.

"Nimeshangaa kuambiwa wanapima hadi sonona nikauliza sonona ndiyo nini nikaambiwa ni masononeko ambayo mtaani ni mengi sana, lakini watu hatuyajui."

Alisema miaka ya nyuma mtu alikuwa akisema ana faili la Mirembe anakuogopa hususani huko vijijini.

"Ukimgusa tu anakwambia mimi nina faili la Mirembe, ulikuwa hata ukimgusa mtu mwingine anakwambia huyo anafaili Mirembe yaani akimaanisha yuko juu ya sheria. Lakini sasa hivi mambo ni tofauti, nawapongeza watumishi ila msichoke kutoa elimu kwa jamii ili kujua nini maana ya afya ya akili," alisema.

Aliipongeza serikali kwa kutoa zaidi ya Shilingi bilioni tano kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya hospitali hiyo, huku akisema wataendelea kuwaomba wabunge kuiomba serikali iongeze bajeti.

Aliwataka wanafunzi kujiepusha na dawa za kulevya akitahadharisha kuwa ni chanzo cha kuchangia magonjwa ya akili.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi wa hospitali hiyo, Dk. Enock Changarawe, aliomba miundombinu iboreshwe kutokana na hospitali hiyo kuwa ya muda mrefu.

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

DAUD LUKANDA KUSHOKA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T.553 BVC yenye Engine No. 3s2866013, Engine Capacity 1990, Model No. GF-SR40G aina ya Toyota NOAH.

Yeyote atakayeiona ataoe taarifa kituo cha polisi kilicho jirani yake.Taarifa ya polisi. DAR/MSI/RB/395058/2022.

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

HAWA SUBIRA MWAIFUNGA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 438 DZX – TOYOTA HARRIER. Chassis namba ACU300060386. Engine namba 2A2B234708. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.

Taarifa ya Polisi: DSM/PHQ/RB/327018/2022.

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA DODOMA**
**LILILOKO DODOMA**
**MAOMBI NA. 185 YA MWAKA 2022**
**KHAMISI RAMADHANI.......................MUOMBAJI**
**VERIUS**
**RIZIKI MBENA .............MJIBU MAOMBI**

**KWA: RIZIKI MBENA**
**POPOTE ULIPO**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi inapatikana katika Baraza hili.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 07.11.2022 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.

**ANAGALIZO:** - kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likidhibitisha kuwa umepokea hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 10 ya mwezi wa Oktoba,2022.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya Geita**
**KITUO CHA NYANKUMBU**
**MKOA GEITA**
**SHAURI LA MADAI 143/2022**
**Jina la Mdai : MARIAMU NYAKITAGARI**
**Jina la mdaiwa: DIANA BLANGIDA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**( kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika mahkama za Mwanzo)**

**Kwa DIANA BLANGIDA WA NYANKUMBU**
**Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/ wameleta madai yake/yao kwamba ( Eleza hapa habari za madai)**

**MADAI YA FEDHA TSH 1,040,000/=**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 13 Mwezi 10 mwaka 2022 saa 8:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.

**ANGALIZO** kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 27 mwezi 9 mwaka 2022

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

THERESIA ROMANUS MWACHA anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba T309 DNT. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/397914/2022

## Padri atuhumiwa kumbaka mtoto aliyekwenda kuungama

**Na Mary Mosha,** MOSHI

PAROKO wa Parokia Teule ya Mtakatifu Dionis Aropagita ya Jimbo Katoliki la Moshi, Padri Sosthenes Bahati (41), amesomewa maelezo ya awali ya kesi anayotuhumiwa kubaka mtoto katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi mkoani Kilimanjaro.

Akisomewa maelezo hayo, alikiri kutambuliwa kwenye gwaride maalumu la utambuzi na kukana kutenda kosa hilo.

Mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Mwandamizi, Salome Mshasha, Wakili wa Serikali Mwandamizi Kassim Nasri, aliyeambatana na Wakili Sabitina Mcharo alidai mshtakiwa alitenda kosa hilo Agosti 12, mwaka huu, mtoto alipokwenda mbele yake kuungama.

"Agosti 12, mwaka huu, mtoto huyo alikuwa kwenye Kanisa Katoliki la Mtakatifu Dionis Aropagita, Kawawa kwa lengo la kushiriki mafundisho ya Kipaimara kama inavyotakiwa na alirudi jioni kwa ajili ya kuungama dhambi zake.

Wakati wa maungamo alimkuta mshtakiwa (padri) amekaa kwenye kiti chake, naye alipiga magoti na kuanza kuungama dhambi zake, kwa kuzitaja moja moja, wakati wa kupokea kitubio, mshtakiwa alianza kumtomasa sehemu mbalimbali za mwili wake hadi sehemu za siri," alidai.

Wakili Nasri alidai baada ya kumtomasa alimvua nguo na yeye kupandisha kanzu yake na kumfanyia ukatili wa kumwingilia kimwili.

"Mtoto alipofika nyumbani kwenye mazungumzo ya mama na mwana, alimsimulia mama yake kilichotokea ndipo mama huyo alipokwenda kutoa taarifa polisi," alidai na kuendelea "uchunguzi wa awali ulionyesha mtoto huyo ameingiliwa na lilipofanyika gwaride la utambuzi alimtambua mshtakiwa huyo."

Upande wa Jamhuri katika kesi hiyo una mashahidi 10, wanne kati yao wataletwa kutoa ushahidi wao mfululizo.

Wakili Nasri alidai kuwa upande wa Jamhuri ulikuwa tayari kuendelea na kesi hiyo ingawa wakili wa utetezi, Edwin Silayo, aliiomba mahakama hiyo kutosikilizwa kwa kesi hiyo ili kumpa nafasi ya kukatana na mteja wake.

Alidai pia wana mpango wa kuegemeza utetezi kwa kuleta ushahidi wa mshtakiwa kutokuwapo eneo la tukio siku ya tajwa.

Hakimu Mshasha aliahirisha kesi hiyo hadi kesho.

Padri Bahati alifikishwa mahakamani Septemba 26, mwaka huu, akikabiliwa na kesi za ubakaji tatu za watoto walio chini ya umri wa miaka 12, mbili zikiwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi na moja katika Mahakama ya Wilaya ya Moshi.

# DC awatoa hofu wageni ebola kuzima Mwenge

**Na Mary Geofrey,** KAGERA

MKUU wa Wilaya ya Bukoba, Moses Machali, amewatoa hofu viongozi wa serikali na wageni wanaowasili wilayani hapo kwa shughuli ya kuzima Mwenge wa Uhuru, kuwa ni salama na hakuna mgonjwa wa ebola.

Rais Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kuzima Mwenge huo Ijumaa, Oktoba 14 na viongozi wa serikali na kitaifa wanatarajiwa kuanza kuwasili mkoani humo leo.

Alisema serikali imechukua tahadhari zote muhimu na hakuna mgonjwa wa ebola katika wilaya mkoani humo.

Pia alisema zipo juhudi zinafanywa na serikali ikiwamo kuainisha vituo vya kuwatenga na kuwatibu wagonjwa watakaobainika kuwa na ugonjwa huo.

Eneo la Nchambya ambako wanajenga Hospitali ya Halmashauri ya Bukoba limetengwa kwa ajili ya kutibu watu watakaobainika kuwa na ugonjwa huo.

"Wilaya ya Bukoba tumejipanga kupokea wageni wanaoingia hapa, nawahakikishia tupo salama, hakuna ebola isipokuwa tunaendelea kuchukua tahadhari zote muhimu zinazotakiwa," alisema Machali.

Awali Mganga Mkuu wa mkoa huo, Issessanda Kaniki, alitembelea kituo cha mabasi cha Bukoba na kutoa elimu kwa madereva wa daladala, makondakta na wapiga debe.

Aliwataka wananchi wa eneo hilo kuendelea kuchukua tahadhari wakati huu ambao serikali inapokea wageni wengi kutoka maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya shughuli ya kuzima Mwenge wa Uhuru.

Kadhalika, alitembelea nyumba za kulala wageni na kutoa elimu hiyo pamoja na kuweka vipeperushi vitakavyosaidia kutoa elimu kwa wananchi.




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (kulia), akimkabidhi Mwenyekiti wa Kamati Maalum (kikosi kazi), Dk. Ali Uki, ripoti ya wajumbe wa kamati maalum ya kuchangia maoni ya washiriki wa mkutano wa wadau wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa, kwa ajili ya kuifanyia kazi katika hafla iliyofanyika jana Ikulu, Zanzibar. **PICHA: IKULU**

## Mwinyi azindua kikosi kazi kuchakata maoni siasa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amezindua kikosi kazi cha kuchakata maoni ya wadau wa siasa Zanzibar baada ya kupokea ripoti ya maoni.

Wiki iliyopita Rais Mwinyi alifungua mkutano wa majadiliano mahususi ya Zanzibar yanayohusu vyama vingi vya siasa.

Akizungumza Ikulu Zanzibar baada ya kuzindua kikosi kazi hicho, Dk. Mwinyi, alisema lengo na madhumuni ni kuendesha shughuli za kisiasa katika hali ya amani, umoja na mshikamano.

Alivipongeza vyama vya siasa vilivyoshiriki katika mkutano huo na makundi mengine ikiwamo asasi za kiraia na makundi mbalimbali ya kijamii ambayo yaliwakilishwa vyema katika mkutano huo.

"Nilipokea taarifa ya mambo yaliyojiri katika mkutano ule na kwa kweli yamepangwa vizuri ambayo yatatoa urahisi kwa kikosi kazi hiki kuyafanyia kazi na kuyapanga vyema na tayari yameshawekwa katika maeneo mbalimbali yanayohitaji kufanyiwa kazi," alisema.

Aidha, alisema ni imani yake timu hiyo ya watu 11 kwa uwezo wao, ubunifu na weledi waliokuwa nao hana shaka wataikamilisha kazi hiyo vyema ili serikali kupokea taarifa rasmi kutoka kwao.

Dk. Mwinyi aliwapongeza wajumbe wa kikosi kazi hicho kwa kuyafanya kazi ya kukusanya maoni ya wadau na kuwa na mapendekezo maalum serikalini.

Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Thabit Idarusi Faina, alisema kikosi kazi hicho pia kitapitia hotuba ya Makamu wa Kwanza aliyoitoa Oktoba 6, mwaka huu, wakati akifunga mkutano huo, kupitia nyaraka mbalimbali ikiwamo Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ya Zanzibar, sheria mbalimbali ikiwamo ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar.

Alisema pia kitapitia ripoti na machapisho yanayohusu malengo ya mkutano huo ili kupata uelewa mzuri wa maoni na mapendekezo ya wadau yaliyotolewa katika mkutano huo.

Faina alisema kikosi kazi pia kitapitia miafaka ya maridhiano yaliyoainishwa kuangalia mafanikio na matatizo katika utekelezaji wake.

Alisema kikosi kazi hicho kitatakiwa kufanya kazi na kuwasilisha ripoti katika muda uliowekwa wa siku 14 kuanzia jana hadi Oktoba 23, mwaka huu.

Msajili wa Vyama vya Siasa Tanzania, Jaji Francis Mutungi, alimpongeza Rais Mwinyi kwa kuitisha mkutano huo na kutoa agizo la kuundwa kwa kikosi kazi hicho ambacho kitakaa kuchakata maoni ya wadau waliyoyatoa katika mkutano huo.

Alisema Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ipo tayari kusaidia kwa lolote atakaloelekeza ili kudumisha amani, utulivu na umoja wa kitaifa nchini.

Mwenyekiti wa kikosi hicho, Ali Uki, alisema kikosi hicho ni tofauti na kikosi kazi kilichoundwa na Rais Samia Suluhu Hassan, kwamba kitafanya kazi kwa mujibu wa ripoti iliyotayarishwa kutokana na mkutano wa siku tatu wa demokrasia ya vyama vingi wa kujadili mambo mahsusi ya Zanzibar.

Alisema msingi mkuu wa kufanya kazi hiyo ni kuona kila kinachojadiliwa kina lengo la kuanzisha Zanzibar mpya, yenye amani, umoja na mshikamano.

Kikosi kazi hicho kinaongozwa na Mwenyekiti wake Ali Uki, Makamu Mwenyekiti, Balozi Amina Salum Ali, mjumbe kutoka CCM, Vuai Ali Vuai na mjumbe kutoka Chama cha ACT- Wazalendo, Jussa Ismail Ladhu.

Wengine ni kutoka CHADEMA, Said Issa Mohammed na mjumbe kutoka Chama cha Wananchi (CUF), Rukia Kassim Mohammed.

Wengine ni mjumbe kutoka Chama cha Demokrasia Makini, Ameir Hassan Ameir, Joseph Abdalla Meza kutoka sekta binafsi, mjumbe kutoka taasisi za kidini Padri Stalei Nikolas Nchinga, mjumbe kutoka wasomi, Professa Mohammed Makame Haji, mjumbe kutoka dini ya kiislamu, Shekhe Thabit Nomal Jongo.

## RIPOTI MAALUM

# Bwana harusi alivyouawa kwa risasi akivua samaki mgodini

### •Ni miezi miwili tangu kuuawa baba kichanga

**Na Mwandishi Wetu,** aliyekuwa KISHAPU

NI simulizi inayobeba simanzi na kiulizo kikuu kwa wakati mmoja, walinzi wa Mgodi wa Almasi El-Hilali wilayani Kishapu mkoani Shinyanga wameua vijana wawili kwa risasi katika matukio mawili ndani ya miezi miwili na wiki moja.

Wakati tukio la kwanza la Machi 10, mwaka huu ni la mauaji ya kijana Cosmas Hamis (23), aliyedaiwa kuingia ndani ya eneo la mgodi na hadi sasa kuna ukimya kuhusu hatua za kipolisi kuchukuliwa, Mei 19, mwaka huu mauaji yanayoshabihiana kwa kila kitu, ikiwamo silaha iliyotumika, yanashuhudiwa tena.

Safari hii kijana Hamis Mayunga (19) naye ameingia kwenye umauti kwa risasi ya bunduki kama ilivyokuwa kwa mtangulizi wake Cosmas, dai kuu ni kwenda kuvua samaki kwenye eneo hilo na aliyetangulia alikwenda kuchimba madini.

Katika hali hiyo ya kushabihiana, baada ya vifo, uchunguzi wa hospitalini hufanyika kisha wazazi wa marehemu wanapatiwa kwa kila tukio 'pole' ambayo kwa tukio la kifo cha Cosmas, polisi walitoa Sh. 100,000 na safari hii kwa Hamis zimetolewa Sh. 200,000 na Mkurugenzi wa Kampuni ya Samu Security, kwa mujibu wa kauli za wazazi waliopokea fedha hizo.

Ufanano mwingine unaojitokeza, vijana hao wote wawili wana wajihi unaoendana kuhusu nafasi zao, Cosmas alikuwa 'bado mbichi' kwenye ndoa yake, baba wa mtoto wa miezi minane, ilhali Hamis alikuwa katika hatua za mwisho za maandalizi ya ndoa yake iliyokuwa imebakisha miezi michache kufungwa.

Ripoti za hospitalini kuhusu matukio hayo, Hamis anaelezwa kifo chake kimetokana na kusababishwa na kinachotajwa kwa lugha ya kidaktari 'jeraha la kifuani', huku ripoti kama hiyo katika mauaji ya Cosmas ilitamka kitaalamu 'Hypovolemic shock secondary to penetrative wound'.

Ni msamiati wa kitabibu ambao ulipata tafsiri ya kitaalamu katika ripoti maalum ya Nipashe kuhusu mkasa huo wa Cosmas ya mwanzoni mwa Aprili, mwaka huu, ukimaanisha 'kupungua kwa damu mwilini kutokana na kuchomwa na kitu chenye nchi kali'.

Majumuisho ya matukio yote mawili ambayo Nipashe imekuwa shuhuda wa hatua mbalimbali, ikiwamo maziko yote, yanabeba sura yenye tafsiri ya unyonge kuanzia ngazi ya wazazi huku kukiwa na kiulizo cha utekelezaji wa haki dhidi ya watoto wao.

Mara zote Nipashe katika kufuatilia matukio hayo, imekuwa ikikutana na kitendawili cha wahusika mbalimbali wa msiba huo kukana kuhusika na kutoa fedha hizo za 'pole' isipokuwa wazazi peke yao kudumu kuwa na uwazi wamepokea fedha kutoka chanzo kipi.

**MKASA WA HAMIS**

Robert Mayunga (21), kaka wa Hamis, anasimulia ulivyokuwa mkasa wa kifo cha mdogo wake, akieleza: "Baada ya kusikia mlio wa risasi, ilibidi niingie ndani ya maji kwenye bwawa ambalo tulikuwa tunavua samaki, nikajificha humo.

"Walinzi walianza kunisaka kwa kumulika tochi, wakanikosa. Walipoondoka, ndipo nikatoka na kukimbia kwenda nyumbani. Kumbe ile risasi ilikuwa imempiga mdogo wangu!"



Mwenyekiti wa Kijiji cha Dulisi, Moses Nshimba (kushoto), akiwa na wazazi wa marehemu Hamis, Mayunga Inegele (katikati) na Shinje Ntemanya katika mazungumzo na Nipashe kijijini huko Septemba 28, mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Mfiwa huyo anayezungumza kwa sauti ya chini na kuna wakati anaangalia juu kwa uso wa simanzi, kuvuta kumbukumbu ya kilichojiri siku hiyo, anaendeleza simulizi yake kwamba:

"Ilikuwa Mei 19, mwaka huu majira ya saa moja jioni, tulipotoka hapa nyumbani (Kijiji cha Dulisi, Kata ya Sekebugolo wilayani Kishapu) mimi, mdogo wangu na vijana wenzetu wawili, kwenda kwenye bwawa la mgodi wa El-Hilali kuvua samaki.

"Tulipoingia ndani ya mgodi, tuliweka mitego yetu kwenye bwawa la mgodi huo ili kunasa samaki. Lile bwawa lina samaki wengi aina ya kambare.

"Ilipofika majira ya saa nne usiku, tukaenda kuota moto kwenye kambi yetu ambayo mara nyingi tulizoea kupumzika huko maeneo ya vichakani, bahati mbaya tulipofika huko wote tukapitiwa na usingizi.

"Ilipofika majira ya saa sita usiku, tukashtuka na kujikuta tayari tumeshawekwa chini ya ulinzi na walinzi wa mgodi, ndipo tukakurupuka kukimbia ili kujiokoa. Wakati wa purukushani hizo, ghafla nikasikia mlio wa risasi.

"Uamuzi wa haraka niliouchukua baada ya kusikia mlio wa risasi, ni kujirusha kwenye maji ya bwawa la mgodi, nikajificha humo hadi majira ya saa nane usiku nilipojiridhisha askari wameondoka kwenye eneo hilo."

Robert anasimulia kuwa baada ya kufika nyumbani majira hayo ya usiku wa manani, alimuuliza baba yao kama mdogo wake alikuwa amefika nyumbani kwa kuwa kila mmoja baada ya tukio hilo alikimbia kwa njia yake ili kujiokoa.

Anasema majibu aliyopata kutoka kwa mzazi wake ni kwamba, mdogo wake alikuwa hajafika nyumbani. Wote, yeye na baba yake, waliamua wasubiri mapambazuko ili wamtafute ndugu huyo.

Anaeleza kuwa asubuhi ilipotimu walisonga hadi mgodini kwenye bwawa hilo kumsaka mdogo wake na katika utafutaji wao, walimwona kwa mbali akiwa amelala chini, lakini ilishindikana kumfikia kwa kuwa gari la walinzi wa mgodi lilikuwa linaelekea eneo la tukio.

"Tulipobaini hali ile ilibidi tujifiche kwenye kichaka, wale askari walinzi wa mgodi wakauchukua mwili wa mdogo wangu, wakaondoka nao.

"Hiyo haikuwa mara ya kwanza kwetu kuingia mgodini, tulikuwa tunaingia mara kwa mara kuvua samaki na walinzi wanatufahamu kabisa, lakini tulishangaa siku hiyo, sijui walipatwa na nini, wakaamua kumuua mdogo wangu kwa kumpiga risasi," Robert anasimulia.

Baba mzazi wa marehemu Hamis, Mzee Mayunga Inegele, anabainisha huyo ni mtoto wake wa tano kati ya 11 na kwamba mwishoni mwa mwaka huu walikuwa wamepanga kumwozesha na taratibu zote za ndoa zilikuwa zimekamilika.

Mzee Inegele, babu wa wajukuu 17, anakitaja kifo cha mwanawe huyo ni cha kinyama na kimeiumiza familia yake inayoshangaa hadi sasa hakuna hatua za kisheria zilizochukuliwa dhidi ya waliotekeleza mauaji hayo.

Anasema amekuwa akishirikiana na uongozi wa kijiji na kata kufuatilia haki za mwanawe, lakini uongozi wa polisi mkoani Shinyanga unawapa majibu kwamba ili kufunguliwa kesi mahakamani, ni lazima mtuhumiwa wa mauaji hayo apatikane, akiuomba uongozi wa juu serikalini kuwasaidia kupata haki hiyo.

Anasema kuwa siku ya tukio wanawe wawili, wakiwa na wenzao wawili kutoka kijijini hapo anaowataja kwa majina Jibuta Jilalabe na Simoni Jilala, waliondoka nyumbani majira ya saa moja usiku kwenda kuvua samaki katika bwawa lililoko ndani ya Mgodi wa El-Hilali na kilichowakuta ni kile kilichosimuliwa na mwanawe Robert.

"Huyu Robert alipofika hapa nyumbani usiku, nilimuuliza 'kumetokea nini?' Ndipo akasema wamekimbizwa na walinzi wa mgodi, lakini mwenzao Hamis hawajamwona na walisikia mlio wa risasi.

Anasema kulipokucha alimwagiza Robert na mjomba wake wakamtafute ndugu yao na baada ya muda mfupi wakampatia taarifa Hamis alikuwa ameuawa kwa kupigwa risasi na mwili wake ulikuwa umechukuliwa na walinzi wa mgodi.

Anasema kuwa baada ya kupata taarifa hiyo, walikwenda Kituo cha Polisi Maganzo, wilayani Kishapu kufuatilia taarifa za kifo cha mtoto wake, wakaambiwa mwili wake ulikuwa umepelekwa Hospitali ya Mgodi wa Almasi Mwadui na walipokwenda huko, walijibiwa haukuwa katika hospitali hiyo.

"Baada ya kuukosa mwili wa kijana wangu pale Mwadui, walituambia umepelekwa Hospitali ya Kolandoto na tulipofika katika hospitali hiyo, tukaambiwa tena haukuwa pale, tukatakiwa twende mkoani (Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga).

"Yaani kuuona tu mwili wa mtoto wangu tulizungushwa kweli. Ili kujiridhisha kama ni wenyewe, tulitembea hospitali mbili hakuna mwili, hadi tulipofika Hospitali ya Mkoa tukaukuta katika chumba cha kuhifadhi maiti.

"Baada ya kuupata mwili wa mtoto wangu, hatukuwa na fedha ya kuusafirisha kwenda nyumbani kwa ajili ya mazishi, tukaomba msaada kwenye mgodi tukakosa, tukapewa Sh. 200,000 na Mkurugenzi wa Kampuni ya Ulinzi ya Samu, tukazitumia kwa usafiri na kununua jeneza.

"Tunaomba uongozi wa juu serikalini utusaidie kupata haki ya kifo cha mtoto wangu maana hadi leo (Septemba 28, 2022) hatujui nini kinaendelea. Tukifuatilia kwa Jeshi la Polisi tunazungushwa tu na kuambiwa ili kufunguliwa kesi hadi mtuhumiwa apatikane, tangu mwezi wa tano (Mei) hadi sasa eti hajakamatwa tu," anawasilisha kilio chao.

Mama mzazi wa Hamis, Shinje Ntemanya anaungana na mumewe kupaza sauti kutaka hatua zichukuliwe dhidi ya waliotekeleza mauaji hayo, akibainisha kuwa kifo cha mwanawe kimemwachia maumivu makali, hivyo "kuna haja haki itendeke".

ITAENDELEA KESHO

# PM akumbusha viongozi wa dini kuhubiri amani

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka viongozi wa dini na Watanzania kujenga utamaduni wa kuhubiri amani nchini wakati wote.

Alitoa rai hiyo juzi katika Msikiti wa Sunni Jamaat, Kisutu mkoani Dar es Salaam, wakati wa maadhimisho ya kumbukizi ya kuzaliwa kwa Mtume Muhammad (S.A.W).

"Mengi yamezungumzwa na viongozi wa dini akiwamo Mufti Aboubakar Zubeir, lakini Rais Samia Suluhu Hassan majira ya mchana (juzi) wakati wa maadhimisho kama haya pale Diamond Jubilee alisisitiza kuhusu kulinda amani ya nchi, hata Mtume Muhammad katika uhai wake alisisitiza suala la amani na umoja, basi ili kumuenzi hatuna budi kufuata mafundisho yake," alisema Majaliwa.

Pamoja na mambo mengine, Majaliwa alisisitiza suala la maadili kwa vijana na kusema kuwa baadhi yao wamekosa maadili, hivyo kuhatarisha amani iliyoko.

"Wazazi na viongozi wa dini hamna budi kukemea kwa nguvu zote viashiria vyote vya mmomonyoko wa maadili unaofanywa na vijana wetu. Kwa kufanya hivyo Tanzania itaendelea kuwa kisiwa cha amani," alisema Majaliwa.

Mufti wa Tanzania Shekhe Aboubakar Zubeir, alisema amani, umoja na upendo ni moja ya misingi ambayo Mtume Muhammad (S.A.W) aliwaachia Watanzania.

Alisema suala la amani Tanzania imelichukua kama tunu zake na Watanzania wote wanapaswa kuhakikisha wanaitunza amani iliyoko kwa gharama yoyote.

Aidha, aliwataka Waislamu nchini kuiunga mkono serikali katika utekelezaji wa miradi na mipango ya maendeleo kwa kufanya kazi kwa bidii.

"Suala la kufanya kazi pia limesisitizwa katika Quran takatifu na ndiyo msingi wa maendeleo ili kuwaunga mkono viongozi wetu wa nchi, hatuna budi kujituma kwa hali na mali katika shughuli za maendeleo ili kujikimu kimaisha na kulijenga taifa. Huo ndiyo wito na rai yangu kwenu wakati huu tunapo adhimisha kuzaliwa kwa Mtume (S.A.W)," alisema.

Balozi wa Hija nchini Tanzania, Shekhe Alhaj Marusu Msii, alisema viongozi wa dini wanapaswa kuhakikisha amani ya nchi inaendelea kuwapo.

Alisema pia wana jukumu la kuliombea taifa ili kulinusuru na majanga mbalimbali.

"Jukumu letu sisi na waumini wa Kiislam ni kuliombea taifa bila kuchoka na kuunga mkono juhudi zinazofanywa na serikali ya kuhakikisha amani hii tuliyoachiwa na watangulizi wetu ina dumu," alisema Alhaj Msii na kuongeza:

"Salamu zangu kwa siku ya leo ambayo ni adhimu sana kwetu nasema Mtume (S.A.W) aenziwe kwa yale mema yote aliyoagiza na kuacha yale yote aliyotukataza."

# Ugonjwa sonona unavyoathiri wanawake kiakili

**Na Elizabeth Zaya**

WATU milioni 1.5 nchini wanaishi na ugonjwa wa sonona huku wengi wao wakiwa wanawake.

Kauli hiyo ilitolewa jana Dar es Salaam na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, wakati wa Kongamano la Kwanza la Kitaifa la Afya ya Akili.

Alisema miongoni mwa dalili hatari za sonona ni kutosema changamoto zako kwa watu.

"Lakini hapa nahitaji pia tufanye takwimu kwa sababu tunaambiwa moja ya dalili ya hatari ya sonona ni kutosema changamoto zako kwa watu. Na wanawake tumekuwa wepesi kushirikisha watu changamoto zetu, kwa hiyo tunapoambiwa kwamba wanawake ndiyo tunaongoza ni vyema tutizame ni watu wapi zaidi wanaathirika na hili," alisema Ummy.

Alisema Tanzania inakadiriwa kuwa na watu milioni saba wenye magonjwa mbalimbali ya akili, ikiwamo yanayotokana na matumizi ya dawa za kulevya, magonjwa ya akili mengi yaliyoko nchini ni yatokanayo na sonona, kihoro, sikozoflenia, matumizi ya bangi na pombe kupita kiasi.

"Na kuna uhusiano mkubwa na wa karibu kati ya afya ya akili na ukuaji wa uchumi katika ngazi ya mtu mmoja, familia, jamii na taifa kwa ujumla. Yapo magonjwa ya akili ambayo yanaathiri katika kufikiri, kuhisi, kutambua na kutenda na hivyo kuwa na mabadiliko ya kitabia na mwenendo ulio tofauti au usioendana na jamii husika, kiimani, kimila, kidesturi na nyanja nyingine za jamii," alisema Ummy.

"Tabia hizo zinatokana na ugonjwa wa akili kuathiri ufanisi wa shughuli za mtu husika pamoja na uhusiano wake na hata kuathiri jamii nzima inayomzunguka."

Aliongeza kuwa, matukio ya kujiua ni moja kati ya sababu ya nne ya vifo vya vijana wenye umri wa miaka 15 mpaka 29.

Waziri huyo wa Afya alisema ni muhimu Bima ya Afya ikakubali kugharamia wenye afya ya akili ili kuwasaidia kupata matibabu kwa urahisi.


**AKIBA COMMERCIAL BANK PLC**
**Company No. 22797**

## NOTICE FOR CONVENING AN EXTRA ORDINARY GENERAL MEETING

**NOTICE IS HEREBY GIVEN THAT AN EXTRA ORDINARY GENERAL MEETING OF AKIBA COMMERCIAL BANK PLC SHALL BE HELD ON SATURDAY, 12TH NOVEMBER 2022 AT DAR ES SALAAM SERENA HOTEL FROM 10:00 AM (EAT)**

**AGENDA:**

**1.0 NOTICE, CONFIRMATION OF QUORUM AND ADOPTION OF THE AGENDA**
**2.0 TO RECEIVE AND APPROVE PROPOSAL FOR CAPITAL ENHANCEMENT**
**3.0 CLOSING REMARKS**

**By Order of the Board**

Niwaeli Mziray
**Company Secretary**

**Distribution:** Shareholders - Akiba Commercial Bank Plc

**Invitees:** Board of Directors - Akiba Commercial Bank Plc
Senior Management - Akiba Commercial Bank Plc
Director, Banks Supervision Department - Bank of Tanzania

**NOTE:**

**A. PAPERS FOR THE MEETING**
Papers for the meetings will be available for collection at the Bank's Registered Offices from Tuesday, 1st November 2022 and at the venue on the date of the meeting.

**B. OPTION TO JOIN VIRTUALLY**
Shareholders may join the meeting virtually if unable to attend physically, by notifying the Company Secretary to register their virtual attendance and obtain meeting access before **Thursday, 10th November 2022.** The meeting can be accessed virtually only by Shareholders who have registered their attendance.

**C. ATTENDANCE BY PROXY**
A Shareholder entitled to attend and vote at these meetings may, if unable to attend in person, appoint a proxy to attend and vote on his/her behalf in accordance with the provisions of the Articles of the Company.

The instrument appointing a proxy must be signed by the respective Shareholder.

The instrument appointing a proxy must be submitted to the Company Secretary at the Bank's registered office or via email by 10.00 a.m. (EAT) **Thursday, 10th November 2022.**

**D. TRAVEL AND ACCOMMODATION**
Each Shareholder shall be responsible for the cost of their own travel and accommodation.

**E. OTHER INFORMATION**
Shareholders are reminded to confirm/update their personal information with the Company Secretary in order to update the Company Register.

**F. CONTACT DETAILS FOR COMMUNICATION**

**Company Secretary**
**Akiba Commercial Bank Plc**
**3rd Floor, Amani Place, Ohio Street**
**P.O. Box 669**
**Dar es Salaam**

**Tel: 0742 972 072 or 0677 152 000**
**Email: cs@acbtz.com or niwaeli.mziray@acbtz.com**

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Ujio wa Rais Ruto nchini udumishe udugu

**RAIS** wa Kenya, Dk. William Ruto, amefanya ziara yake nchini Tanzania ikiwa ni taifa la kwanza kwa Afrika Mashariki kulitembelea tangu alipoapishwa rasmi Septemba 13.

Kwetu sisi ni heshima kubwa kuteuliwa kuwa nchi ya kwanza kwa Rais huyo wa awamu ya tano nchini Kenya kuja Tanzania tukiamini kuwa anatuamini na kutuweka kwenye orodha ya ndugu, majirani na washirika muhimu tunaotegemeana.

Rais Ruto alitangazwa kuwa mshindi wa kiti hicho katika uchaguzi uliokuwa na ushindani mkubwa dhidi ya mpinzani wake Raila Odinga, ambaye baada ya kutangazwa kwa matokeo aliyapinga mahakamani na kuomba yarudiwe kuhesabiwa, lakini ushindi ukabaki kwa Ruto.

Nchi hizi mbili zimekuwa na ushirikiano mkubwa hasa kwa raia wake ambao pamoja na kuwa marafiki, lakini kuwa na fursa ya kufanyakazi.

Kenya ni kaka mkubwa katika ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na mdau mkuu wa kibiashara na Tanzania ambaye amewekeza vitega uchumi vingi nchini na kuwezesha upatikanaji wa bidhaa muhimu kuendelea kuwapo.

Mshirika huyu mkuu kibiashara ana nafasi ya kipekee kwani kuzungumza Kiswahili kunaongeza ujirani baina ya raia wetu na hili ni jambo lingine linalozifanya nchi hizi kuwa na ushirikiano wa kitamaduni na hata maingiliano ya kiutamaduni.

Kwa msisitizo ushirikiano wa kibiashara pia umekuwa mkubwa kutokana na bidhaa zinazotengenezwa kutoka nchi hizo mbili kuuzwa bila tatizo na wafanyabiashara wakifurahia uwekezaji na uzalishaji.

Ukitembelea maduka mengi ya Tanzania lazima utakutana na bidhaa za Kenya na vivyo hivyo kwa upande wa Kenya, bidhaa za Tanzania hasa kwa upande wa vyakula vya nafaka vina soko na vinakubalika.

Matumizi ya lugha ya Kiswahili, kinachozungumzwa na nchi nyingi za Afrika na pia kupitishwa kuwa lugha rasmi kwa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kuzipa Tanzania na Kenya jukumu la pamoja na kuiendeleza lugha hiyo kimkakati.

Rais Samia Suluhu Hassan, alipokwenda nchini Kenya kushuhudia uapisho wa Rais Ruto, alibatizwa jina la Shangazi wa Afrika Mashariki, ni kielelezo kuwa anapewa heshima kubwa na marais wa nchi wanachama wa jumuiya hiyo kwa kuwa ndiye mwanamke pekee rais katika nchi hizo, ambaye pamoja na jukumu la kuongoza pia anasimamia uwapo wa biashara huru na yenye tija katika ukanda huu.

Rais Ruto kuiteua Tanzania kuwa nchi ya kwanza kuizuru Afrika Mashariki, inaweza kuwa ni sababu ya heshima anayompa Rais Samia na kuonyesha nia yake ya kujenga ushirikiano imara kati ya nchi hizo mbili majirani na marafiki.

Katika mazungumzo yao, marais hao wamekubaliana kuendelea kushirikiana kuondoa vikwazo ambavyo vinakwamisha biashara kati ya mataifa hayo mawili kusonga mbele.

Vile vile, suala la usalama katika mipaka ya majirani hao limepewa kipaumbele kuwa ni jambo muhimu katika kuzifanya nchi hizo zisonge mbele kimaendeleo na kudumisha amani na ushirikiano.

Tunaoumbea udugu na umoja kati ya mataifa haya udumu kwa kuwa bila Tanzania, Kenya haiwezi kuwa mshirika mkuu kibiashara na kiuchumi kadhalika bila Kenya, Tanzania haiwezi kujivunia mafanikio.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

## Kuweka elimu kujitegemea ndiko kumuenzi Mwl. Nyerere

**IMETIMIA** miaka 23 tangu Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, alipofariki dunia, huku akiicha Tanzania ikiwa kwenye mikono ya viongozi wengine waliofuata baada yake.

Pamoja na kwamba Baba wa Taifa hayupo, ninaamini kwamba, fikra, mawazo na falsafa zake bado zinaendelea kuishi katika vichwa vya Watanzania wenye mapenzi mema na nchi yao na kimsingi, alijaliwa kuwa na uwezo wa mawazo na kuyafanyia kazi kwa vitendo na kupata matokeo na pia alikuwa na ujuzi wa kubadili fikra hizo kuwa uhalisia ambao unaweza kuonekana hata leo.

Yapo mawazo na fikra zake nyingi, miongoni mwake ilikuwa ni kutamani kuyaona nayo ni elimu inayolingana na uhitaji wa jamii, huku akitilia mkazo iwe ya kujitegemea, kwa kuwa alikuwa anatambua umuhimu wake.

Kwa waliobahatika kupata elimu ya kujitegemea, watakumbuka kuwa huo ulikuwa ni mwanzo kuhusu mfumo wa elimu ulioendana na uhalisia wa jamii iliyokuwapo wakati na baada ya uhuru.

Hiyo ilitokana na ukweli kwamba, aliamini elimu hiyo ingekuwa ufunguo wa ujenzi wa jamii mpya ya Watanzania ambao walikuwa wamenaswa na makucha ya wakoloni.

Ili kutimiza lengo hilo katika elimu, aliamua kupitia sera ya vijiji vya ujamaa wale wote wanaopata elimu, wanapohitimu warudi vijijini kwao watumie elimu waliopata kuleta maendeleo.

Kwa ujumla ni kwamba, elimu ina jukumu muhimu katika maisha ya kila siku kwani inasaidia kuwafanya vijana kuwa na ujuzi ambao wanaweza kuutumia vizuri na kujiletea maendeleo

Ninadhani Baba wa Taifa aliona mbali alipoanzisha elimu hiyo, ili kwamba mwanafunzi anapohitimu, awe na kitu cha kufanya kupitia elimu aliyopata, ili aweze kunufaika nayo na kuinufaisha jamii yake pia.

Lakini sasa baadhi ya wanafunzi wanasoma na kuhitimu, kisha wanarudi nyumbani kwao kugeuka kuwa mzigo kwa familia zao badala ya kuwa suluhisho la matatizo ya jamii kupitia elimu aliyopata.

**Kwa ujumla ni kwamba, elimu ina jukumu muhimu katika maisha ya kila siku kwani inasaidia kuwafanya vijana kuwa na ujuzi ambao wanaweza kuutumia vizuri na kujiletea maendeleo**

Kwa mfumo huo wa elimu ya kujitegemea, alitamani wasomi waitumikie jamii, wakati serikali, baada ya wazazi na walezi kutoa fedha na rasilimali nyingi kuwasomesha, hivyo walikuwa na deni la kulipa kwa kuitumikia jamii.

Wakati huu Tanzania inapoadhimisha kumbukumbu ya miaka 23 ya kifo chake, ni vyema akaenziwe kwa kurejesha elimu ya kujitegemea ili kuwafanya wasomi wa sasa kuwa sehemu ya jamii.

Badala ya kuelimika na kwenda kujichimbia kwingine au kuzunguka kupata ajira, basi wakishapata elimu warudi katika jamii waliyotoka kusaidia kuleta maendeleo na si kujitenga na kujiona hawawezi kushirikiana na jamii yao.

Ikumbukwe kwamba kile ambacho Baba wa Taifa alikusudia kwenye elimu, ni kuitafuta na kupata maarifa ambayo ni suluhisho la matatizo yanayowakabili watu na yeye mwenyewe.

Ukweli ni kwamba mchakato wa elimu ya kujitegemea kwa undani wake unaweza kupata mambo mengi ya kuvutia uhusiano na sifa za kibinadamu, fursa, tamaa na mahitaji kwa ajili ya maendeleo yake na jamii inayomzunguka.

Mtu anaweza kupata ujuzi ikiwamo ualimu akaenda katika jamii akasaidia kuondoa adui ujinga, mwingine anaweza kupata ujuzi wa udaktari na fani nyingine nyingi za kuweza kusaidia kwenye jamii yake.

Hivyo, kwa ujumla wake elimu ya kujitegemea inaweza kupunguza wahitimu kuzunguka na vyeti katika ofisi mbalimbali kutafuta kazi, badala yake watatumia ujuzi waliopata kujiajiri, pongezi

serikali kwa kujitahidi kujenga vyuo vya ufundi kila kata, kwani bila kufanya mabadiliko kama hayo, tunaweza kuendelea kuzalisha wasomi wengi ambao haiwezi kuwa na msaada au kutatua matatizo katika jamii yao.

## Watoto 4 raia wa Burundi wahukumiwa kifungo cha nje, wiki 2 kurudishwa kwao

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imewahukumu watoto wanne raia wa Burundi kifungo cha nje cha mwaka mmoja na kutoa wiki mbili kwa upande wa Jamhuri kufanya utaratibu wa kuwarudisha nchini mwao ili wakaungane na wazazi wao.

Watoto hao (majina yanahifadhiwa) wanatuhumiwa kwa makosa mawili ya kuingia na kuishi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila Visa au nyaraka yoyote inayowaruhusu kuishi nchini.

Hukumu hiyo ilisomwa jana na Hakimu Mkazi Mwandamizi, Francis Mhina, baada ya raia hao kukiri makosa yao na mahakama kuwatia hatiani kwa kuingia na kuishi nchini bila kibali.

Alisema raia hao wanne ni watoto ambao wana umri chini ya miaka 18 ana wahukumu kifungo cha nje cha mwaka mmoja.

Pia alisema watoto hao watarudishwa kwao nchini Burundi kwa mujibu wa Sheria ya Uhamiaji na pia ametoa wiki mbili kwa upande wa Jamhuri kufanya utaratibu wa kuwarudisha kwao ili kuungana na wazazi wao.

Awali, Wakili wa Serikali kutoka Idara ya Uhamiaji, Hadija Masoud na upande wa Ustawi wa Jamii, Warida Juma waliiomba Mahakama iwaachie huru ili wakaungane na familia zao.

Pia Mahakama hiyo imemhukumu Eric Ibigilimana, Mtrambekula Ayoub na Roselimana Randinyo, kulipa faini ya Sh. 500,000 kwa kila kosa na wakishindwa watatumikia kifungo cha miezi mitatu jela.

Ilidaiwa Oktoba 6, 2022 washtakiwa walikutwa wakiishi katika nyumba iliyoko mtaa wa Mchikichini, Kariakoo Wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam na kupelekwa Ofisi ya Uhamiaji Ilala na kukiri kutenda makosa hayo.



Wafanyakazi wa Benki ya Azania wakiongozwa na Meneja wa benki hiyo tawi la Geita, Rhoda Baluhya (mwenye suti nyeusi), wakisherehekea ushindi katika kundi la taasisi za fedha wakati wa Maonesho ya 5 ya Kitaifa ya Teknolojia na Madini yaliyofanyika kitaifa mkoani Geita na kuhitimishwa mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Pindi aipa maelekezo ma5 Bodi ya Misitu

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, ametoa maelekezo matano kwa Bodi ya Wadhamini wa Mfuko wa Misitu Tanzania ikiwamo kuwezesha miradi ya uzalishaji wa mkaa mbadala kama sehemu ya kupunguza ukataji miti kwa ajili ya kuni na mkaa.

Maelekezo hayo yalitokana na maeneo ya misitu kukabiliwa na wimbi la uvamizi kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kibinadamu.

Dk. Chana alitoa maelekezo hayo wakati wa hotuba yake kwenye uzinduzi wa bodi ya tatu ya wadhamini wa Mfuko wa Misitu Tanzania uliofanyika jijini hapo jana.

"Natoa rai kwa bodi kuandaa utaratibu mzuri wa kushirikisha sekta binafsi, kuwezesha miradi ya uzalishaji wa mkaa mbadala kama sehemu ya kupunguza ukataji miti kwa ajili ya kuni na mkaa," alisema.

Alibanisha kuwa serikali inahimiza ushirikishwaji wa sekta binafsi katika kukuza uchumi na imeweka mkazo uhifadhi wa maliasili na utunzaji wa mazingira.

Kadhalika uwapo Mfuko wa Misitu Tanzania ni mojawapo wa jitihada za kutatua changamoto hizo kwa lengo la kuendeleza uhifadhi wa rasilimali misitu kwa manufaa ya kizazi kilichoko na vizazi vijavyo.

Pia aliagiza kuwezesha miradi ya kuongezea thamani mazao ya misitu na nyuki katika maeneo yote yaliyohifadhiwa na kuwezesha miradi ya kimkakati ambayo ina tija katika uhifadhi na uendelezaji wa rasilimali misitu.

Agizo lingine ni kuboresha utaratibu wa utoaji wa ruzuku kwa kuangalia uwezekano wa kutoa fedha ambazo zitarejeshwa na kupewa wadau wengine.

Alisema jukumu la kusimamia Mfuko wa Misitu Tanzania ni zito, lakini pamoja na uzito wa jukumu hilo, wizara ina matumaini makubwa kuwa bodi hiyo itasimamia mfuko kwa uadilifu, uaminifu na ufanisi.

Alisema nchi imejaliwa kuwa na misitu inayokadiriwa kuwa hekta milioni 48.1 ambazo zinachukua theluthi moja ya ukubwa eneo la nchi.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Juma Mkoni, alisema Bodi ya Wadhamini ya TaFF ni ya tatu kuanzishwa.

Alisema katika kipindi cha miaka 10 ya utendaji wake kuanzia mwaka 2011/2012 hadi 2021/2022, Mfuko umefanikiwa kukusanya Sh. bilioni 62.26.

Fedha hizo zimetumika kugharamia utekelezaji wa majukumu ya mfuko ikiwa ni pamoja na kutoa ruzuku kwa miradi 738 inayotekelezwa katika mikoa yote ya Tanzania Bara na miradi hiyo inachangia usimamizi na uendelezaji wa misitu na kuboresha uhifadhi wa rasilimali misitu.

## KABWELA



# LHRC yataja sababu 4 kupinga adhabu ya kifo

**Na Sabato Kasika**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimetoa sababu nne za kutaka adhabu ya kifo ifutwe nchini, ambazo kinaamini serikali inaweza kushawishika na kuchukua hatua.

Mkurugenzi Mtendaji wa kituo hicho, Anna Henga, alitoa sababu hizo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kupinga Adhabu ya Kifo.

Alitaja sababu ya kwanza kuwa adhabu ya kifo hairekebishi tabia ya aliyetenda kosa na kwamba mtu aliyetenda kosa la mauaji baada ya kuhukumiwa kifo, hawezi kuwa na nafasi ya kurekebisha tabia yake na jamii inayomzunguka.

"Adhabu hiyo ni sawa na kulipiza kisasi badala ya kurekebisha mhalifu, hivyo ni sahihi kusema kwamba adhabu haifanyi watu wabaya kuwa wazuri katika jamii, kuna uwezekano mkubwa wa makosa yanayoadhibiwa na adhabu hii kuendelea siku hadi siku," alisema Henga.

Alitaja sababu ya pili ya kupinga adhabu hiyo kuwa haitoi unafuu au msaada kwa upande wa waliotendewa kosa badala yake mtendaji wa kosa kuhukumiwa adhabu hiyo kwa kunyongwa hadi kufa.

"Sababu ya tatu, adhabu ya kifo hairekebishiki. Kumekuwa na mifano mingi katika nchi mbalimbali ulimwenguni ambapo watu walinyongwa hadi kufa kwa maamuzi ya mahakama na baadaye kuthibitika kwamba hawakutenda makosa yaliyosababisha adhabu ya kifo," alisema.

Alitaja sababu ya nne kuwa uwapo wa adhabu hiyo haufanyi watu waogope kutenda makosa, badala yake inaongeza maumivu kwa jamii hasa kwa familia za wafiwa.

"Katika misingi ya haki za binadamu, adhabu hiyo inapingana na haki ya kuishi na kwa upande mwingine, adhabu ya kifo sio adhabu tu bali ni kitendo ambacho huharibu kabisa maisha ya mwanadamu ambayo hayawezi kurejelewa hata pale itakapogundulika ilitekelezwa kwa makosa," alisema.

Henga alisema wana sababu nyingi za kupinga adhabu ya kifo, lakini wametaja hizo nne ambazo wameona zinatosha kuishawishi serikali kuchukua hatua za kuondoa adhabu hiyo nchini.

"Ni wakati mwafaka sasa kwa serikali kufuta adhabu hii kwani Tanzania ni nchi ya kidemokrasia inayofuata misingi ya haki za binadamu, lakini adhabu hii ina mizizi ya kikoloni ambayo kimsingi ilikuwa ni ya kinyonyaji, uonevu na ukatili, hivyo haifai kuendelea kuwapo," alisema.

Vile vile, alisema kituo hicho kinaona kuna haja kufanyika kwa marekebisho ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu ili kuondoa vifungu vilivyoweka adhabu ya kifo, kulinda haki ya kuishi, kwa kuweka adhabu mbadala," alisema.

Alisema mwaka 1992, ripoti ya Tume ya Jaji Nyalali iliwahi kutoa mapendekezo ya kufanya marekebisho ya sheria, ili kuondoa adhabu ya kifo kwa kuwa ni ya kikoloni.

"Wakati wa uongozi wa awamu ya tano, wafungwa wote wa hukumu ya kifo walisamehewa na adhabu yao ilibadilishwa kutoka kifo hadi kifungo cha maisha, adhabu hii ilipokelewa vyema na kituo chetu," alisema.

Alisema adhabu hiyo inatweza utu wa mtu na kuvunja haki ya kuishi kama ilivyoainishwa katika Mikataba ya Kimataifa na Kikanda ya Haki za Binadamu.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani), jijini Dar es Salaam jana kuhusu maadhimisho ya 20 ya Siku ya Kimataifa ya Kupinga Adhabu ya Kifo. Kulia ni Mkurugenzi wa Uchechemuzi na Maboresho wa kituo hicho, Fulgence Massawe. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Upelelezi wakwamisha kesi Sabaya kuendelea

**Na Mary Mosha,** MOSHI

UPANDE wa utetezi katika kesi inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya umeuomba upande wa Jamhuri kuharakisha upelelezi kulingana na mwongozo unaotaka kukamilika ndani ya siku 90.

Mwongozo huo uliotolewa mwaka 2022 unautaka upelelezi ukamilike ndani ya siku 90 na unaelekeza kuanza kutumika Oktoba mosi, mwaka huu.

Mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Mwandamizi wa Mahakama hiyo, Salome Mshasha, Wakili wa Utetezi, Hellen Mahuna, aliomba busara ya mhimili huo na kwamba mteja wao tayari amekaa magereza zaidi ya siku 130.

"Tunaomba mahakama hii tukufu kuangalia mwongozo unavyoelekeza ili kusaidia upatikanaji wa haki kwa mteja wetu ikiwa ni pamoja na kuharakisha ushahidi," alidai.

Awali, Wakili wa Serikali, Susan Kimaro, akiambatana na Wakili Nasri Kasimu, aliiomba mahakama kupanga tarehe nyingine ya kutajwa kwa kesi hiyo kwa kuwa upelelezi haujakamilika.

"Niiombe mahakama yako ipange tarehe nyingine ya kutajwa kwa kesi hii, bado upelelezi haujakamilika, lazima upande wa utetezi utambue juhudi zilizofanywa ukizingatia kesi hili ilikuwa na wastakiwa watano na kwa sasa yupo mmoja, hii ni hatua kubwa," alisema.

"Pia, mwongozo unatuongoza kesi hii iwe ndani ya siku 90 na umeanza 1/10/2022 hivyo tupo ndani ya muda na tuna imani ndani ya siku 90 tutakuwa tumefika mbali au kukamilisha upelelezi," alisema.

Akijibu maombi ya upande wa utetezi, Hakimu Salome alitaka upande wa utetezi kusoma mwongozo vyema kwa kuwa Jamhuri walianza kufanyakazi ndani ya mwezi huu na kuwa wako ndani ya muda.

Kesi hiyo ilihairishwa hadi Oktoba 24, mwaka huu, na Sabaya alipelekwa gerezani.

# Stempu, Posta kiganjani vyarahisisha huduma

**Na Golden Kisapile, TUDARCo**

SHIRIKA la Posta Tanzania limezindua mfumo wa posta kiganjani na stempu mpya kati ya Tanzania na Omani zenye vivutio vya utalii vinavyopatikana nchini.

Akizindua mfumo na stempu hizo jijini Dar es Salaam, Waziri wa Habari na Mawasiliano na Tekonolojia ya Habari, Nape Nnauye, amesema serikali itaendelea kuliwezesha Shirika la Posta kufikisha huduma maeneo ya pembezoni.

"Pia kuna mabadiliko na mageuzi makubwa kwenye posta ya sasa kwa sababu huduma zetu zinakwenda kupatikana kidijitali kwenye simu janja," alisema Nnauye na kuongeza:

"Ni kumbukumbu muhimu ya wadau wa siku ya posta duniani, nawapongeza wadau wote wa posta kwa kuadhimisha siku hii ya posta duniani yapo mabadiliko mengi kama vile huduma ya posta kiganjani ambayo inaweza kuwafikia Watanzania, hivyo ukipeleka kiganjani maana yake umemfikia kila mtu,"

Kwa mujibu wa Waziri huyo, takwimu za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), simu zinazotumika ni milioni 58 huku watumiaji wa intaneti ni milioni 37 ambao hufanya uamuzi mtandaoni.

Alisema miundombinu ya posta kiganjani inaweza kuwahudumia wananchi wengi kwa muda mfupi na kuchangia kasi ya ukuaji biashara kwa ujumla.

"Hili limejionesha wazi likiwa ni pamoja la duka mtandao la posta, ambalo litaleta mabadiliko katika watumiaji wa huduma hii, ukitumia mfumo huu utaweza kupeleka bidhaa yako kwenye maduka 800 kwa wafanyabiashara wakubwa na wadogo," alisema.

Nnauye alisema kujiunga kwenye duka la posta ni bure na mtu anaweza kupeleka bidhaa zake duniani kote, jambo litakalorahisisha wanunuzi kufanya uamuzi na kukuza uchumi wao na nchi kwa ujumla.

Aidha, alisema stempu hizo mpya zitasaidia kutangaza utalii nje ya nchi kwa kuwa kutakuwa na mivutio vyote vinavyopatikana.

Awali, Posta Msta Mkuu, Macrice Mbodo, alisema huduma mpya zimerahisisha kwa taasisi zinazotoa huduma kama Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Mamalaka ya Usajili wa Vizazi na Vifo (RITA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Jeshi la Uhamiaji.

Alisema kwenye sekta ya elimu posta inasafirisha vitabu kwenda shule mbalimbali jambo linalowarahisishia wanafunzi wa kidato cha sita kutuma maombi Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB).

## Hukumu ya anayedaiwa kuua na kuzika mwili Okt. 17

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, inatarajia kutoa hukumu dhidi ya mshtakiwa Hemed Ally, Oktoba 17, mwaka huu, kwa tuhuma za kumuua Farihani Maluni eneo la Sharif Shamba, Ilala, Dar es Salaam na kumzika mbele ya nyumba aliyokuwa akiishi.

Kesi hiyo ililetwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Joyce Minde wa mahakama hiyo kwa ajili ya majumuisho ya mwisho.

Upande wa mashtaka ulifunga ushahidi wake kwa mashahidi zaidi ya wanane na vielelezo kadhaa ikiwamo godoro linalodaiwa kufungwa pamoja na mwili wa marehemu Maluni na kisha kufukiwa ardhini.

Kwa upande wa utetezi, mshtakiwa Ally alijitetea mwenyewe huku akiongozwa na wakili wake, Caroline Kigembe na kudai siku inayodaiwa alimuua Maluni, alikuwa mahabusu kwa tuhuma za kupotea kwa marehemu.

Awali, Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Binadamu na vifo vya mashaka, Innocent Mosha, alidai kuwa Maluni kabla ya kuuawa na kufukiwa alifungwa kamba ya katani mikononi na kichwani alifungwa plasta.

Aidha, alidai kuwa haikuwa rahisi kujua chanzo cha kifo cha Maluni, lakini kutokana na uwapo wa plasta eneo la fuvu alihisi aliuawa kwa kuzibwa mdomo na kumsababishia akose pumzi.

Alidai kuwa Februari 9, 2015 akiwa katika eneo lake la Hospitali ya Taifa Muhimbili alipelekewa taarifa na RCO wa Ilala ikimtaka kwenda Sharif Shamba, Ilala kuchunguza mwili wa binadamu unaohisiwa kufunikwa ndani ya ua wa nyumba.

Akiongozwa na Wakili wa Wakili Serikali, Salome Asey, Dk. Mosha alidai alichukua vifaa vyote vya kazi na kuongozana na askari polisi hadi eneo la tukio.

Alidai walipofika eneo hilo majira ya saa sita kasoro mchana, alikuta vijana wakiwa wameshaanza kufukua eneo hilo, ndani ya shimo walikuta matofali mapya, masalia ya mwili yaliyokuwa yamezungushiwa ndani ya godoro, huku mikono ya masalia ya mwili ikionekana kufungwa kwa katani na fuvu likiwa na plasta.

Inadaiwa Juni mwaka 2014 Hemed Ally alimuua Farihani Maluni eneo la Sharif Shamba na kumzika mbele ya nyumba aliyokuwa akiishi.

# Wawekezaji watakiwa kuzingatia malengo ya ardhi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, amesema wawekezaji wanatakiwa kuzingatia malengo ya ardhi waliyopewa badala ya kufanyia matumizi mengine tofauti na walivyoomba.

Kikwete aliyasema hayo juzi mjini hapo alipotembelea Maonesho ya Biashara na Uwekezaji yaliyoandaliwa na Mkoa wa Pwani kwa kushirikiana na Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO), Kanda ya Mashariki.

Aliwataka wawekezaji wanaochukua ardhi kwa ajili ya uwekezaji kuitumia vizuri kwa kuiga wengine ambao wameendeleza maeneo yao akiwamo Said Bakhresa, ambaye ameanza uzalishaji katika kiwanda cha sukari alichojenga Bagamoyo, mkoani Pwani baada ya kupatiwa ardhi.

Aliwaagiza watendaji Idara ya Ardhi kuhakikisha viwanda vyote vilivyoko mkoa huo vinatambulika na ambao hawana hatimiliki wapatiwe.

"Kipaumbele kimojawapo cha Rais ni uwekezaji na sisi ndiyo tunatoa hati, anayepewa ardhi anatakiwa aiendeleze na kuzingatia lengo, niwapongeze wale ambao mnafanya yale ambayo yameelekezwa na Rais," alisema.

Kikwete pia aliwaelekeza watendaji wa wizara hiyo kuwa sehemu ya suluhisho la matatizo ya wananchi upande wa malalamiko kwa kuwapa ushirikiano na ikiwezekana kufika kwenye eneo badala ya kukaa ofisini na kutoa majibu ambayo hayaleti matokeo chanya.

"Watu wanapokuja na matatizo wewe unatakiwa kuwa sehemu ya kusuluhisha sio anakueleza tatizo lake wewe unamjibu tu bila kujua chanzo na kutafuta njia ya kulimaliza, wizara hii lazima iwe sehemu ya suluhisho nendeni kwenye maeneo yenye migogoro," alisisitiza.

Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Pwani, Hussein Idd, alisema katika siku za maonyesho hayo zaidi ya hati 150 zilitolewa na zipo zilizokamilishwa.

Aliwataka wananchi kufika kwenye ofisi za idara hiyo kwa Mkoa wa Pwani kuchukua hati zao.



Meneja wa Benki ya Absa Tawi la Moshi, Pendo Abdallah (katikati), akikabidhi zawadi kwa Meneja wa Fedha wa Kampuni ya Uuzaji na Usambazaji Kahawa ya Rafiki Coffee Limited, Edwin Mlay, wakati wa kuadhimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja, mkoani Kilimanjaro juzi. Kulia ni Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano wa Absa Tanzania, Aron Luhanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mradi maji Bangulo kunufaisha kaya za pembezoni

**Na Joseph Mwendapole**

WAKAZI zaidi ya 2,000 wa Kata za Gongo la Mboto, Pugu Station, Kinyerezi na maeneo jirani ya Bangulo wilayani Ilala, jijini Dar es Salaam, wanatarajiwa kunufaika na huduma ya maji kupitia mradi wa maji Bangulo.

Mradi huo unaotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), unatarajiwa kukamilika Novemba, mwaka huu.

Akizungumza mwishoni mwa wiki kuhusu utekelezaji wa mradi huo, Mhandisi wa DAWASA-Kinyerezi, Zephania Massaga, alisema utekelezaji wa mradi umehusisha kazi mbalimbali ikiwamo uchimbaji na ulazaji wa bomba za inchi 8,6,4,3,2 na 1.5 kwa umbali wa zaidi ya kilomita 20 na uligharimu Sh. milioni 550.

"Utekelezaji wa mradi huo, unatarajiwa kukamilika Novemba 2022 na wananchi wa maeneo tajwa watanufaika na huduma ya uhakika ya majisafi kutoka DAWASA," alisema Mhandisi Massaga.

Alisema pia mradi wa maji Bangulo B utanufaisha wakazi wa mitaa ya Ulongoni B, Mwembe Supu, kwa Pepepeteka, Bangulo Mwembe Kiboko, Bangulo Shule ya Msingi na Kifuru kwa Asha Madenge.

Mwenyekiti wa Kata ya Bangulo, Ashraf Mwakanosya, alisema wananchi wa maeneo unakopita mradi huo wamepata faraja kubwa na wana matumaini makubwa ya huduma hivi karibuni.

"Tuipongeze serikali kupitia DAWASA kwa uamuzi wa kutekeleza mradi huu ambao utaondoa changamoto ya huduma ya maji kwa wakazi wote, tunapata matumaini ya huduma ya maji kwa kazi tunazojionea zinaendelea kutekelezwa sasa," alisema Mwakanosya.

Alitoa wito kwa wananchi kuwa na subira wakati Mamlaka ikiendelea na utekelezaji wa mradi huo na kuwa walinzi wa miundombinu inayowekwa katika maeneo yao kwa kutoa taarifa wanapobaini hujuma.

Mkazi wa Mtaa wa Bangulo Mwembe, Kiboko Rashidi, alitoa pongezi zake kwa serikali kuwasogezea huduma ya maji jambo ambalo limesubiriwa kwa muda mrefu na kutoa wito kwa mamlaka kutekeleza mapema ili kukata kiu ya wananchi wengi.

Mradi wa maji Bangulo ni miongoni mwa miradi inayotekelezwa na DAWASA inayolenga kufikisha asilimia 95 ya upatikanaji wa huduma ifikapo 2025.

# Machinga Mwanza watamani kuweka eneo Makoroboi

**Na Pendo Thomas,** MWANZA

BAADHI ya wafanyabiashara wadogo maarufu machinga jijini hapo, wameanza kurejea katika maeneo yao ya awali katikati ya jiji hilo huku wakieleza kulihitaji eneo la Makoroboi hata kwa kulipia.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Wamachinga Mkoa wa Mwanza, Mohamed Dauda, alisema ushirikishwaji zaidi unahitajika baina ya serikali na kundi hilo katika kuchagua maeneo wanayopelekwa.

Aliiomba serikali kuona haja ya kuwapatia eneo la katikati ya mji likiwamo la Makoroboi na kuwa wako tayari kulilipia ili walitumie kama wawekezaji.

"Mimi nalia na eneo la Makoroboi wanasema wanataka wampe mwekezaji kwanini wasitupe sisi machinga tuwekeze tuko tayari kulipia gharama, lakini tuwe maeneo ya mjini," alisema Dauda.

Akithibitisha ongezeko la wafanyabiashara hao katika maeneo ya mjini, Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Hassan Masala, wakati akizindua SACCOS ya SHIUMA Ilemela inayoundwa na wafanyabiashara wadogo wa wilaya hiyo ikilenga kutoa fursa ya kukuza mitaji, alisema licha ya kuboresha miundombinu ya masoko, ikifika jioni kundi hilo hurejea barabarani.

Alitoa muda wa siku 14 kwa wafanyabiashara hao kukaa na maofisa biashara wa wilaya kubaini sababu ya kuyakimbia masoko waliyotengewa ili kufikia suluhisho la kudumu.

"Hatutakubali kuacha watu waendelee kurudi nyuma wakati sisi tulishapiga hatua, tunapokaa kimya wasitujaribu wasione kwamba hatuna nguvu za kuwaondoa," alisema Masala.

Mwenyekiti wa SHIUMA Ilemela SACCOS, Mery Thomas, alisema kutokana na masharti magumu ya mikopo katika taasisi za kifedha, wameamua kuunganisha nguvu pamoja ili wafanyabiashara wadogo wapate mitaji yenye masharti nafuu.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Frank Nyabundege, akipokea zawadi ya mayai kwa Glory Mwakyao ambaye ni Ofisa wa The Great Farm Ltd, wafugaji wa kuku wa mayai, ambao ni wanufaika wa mkopo kutoka TADB, Dar es Salaam katika hafla ya kuhitimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Posta yaomba wateja kuendelea kutumia huduma zao

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SHIRIKA la Posta Tanzania (TPC), limewaomba wateja wake kuendelea kuliunga mkono kwa kupata huduma mbalimbali zikiwamo za kusafirishiwa mizigo mikubwa na barua kwa njia ya haraka (EMS) ndani na nje ya nchi.

Meneja wa Posta Mkoa wa Singida, Michael Mwanachuo, akizungumza katika mahojiano na gazeti la Nipashe kuhusu wiki ya huduma kwa wateja, alisema shirika hilo kwa sasa linatoa huduma kwa kasi na ufanisi kwa kutumia mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Mwanachuo alisema kwa kutumia TEHAMA ya Posta Kiganjani ambayo humwezesha mteja yeyote kupata huduma zao popote, mpaka sasa fursa mbalimbali kwa matokeo bora na ya uhakika zinaendelea kutolewa kwa kuzingatia kasi na ufanisi, ikilinganishwa na siku za nyuma.

"Posta kwa sasa tupo kidijitali zaidi nitoe wito kwa wananchi kuzidi kutembelea ofisi za shirika letu na kutuunga mkono kwa kujipatia huduma zetu mbalimbali za kidijitali zilizoboreshwa," alisema.

Mwanachuo alisema wakiwa kwenye maadhimisho ya wiki ya huduma kwa wateja, wafanyakazi wa shirika hilo walishiriki kufanya usafi wa mazingira na kutoa faraja kwa wagonjwa katika Hospitali ya Mkoa wa Singida.

Maadhimisho hayo ambayo kaulimbiu ni 'Posta Twenzetu Kidijitali-Haijawahi Tokea' yamekuwa na mvuto kwa wananchi ambao wameoneshwa kufurahishwa na maboresho ya huduma zinazoendelea kutolewa kwa sasa na shirika hilo.

Posta inatoa huduma za kidijitali za uwakala wa fedha, masanduku ya barua, duka mtandao, intaneti na mfumo madhubuti wa kufuatilia barua au kifurushi kilichotumwa kupitia mtandao kujua kimefikia wapi au kimepokewa na nani.

Huduma nyingine ni pamoja 'Posta Cash', Uwakala wa Bima, Huduma za uuzaji wa hisa za kampuni mbalimbali na huduma za Bodi ya Mikopo na Baraza la Mitihani na huduma kwa wananchi wanaohitaji vyeti vya kuzaliwa na kazi ya kujaza fomu na nyaraka zote ni sehemu ya majukumu ya shirika hilo.

Shamrashamra za maadhimisho zilipambwa na shughuli mbalimbali na kula keki na wateja wao wakiwamo wachezaji wa timu ya mpira wa miguu ya Singida Big Stars kama sehemu ya kurudisha shukrani.

# Polisi Muheza yasambaratisha kijiwe cha kuuza dawa za kulevya

**Na Steven William,** MUHEZA

JESHI la Polisi wilayani Muheza, mkoani Tanga, limeendelea na operesheni ya kubaini mianya ya uhalifu na kusambaratisha kijiwe cha kuuza dawa za kulevya.

Katika operesheni hiyo watuhumiwa waliokamatwa walifikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Muheza na walipatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo jela au kulipa faini.

Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai wilayani Muheza ambaye ni Kaimu Mkuu wa Polisi Wilaya, Charles Ntenga, alisema jeshi hilo lilianza operesheni hiyo katika Mtaa wa Majani Mapana ambako kulikuwa kunauzwa dawa hizo ikiwamo pombe haramu ya gongo.

Alisema kwa sasa eneo hilo limefungwa na polisi kufanya biashara za baa kutokana na uhalifu uliokuwa umekithiri ikiwamo wizi na kukaba watu.

Pia jeshi hilo lilifanya operesheni ya kusaka wahalifu katika Kijiji cha Lusanga, wilayani Muheza.

Juma Selemani na Bakari Juma, wote wakazi wa Majani Mapana wilayani hapo walilipongeza Jeshi la Polisi na Mkuu wa Upelelezi Wilaya ya Muheza kwa kufanikiwa kufanya operesheni katika maeneo hayo na kukamata wahalifu waliokuwa wakisumbua kwa matukio ya uhalifu.

Wakati huo huo, Jeshi la Polisi kitengo cha Usalama Barabarani linaendesha operesheni dhidi ya magari yote yasiyokidhi vigezo na pikipiki ili kuwahakikishia usalama watumiaji wa vyombo vya moto.

Operesheni hiyo inaendeshwa na Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Muheza, ASP Leonard Bandora, kwa kushirikiana na askari wake.



**HABARI ARUSHA**

# Wanafunzi wasimulia maajabu maeneo ya vivutio vya utalii

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

WANAFUNZI wa Shule ya Msingi Prestige ya jijini Dar es Salaam, wameeleza maajabu ya vivutio vya utalii vilivyoko nchini na kushauri watoto wa shule nyingine kupatiwa nafasi ya kutembelea hifadhi za taifa na maeneo ya vivutio vya utalii.

Wakizungumza jana na waandishi wa habari, katika Kituo cha Utalii cha Cultural Heritage jijini hapo baada ya kutembelea Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Hifadhi ya Taifa ya Tarangire na Manyara, wanafunzi hao wameeleza kuona maajabu mengi katika hifadhi hizo.

Kenzi Lewanga, Jaden James, Diana Komu, Illa Munisi na Ebeneza Charles, walisema hawakuwahi kuona kama Tanzania imejaliwa kuwa na wanyama wengi wa aina mbalimbali ikiwamo ndege na mazingira mazuri ya kuvutia.

"Kuna maajabu mengi tumeona ndani ya Bonde la Ngorongoro, Olduvai George na makundi makubwa ya tembo katika Hifadhi ya Tarangire," alisema Lewanga.

Diana Komu alisema ameshuhudia katika Hifadhi ya Manyara, simba wakipanda miti huku kukiwa na wanyama wengi.

Munisi alisema wakiwa katika Kituo cha Caltural Heritage wamepata elimu ya asili na historia na maisha ya wale wa kale, michezo ya wanyama na vitu vya asili.

"Tumepata elimu nzuri, tumejifunza vitu vingi na maswali haya huwa tunaulizwa shuleni kwenye mitihani na sasa tumejionea wenyewe," alisema.

Mwalimu wa shule hiyo, Dorice Brown, alisema shule hiyo iliyoko jijini Dar es Salaam, iliamua kuwapeleka wanafunzi kujifunza kwa vitendo vivutio vya utalii na rasilimali za taifa katika hifadhi.

"Tumetembelea hifadhi za taifa na hapa katika Kituo cha Tanzanite Cultural Heritage watoto wamejifunza historia nzuri ya binaadamu na vitu vya asili," alisema.

Wanafunzi 25 wa shule hiyo ambao wanasoma darasa la tano wameahidi kuwa mabalozi wa utalii wa Tanzania baada ya kurejea shuleni.

# Uchangiaji damu Hospitali Mount Meru bado tatizo

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

HOSPITALI ya Rufani ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru, imesema kwa sasa kiwango cha uchangiaji damu kimepungua kutokana na wachangiaji wakubwa nchini kuwa wanafunzi wa sekondari na vyuo vikuu.

Akizungumza na waandishi wa habari, Ofisa Muuguzi wa Hospitali hiyo, Ruth Kalala, alisema kutokana na uhitaji wameguswa kuzungumzia hilo baada ya kuwaona wafanyakazi wa Shirika la Posta Mkoa wa Arusha wakijitokeza kuchangia damu ili kusaidia wahitaji.

"Jamii haina mwamko wa kuchangia damu, je ni nani anayetakiwa kuchangia damu? Ni mimi na wewe ilimradi tu uwe na umri wa kuanzia miaka 18 hadi 65. Uzito kilogramu 50 kwenda juu.

"Usiwe na magonjwa sugu kama kuanguka kifafa, magonjwa ya moyo, ugonjwa wa kisukari ugonjwa wa pumu na usiwe mama mnyonyeshaji mtoto wa chini ya miezi sita au mama mwenye hali ya ujauzito," alisema.

Kabla ya kuchangia damu, Meneja wa Posta Mkoa wa Arusha, Athumani Msilikale, alisema wameshiriki katika uchangiaji huo, kwa ajili ya wagonjwa wenye uhitaji.

"Leo ni Siku ya Posta Duniani, sisi Mkoa wa Arusha tumeamua kusherehekea kwa kuchangia benki ya damu hapa Mount Meru.

"Tumeangalia ni kitu gani tunaweza kufanya kinachoenda kugusa maisha ya wananchi, uhai ni muhimu ndiyo maana tumeamua kuchangia benki ya damu."

Alisema shirika hilo limeboresha huduma zake kidigitali, kwa lengo la kuwafikia wananchi wengi na kuwahudumia kwa haraka.



Meneja wa Posta Mkoa wa Arusha, Athumani Msilikale, akikabidhi zawadi za vitu mbalimbali kwa mmoja wa wanawake waliojifungua katika Hospitali ya Rufani ya Mount Meru jana. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# DC apiga chapuo ujenzi majengo ghorofa shule msingi, sekondari

**Na Jaliwason Jasson,**
SIMANJIRO

UFINYU wa ardhi kwenye maeneo ya umma katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani, Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, umemsukuma Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Suleiman Serera, kuanza kupigia chapuo matumizi ya ujenzi wa majengo ya ghorofa katika shule za msingi na sekondari.

Dk. Serera alielekeza taasisi zote za umma kuanza kufikiria kuja na mpango huo alipokuwa akizungumza na viongozi wa mamlaka hiyo, baada ya serikali kuipatia Shule ya Sekondari Mirerani, Sh. milioni 40 za ujenzi wa madarasa mawili.

"Hizo ni hatua za kukabiliana na tatizo la ufinyu wa eneo. Pia naagiza kila taasisi, bodi ya shule kuhakikisha maeneo ya shule yanapimwa na kuwekewa mipaka/uzio ili kutatua tatizo la uvamizi wa maeneo ya shule,"alieleza.

Dk. Serera alisema viongozi hao wakijenga msingi wa ghorofa kwa kuanzia, hayo madarasa mawili na ofisi ya walimu, madarasa mengine yatakayofuata yatakuwa ya ghorofa.


"Maeneo ya ujenzi ni madogo hivi sasa, anzeni kujenga msingi wa ghorofa, kwa sababu shilingi milioni 40 haiwezi kujenga ghorofa ila nataka madarasa yanayofuata yawe ya ghorofa," alisema Dk. Serera.

Alizishauri kamati shule za msingi na bodi za shule za sekondari, kuanzisha utamaduni wa kujenga majengo ya ghorofa pindi zinapoamua kuongeza majengo mapya.

Pia alisisitiza baadhi ya shule za msingi zilizoko Mirerani, zimeanzishwa miaka mingi iliyopita, wakati huo idadi ya wanafunzi ilikuwa ndogo, lakini kwa sasa idadi ya wanafunzi imeongezeka, huku maeneo yaliyotengwa yakibakia yale yale.

Diwani wa Mirerani, Salome Mnyawi, akizungumza katika kikao kazi hicho, alisema agizo hilo la Mkuu wa Wilaya, linapaswa kutekelezwa kwani litakuwa na maendeleo na litachukua nafasi ndogo ya ujenzi wa madarasa.

Naye Diwani wa Endiamtu, Lucas Zacharia, alisema majengo ya ghorofa ndiyo suluhisho la ujenzi wa madarasa ya sekondari hiyo ni suluhu ya uhaba wa eneo.





## Shirika lajitosa kulisha chakula wanafunzi shule za msingi 53

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Save the Children limejitosa kugharamia chakula kwa wanafunzi zaidi ya 28,000 kutoka shule za msingi 53 katika wilaya za Handeni na Mkinga ambazo zinatishiwa na uhaba wa chakula.

Shirika hilo, limekabidhi miongozo ya utoaji wa chakula katika shule za wilaya hizo kupitia Mpango wa Taifa wa Ugawaji wa Chakula.

Kwa mujibu wa Mratibu wa Uhakika wa Chakula wa Mkoa wa Tanga, kutoka Shirika la Save the Children, Anania Yusto, miongozo inakwenda kusimamia na kuratibu namna gani viongozi wa shule watakavyolisha shule zao.

"Katika wilaya hizo mbili zilionekana kukabiliwa na uhaba wa chakula katika tathmini ya lishe nchini, ndiyo maana tumekuja na mpango maalumu wa kulinda lishe zao," alisema.

Alisema Shirika la Save the Children, kupitia mradi wao wa uhakika wa chakula, wanashiriliana na Shirika la World Vision, kuhakikisha miongozo hiyo inadhibitiwa.

"Lakini tunaratibu mpango mzima wa hii miongozo na kuendelea kusimamia matumizi yake huko shuleni. Kwa hiyo hii miongozo itakwenda kuhakikisha shule hizi 53 zinazopata chakula kupitia mradi wetu, unaendelea kupata miongozo na rejea," alisema.

Aidha, alisisitiza kuwa mradi huo pia unaweka wigo mpana katika utendaji wake, kwa kuwa wanakabiliana na majanga mbalimbali, ambayo yametokana na mvua iliyosababisha ukosefu wa chakula.

"Na kwa tukio hilo, tutahakikisha tunaendelea kuratibu hali halisi ya vijana wetu walioko shuleni kupitia miongozo itakayotolewa huko mbele za upimaji wa hali ya lishe itakayotolewa shuleni," alisema.

Hata hivyo, baadhi ya walimu waliokabidhiwa miongozo hiyo, akiwamo Grace Mbanga, ambaye ni Ofisa Elimu Sayansi Kimu, Halmashauri ya Wilaya ya Handeni, alisema mradi huo umesaidia kuondoka utoro kwa wanafunzi ikiwa ni pamoja na kupunguza kwa kiasi kikubwa mimba za utotoni.

"Idadi ya watoto imeongezeka kwa kiasi kikubwa shuleni na hata utoro hakuna kwa kuwa inapofika muda wa kwenda kula watoto hawaendi majumbani wanabaki shuleni, huu mradi umetusaidia sana sisi walimu na hata watoto wetu," alisema Grace.

Mwalimu, Elibariki Samballu, alisema mpango huo kabambe umekuwa mzuri kutokana na matokeo mazuri kwa sababu wameweza kuchochea kiwango cha mahudhurio ya wanafunzi.

# Kanzi data ya sensa kuwajengea uwezo vijana nchini kujiajiri

**Na Oscar Assenga,** TANGA

KAMISAA wa Sensa ya Watu na Makazi, Anne Makanda, amesema serikali imepanga kutumia kanzi data ya sensa ya mwaka huu, kuwajengea uwezo vijana kujiajiri katika sekta isiyo rasmi ili kupunguza msururu wa wanaosaka ajira serikalini.

Aliyasema hayo juzi jijini Tanga, alipokutana na Kamati ya Sensa ya Mkoa huo na kupokea taarifa ya utekelezaji wa kazi hiyo.

"Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, ameweka nguvu kubwa kwa wafanyabiashara wadogo, maarufu wamachinga na anasubiri baada ya kutangazwa matokeo ya sensa, atafanya mambo yake ambayo ameyapanga.

"Hivi mnajua machinga ndiyo sekta ambayo inachukua watu wengi sana na nafasi yao ni kubwa sana duniani, na imekuwa na mchango mkubwa wa maendeleo?" Alihoji Makinda.

Kwa mujibu wa Makinda, Tume ya Taifa ya Takwimu (NBS), kwa sasa inakamilisha mchakato wa tathmini ya jumla kuhusu sensa ya mwaka huu ilivyofanyika na wataikabidhi kwa Rais Samia Suluhu Hassan, kabla ya mwisho wa Oktoba.

Hata hivyo, Makinda, alisema hivi sasa serikali kupitia Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na ya Visiwani Zanzibar (OCGS), wanaandaa mpango wa mafunzo kuhusu matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi, baada ya kutangazwa.

Alisema NBS na OCGS wanaandaa mpango huo na takwimu zilizopatikana itabidi zifanye kazi, baada ya Rais kutangaza kutakuwa na programu za kufundisha wananchi maana ya takwimu hizo.

Awali, Mratibu wa Sensa, Mkoa wa Tanga, Tony Mwanjota, alisema wamefanikiwa kuhesabu kaya za Watanzania kwa asilimia 95, ikiwamo kuyafikia majengo yote, kutoa elimu na hamasa kwa wananchi.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba, alisema mkoa huo umeendelea kutekeleza agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la kutenga maeneo kwa ajili ya kilimo.



Mwakilishi wa Taasisi ya Lady Fatemah Trust, Taub Sharrif (kulia), akimwonesha Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omary Mgumba (katikati), mabegi na madaftari waliyotoa kwa ajili ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Pongwe yenye watoto wenye mahitaji maalumu juzi. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Hashim Mgandilwa, taasisi hiyo ilitoa msaada wa Sh. milioni 220 kwa ajili ya ukarabati wa shule hiyo. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA.**

# TNBC yadokezwa sababu kushamiri biashara magendo

**Na Mary Mosha,** MOSHI

BARAZA la Biashara Mkoa wa Kilimanjaro (TNBC), limeelezwa kushamiri kwa biashara ya magendo katika wilaya za Rombo, Siha na Same, kunatokana na jamii kugeuza magendo kuwa ni sehemu ya majukumu yao ya kila siku ya kutafuta mkate na kukuza kipato chao kiuchumi.

Akieleza hali halisi katika mipaka ya Holili, Tarakea na Siha (Kamwanga), Ofisa Elimu kwa Walipa Kodi wa Mamlaka ya Mapato Mkoa wa Kilimanjaro, Odupoi Papaa, alisema msukumo wa Watanzania kufanya hivyo unachangiwa zaidi na nafuu ya bei za bidhaa kutoka nchi jirani ya Kenya.

"Kuna mambo kama vile tofauti ya bei kwa baadhi ya bidhaa, kati ya nchi za Kenya na Tanzania na kukosekana kwa uzalendo kwa baadhi ya wafanyabiashara.

"Haya ni mambo yanayochochea watu wafanye biashara ya magendo badala ya kufanya biashara halali kwa kulipa kodi ya forodha mipakani."

Mkoa wa Kilimanjaro, unatajwa kuwa na njia za panya zaidi ya 300 zilizoko katika eneo la mpakani wilaya za Siha, Same na Rombo.

Kutokana na kukithiri kwa magendo, TRA imesema bado inaendelea kufanya doria za mara kwa mara ili kuwabaini wanaofanya hivyo, ikishirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurudn Babu, akizungumza katika mkutano huo, aliwaagiza wakuu wa wilaya kudhibiti magendo katika maeneo yao na kumpatia taarifa ya utekelezaji wa agizo lake.

"Pia niwasihi wafanyabiashara, kwamba ni vizuri wafanyabiashara wetu wakajiepusha na biashara za magendo wakati wanapofanya shughuli zao za kibiashara katika maeneo yao ili wao wenyewe pamoja jamii inayowazunguka wasiathirike na athari zitokanazo na biashara hiyo," alisema.

Amran Kangesa, ambaye ni mmoja wa wafanyabiashara alisema biashara ya magendo ikiachwa iendelee ina madhara ya kiafya kutokana na wafanyabiashara kuingiza bidhaa zilizopita muda ambazo zinaweza kuwasababishia walaji magonjwa mbalimbali ikiwamo saratani.

Kwa upande wake, Faustina Ndossi, waliwaomba maofisa wa TRA, kuendelea kutoa elimu ya mara kwa mara kwa wafanyabiashara ili kuhakikisha biashara hiyo ya magendo inakomeshwa.

Nipashe
# TESA
Jumanne Oktoba 11, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI




**Ni ukweli sasa kuwa kusoma, kufaulu sayansi inawezekana**




FAO inavyokutengenezea kijana mazingira kukopesheka, kujiajiri




**Mtu anapoenda hospitali kwa homa, malaria apime afya akili**

ELIMU

**NA CHRISTINA HAULE, DODOMA**

# Athari tabianchi si mafuriko, vimbunga pekee hata unyanyasaji kijinsia umo pia

• Huongeza uhaba wa chakula, maji, nishati



Uhaba wa maji unaotokana na ukame unalazimisha watoto kuyafuata umbali mchana hata usiku na wakati mwingine kunyanyaswa, kutumikishwa na kudhalilishwa utu wao. **PICHA: MTANDAO**

MABADILIKO ya tabianchi na hali mbaya ya hewa inayoleta njaa, uhaba maji na kuongeza umaskini kuanzia chakula, nishati na mahitaji ya kila siku, yanatajwa kuwa ni moja ya sababu za kuchangia kuendelea kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa jamii licha ya kuwapo makatazo na maelekezo yanayotolewa mara kwa mara na serikali na asasi za kiraia.

Mratibu wa mradi wa kuleta mabadiliko kwa wanawake vijijini (RWCC), Catherine Kasimbazi, anasema hayo, wakati wa mafunzo kwa wanahabari kuhusu ukatili wa kijinsia, akirejea kazi za utafiti mbalimbali walizofanya kwenye mikoa inayotekeleza mradi huo, akibainisha kuwapo kwa changamoto zilizoko katika mikoa mingi ya Tanzania zinazoashiria ukatili wa kijinsia unaohusishwa na mabadiliko ya tabianchi.

"Ukosefu wa mvua umeleta njaa, unaumiza mifugo na yote yanasababisha kuwapo kwa biashara ya ngono miongoni mwa wanawake ili waweze kupata fedha za kumudu maisha yao na kusaidia familia zao. Siyo lazima kujipanga barabarani kusaka wateja, lakini kuna namna ya kuuza mwili ili kupata mahitaji."

Anaitaja changamoto nyingine inayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi kwa wa kingono unaosababishwa na kuibuka kwa kasi masuala ya ndoa na mimba za utotoni kufuatia wazazi kuchukua hatua za kuwaozesha mabinti wakiwa katika umri mdogo ili wapate pesa za kujikimu, mifugo na mali nyingine ili waishi.

Catherine anaitaja changamoto nyingine kuwa ni tatizo la maji hasa maeneo yasiyo mijini na miji midogo linalosababisha kutokea kwa vitendo vya ukatili wa kingono kwa wanawake na watoto baada ya kutembea umbali mrefu kutafuta maji na pengine kukesha mtoni au visimani hata mabondeni wakitafuta huduma hiyo.

Anafafanua kuwa yote hayo yanafikia hatua ya kurubuniwa hasa na wanaume wenye vyombo vya usafiri, wenye nguvu za kusaka na kuwaletea maji na matokeo yake wanawake na watoto wanabakwa, yapo matukio ya kulawitiwa sambamba na kuwapo kwa migogoro ndani ya ndoa na pengine nyingine kuvunjika.

Aidha, wasichana kupata ujauzito na kukatishwa masomo

INAENDELEA UK.18

UCHAMBUZI

NA JOSEPH MWENDAPOLE

# Mitaala mipya ikiiva kuwa mwarobaini mafanikio kielimu

• Wasomi wapikwa pande mbili darasani, ofisini




Vijana wakiwa kazini kwenye moja ya viwanda. **PICHA: MTANDAO**

ILI elimu wanayopata Watanzania iwe ya kuwapa maarifa zaidi badala ya nadharia, mchakato wa kufumua na kuunda upya mitaala unaendelea, ili kuisuka na kufanikisha kupika wasomi au wahitimu walioiva kujitegemea.

Nyuma ya pazia inaelezwa kuwa uzoefu unaonyesha kuwa wahitimu wengi hawamudu kujiajiri wanapomaliza masomo ya vyuo vikuu pengine kutokana na elimu wanayopata, iko kinadharia zaidi.

Yapo maelezo kuwa vijana kwa maelfu wanazunguka mijini na kwenye majiji kutafuta ajira wanapomaliza elimu ya sekondari, vyuo vikuu na vya kati vya ufundi na sababu inayoelezwa ni kukosa ujuzi wa kujiajiri, lakini hawaajiriki.

Wengi wamekuwa wakiendelea kuishi na wazazi na walezi hata baada ya kumaliza elimu ya juu na wakiulizwa jibu wanalotoa ni jepesi kwamba hakuna ajira.

Lakini, wakati vijana wakilalamikia ukosefu wa ajira baadhi ya waajiri nao wanalalamikia wahitimu hao kwamba wanakosa ujuzi unaostahili kwa maana kwamba wanahitimu wakiwa hawajaiva kwenye fani wanazosomea.

Ni kutokana na malalamiko hayo, Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), hivi karibuni kimeanzisha programu ya uanagenzi ambayo mwanafunzi anasoma chuoni hapo huku akiendelea kufanya kazi kwa mwajiri wake.

> Tunataka kuandaa watu wenye uwezo wa kufungua macho na kuona fursa mbalimbali na kuzitumia isavyo kwenye mazingira yao badala ya kutegemea kalamu na karatasi peke yake.

Mkuu wa Programu ya Uanagenzi, Dk. Mariam Tambwe, anasema hayo katika mahojiano na Nipashe jijini na kuongeza kuwa itamwezesha mwanafunzi kusoma mafunzo yake nusu chuoni nusu kwa mwajiri na kwamba lengo ni kumpatia ujuzi unaohitajika kwenye soko la ajira.

Aidha, CBE ilianzisha kozi hizo baada ya waajiri wengi kulalamika kwamba vyuo vinazalisha wahitimu ambao hawajaiva vya kutosha hivyo kulazimika kuwapa mafunzo ya muda mrefu wanapowaajiri kwenye kampuni zao.

Dokta Mariam anasema malalamiko kama hayo yanasikika karibu dunia nzima na kwamba wahitimu wengi kwa sasa hawakidhi mahitaji ya soko la ajira kutokana na kukosekana umahiri wa hali ya juu kwenye fani mbalimbali wanazosomea.

"Wanalalamika kwamba wahitimu wengi wanaozalishwa vyuoni ni tofauti na mahitaji ya soko ndiyo sababu CBE sasa tumeamua kujibu changamoto hiyo kupitia program ya uanagenzi ambayo mwanafunzi atasoma nusu darasani na nusu kwa mwajiri," anasema Dk. Mariam.

Mwaka jana Rais Samia Suluhu Hassan aliagiza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kufumua mfumo wa elimu na mitaala ili kuandaa itakayokuwa na majibu sahihi ya elimu.

Agizo hilo linakuja baada ya mfumo wa sasa na mitaala kuonekana havikidhi mahitaji ya wakati kwani ni vya zamani na huenda kuna mambo ya kuongeza ili kwenda na wakati.

Tangu litolewe agizo la Rais Samia, kikosi kazi cha wizara hiyo kilianza na kinaendelea na mchakato wa kubadili mfumo wa elimu na kuandaa mitaala inayolenga kutatua changamoto za nyakati za sasa.

Kamishna wa Elimu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Lyabwene Mutahabwa, anasema mitaala mipya itawaandaa wanafunzi kusimama wenyewe kujitegemea baada ya kumaliza elimu.

"Tunataka kuandaa watu wenye uwezo wa kufungua macho na kuona fursa mbalimbali na kuzitumia isavyo kwenye mazingira yao badala ya kutegemea kalamu na karatasi peke yake," anasema.

"Kwa hiyo kama ni ujuzi wa ushonaji kutengeneza sabuni, kusindika, kufuma, ususi suka, uashi na uchomeleaji kwa hiyo tangu mheshimiwa Rais atoe agizo tunaendelea na mchakato na lengo ifikapo Januari 2024 vianze kutumika," anasema Mutahabwa.

Anasema kikosi kazi kilichoundwa kimepokea maoni ya wadau mbalimbali na mitaala hiyo itakuwa na sura tatu ya kwanza itakuwa ni maarifa, nyingine maadili na ya tatu ujuzi.

"Viongozi wetu wa dini wamesisitiza sana suala la maadili. Wamesema yapewe msisitizo kutokana na mmomonyoko wa maadili kwa sababu hata ndugu hawaaminiki. Mitaala yetu mipya itazingatia elimu ya kichwani, ya moyo na ya ujuzi wa kazi za mikono.

Kichwa ni maarifa, moyoni maadili na mikono ni ujuzi wa shughuli mbalimbali za kiufundi na stadi," anasema Kamishna wa Elimu na kuongeza: "Hayo yote tuyazingatie katika kutoa elimu tuwe na maarifa na maadili, huruma na kusaidia wengine na tusiwe na dharau, wawapende wenzao wa ngazi zote bila ubaguzi hapo tutakuwa na maadili yetu Watanzania."

Anasema serikali inakusudia kutengeneza taifa lisilo na mafisadi, lililosheheni raia ambao wako tayari kuifia Tanzania. Aidha inatamani sana wanafunzi wanaosoma katika vyuo vikuu, vya kati na ufundi pamoja na sekondari, shule za msingi na sekondari watoke wakiwa na maadili na uzalendo wa kuipenda na kuipigania nchi yao kwa dhati na siyo kwa unafiki, anasema Kamishna wa Elimu.

Anasema wazazi wanajukumu la kuhakikisha wanawalea na kuwafundisha maadili watoto wao badala ya kuwaachia jukumu hilo walimu pekee.

Katika mwendelezo wa kukusanya maoni kutoka kwa wadau mbalimbali, hivi karibuni Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilikutana na Kamati ya kitaifa ya uboreshaji wa mitaala inayoongozwa na Profesa Makenya Maboko jijini Dodoma.

Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi TRA, Richard Kayombo, akawasilisha mada kuhusu umuhimu wa kuingiza masuala ya elimu ya kodi katika mitaala ya msingi na sekondari.

"TRA inaamini kwamba kama kungekuwa na somo la kodi linalosomwa na wanafunzi katika shule za msingi na sekondari tungeweza kuwa na raia wanaoelewa kodi," anasema Kayombo.

Aidha, anaeleza kuwa TRA inakusanya kodi kutoka kwa walipa kodi ambao hawana ufahamu na hawajui umuhimu wa kulipa kodi hivyo, kama wanafunzi watafundishwa somo la kodi shuleni, itafanikisha kupata Watanzania wenye uelewa mpana kuhusu kodi na kujenga utamaduni wa kulipa kodi na kuchangia mapato ya serikali kwa hiari.

UCHAMBUZI
**NA MWANDISHI WETU**

# Mtu anapoenda hospitali kwa homa, malaria apime afya akili

DUNIA imeadhimisha Siku ya Afya ya Akili kwa mwaka huu inayosukumwa na kaulimbiu ya kuhakikisha afya ya akili na ustawi kwa wote inakuwa kipaumbele kimataifa, lakini ikianza na kila mmoja kuzingatia na kuipa umuhimu afya ya akili yake.

Afya ya akili inafafanuliwa na wataalamu kuwa ni ukamilifu wa michakato ya kiakili, kimwili na kijamii na ndiyo inayoamua namna unavyofikiria, kuhisi na kutenda na ndiyo inayokusaidia kuamua mambo na namna ya kuyashughulikia matatizo kama kufadhaika, mihemko, hofu, hasira na mahusiano baina yako na wengine.

Iwapo hutatibu na ukazidiwa na matatizo ya akili kama kuwa na woga mno, kuogopa kurogwa, kusononeka kutokana na kufanyiwa matendo ya udhalilishaji, mfadhaiko, sonona na msongo wa mawazo unaweza kupata magonjwa ya akili.

Aidha, magonjwa hayo ni matatizo kwenye ubongo yanayokufanya kuwa na hisia, fikira, maneno na matendo tofauti na wengine na hata kushindwa kukabiliana na changamoto za matatizo yanayokukabili.



Kuwatesa kwa kuwafunga minyororo wenye matatizo ya afya ya akili siyo tiba, wanatakiwa kupelekwa hospitali kutibiwa. **PICHA: MTANDAO**

Mtaalamu wa Afya ya Akili na Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Dk. Isaac Lema, anasema hayo wakati wa mkutano na wahariri wa vyombo mbalimbali kuzungumzia kilele cha siku ya afya ya akili duniani ambacho ni kila mwaka Oktoba 10.

Anasema leo inashangaza watu wengi wakiumwa maradhi ya mwili kama moyo, homa, tumbo na kichwa wanakimbilia hospitalini lakini wakiwa na shida ya matatizo ya akili hawaendi hospitalini ni kwanini?

Mtaalamu wa afya ya akili anaeleza kuwa ni asilimia 12 pekee ya Watanzania wametibiwa magonjwa ya akili lakini wengine hawajajichunguza licha ya magonjwa kuwa zaidi ya 280, na hata wao kufahamu kuwa wana tatizo linalowasumbua.

"Hata hivyo ni vyema kukumbuka kuwa unapokuwa na matatizo ya afya ya akili haimaanishi kuwa una shida ya akili na cha muhimu ni kwenda hospitali kuyatibu.

"Ukiumwa miguu, tumbo au kichwa unakimbilia hospitalini, unapopata matatizo ya akili unayapeleka wapi? Vitu kama hisia za huzuni, sonona, uchungu mkali na maumivu ya kuachwa na mwenza au kutelekezwa, kudharauliwa na kunyanyaswa kijinsia yanabaki moyoni. Utaishi nayo mpaka lini na yatakuumiza mpaka wapi? Ni wakati wa kuchukua hatua na kuyapeleka hospitali," anakumbusha .

> " Ukiambiwa una matatizo ya afya ya akili haimaanishi kuwa huna akili, zipo. Tuache kuangalia kuwa wenye matatizo hayo ni wale wanaokota makopo. Hapana.

Anasisitiza ulazima wa kufunguka na kuwashirikisha wengine hasa wataalamu wa afya, wanasihi na maofisa wa ustawi wa jamii matatizo ya afya ya akili ili kukabiliana nayo.

Matatizo hayo huanzia kwenye miaka 14 hadi 29 kwenye umri balehe na kwamba kiasi umri unavyoongezeka matatizo ya akili pia huongezeka kama kupoteza kumbukumbu, kuwa na furaha zaidi, wasiwasi kupindukia na ukali au hata kufadhaika.

"Mfadhaiko ni matatizo ya afya ya akili mfano ukiwa barabarani unaweza kuhofia foleni ukaanza kuzungumza mwenyewe ukihofu mafuta yataisha, au huyu ananibana atanigonga na hofu nyingine lakini ukifika salama umepona."

Anasema na kuongeza kuwa mfadhaiko unapozidi huwa tatizo kubwa lakini ukidhibitiwa hakuna cha kuogopa.

Dokta Lema anasisitiza kuwa magonjwa mengi ya akili duniani yanaanza katika umri wa utotoni na hali huwa mbaya zaidi kwenye umri wa kupevuka ambako watu hukabiliwa na mihemko na mashinikizo mbalimbali na pasi kutibiwa inaweza kuwa na athari mbaya.

Anasema miaka 14 hadi miaka 29 ndiko kwenye changamoto kubwa na kwamba bila kuripoti na kubainishwa pamoja na kutibiwa yanaweza kuwa na athari mbaya kama ambavyo zinaanza kuonekana sasa.

Anataja matatizo ya akili husababishwa na msongo wa mawazo kama kukosa pesa, majukumu kazini, uhusiano na wakati mwingine matumizi ya vilevi vikali kupundukia, kukosa usingizi na magonjwa kama malaria.

Anasema kila mtu ana uwezo wa kukabiliana na matatizo ya afya ya akili lakini mara nyingi wengi hukata tamaa hivyo kupata magonjwa.

Anakumbusha kuwa matatizo ya afya hiyo yanaweza kutokana na uwezo wa mtu kuchakata taarifa kwani zipo zinazoleta taharuki, kwa mfano ukisikia kuhusu magonjwa hatarishi unaweza kushindwa kuhimili.

Hata hivyo ili kupona Dk. Lema anasema ni lazima kujipa kinga akitoa mfano kwa wanasiasa wakati wa uchaguzi wanakumbushwa kuwa hata kama utashindwa ufahamu kuwa unaposhiriki na kuangushwa kuna maisha baada ya uchaguzi.

### ATHARI KWA JAMII

Dokta Lema anasema athari za afya duni ya akili ni pamoja na kushambulia na kuua watu ovyo mfano kupiga na kuua wezi, kutishia wengine ukianza unanijua mimi ni nani? Kugomba na kurushia matusi maneno makali kwenye daladala, watu kuua wenza watoto, wapenzi kwa kisingizio cha wivu na hata kutamba na kutishia wengine kuwa hapa patachimbika iwapo jambo litatokea.

### ANASISITIZA TIBA

Kuwaona wataalamu hospitalini na kwamba ni lazima kupima mara mbili au tatu kila mwaka kwa kuripoti matatizo ya afya ya akili kama sonona, hasira kali, hofu, wasiwasi wa kurogwa au kupigwa na mapepo kwa wahudumu wa afya ili wakusaidie na kukutibu.

Anashauri kulala angalau saa nane mfululizo au pungufu kuwa saa sita kila siku, kufanya mazoezi mara kwa mara, kupumzika, kuacha pombe na vilevi kama sigara, dawa za kulevya na mambo hatarishi.

### VIPI NGUVU ZA KIUME?

Mbobezi katika fani ya afya ya akili, Dk. Samwel Lindikoki, anayefanya kazi katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, anakumbusha kuwa matatizo ya afya ya akili huanzia utotoni kama kuwa na watoto watundu, wasiotii, watukutu, wanaokula magodoro na hata wenye usonji na kuwataka wazazi na walezi kuwachunguza na kuwapeleka hospitalini kuna tiba.

Akizungumzia suala la jamii kuwa na hofu kubwa ya ukosefu wa nguvu za kiume anasema ni tatizo la afya ya akili na kwamba eneo hilo lina magonjwa zaidi ya 20.

"Leo watu wanaodhani hawana nguvu hizo, wanasaka dawa, wapo wanaotaka kuongeza ukubwa wa maumbile. Eneo hili lina magonjwa mengi kama kuangalia picha za ngono mitandaoni ni matatizo pia, kubaka na kunajisi watoto..."

Mtaalamu Lindikoki anataja pia watu kuamini uchawi na kurogwa kuwa ni tatizo na kusababisha matatizo kwenye afya ya akili na ndicho chanzo cha kuua wengine kuwa ni wachawi, kuzua mitafaruko kuwa watu wanaoamini nguvu za giza na kuongeza matatizo kwenye jamii inayoogopa ushirikina.

### HUJAKOSA AKILI

Mtaalamu wa afya ya akili kutoka Wizara ya Afya, Dk. Erasmus Mndema wa Afya ya Akili Wizara ya Afya, anakumbusha kuwa na matatizo ya akili si kukosa akili na kwamba wapo waliopata tuzo ya Nobel kwa kazi kuwa walizofanya licha ya kuwa maradhi ya akili.

ELIMU

NA GERALD KITABU, RUFIJI

# FAO inavyokutengenezea kijana mazingira kukopesheka, kujiajiri

• Uliyehitimu chuo kikuu, sekondari umo



Vijana wakulima wakiwa kazini wilayani Rufiji wakifanyakazi chini ya mpango wa kilimo cha kibiashara unaofanywa na FAO. **PICHA: GERALD KITABU**

VIJANA wa mikoa ya Pwani, Dodoma, Singida na Arusha, ni wanufaika wa mpango wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa-FAO la kuwaatamia vijana likiwapa elimu na maarifa ili wajianzishie miradi, wakope na wajiondoe kwenye umaskini, kupitia kilimo biashara.

FAO inawatengenezea mazingira ya kukopesheka na kujiajiri kupitia mpango wa kuatamia vijana 'Youth Incubation Program', unaolenga waliomaliza kidato cha nne, cha sita na vyuo vikuu.

Wasomi wa vyuo vikuu na wahitimu wa kidato cha nne na sita wako kazini na shughuli inaendelea katika Wilaya za Rufiji, Kibiti na Mkuranga mkoani Pwani kwenye kilimo cha mboga, kuna wengine Dodoma, Singida na Arusha ambako vijana wanajishughulisha na viazi pamoja na maharage lishe.

Mkoani Pwani vijana wanufaika wanajishughulisha na kilimo biashara katika kijiji cha Mkongo kilichoko Rufiji, wengine wako Kibiti na Kijiji cha Sunguvini wilayani Mkuranga.

Walioko Rufiji, wanalima mboga kama pilipili mwendokasi, bamia, nyanya na matango wanaeleza katika mazungumzo na Nipashe.

Kaimu Ofisa Kilimo, Mifugo na Uvuvi Wilaya ya Rufiji, (DALFO) Hussein Harry anasema: “Tunawatambua na kuwathamini vijana wanaojishughulisha na kilimo biashara walioko AGL Farm Ltd na tuna mpango wa kuwakopesha kutoka kwenye ile asilimia 10 iliyotengwa kwa ajili ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.”

> “Tunajivunia mpango wa FAO wa kuatamia vijana kuwagusa hapa kwenye wilaya yetu, tutahakikisha vijana hawa wanapata mikopo kuendeleza kilimo biashara ili wakawe mfano bora katika maeneo walikotoka.

“Tunajivunia mpango wa FAO wa kuatamia vijana kuwagusa hapa kwenye wilaya yetu, tutahakikisha vijana hawa wanapata mikopo kuendeleza kilimo biashara ili wakawe mfano bora katika maeneo walikotoka,” anasema.

Anaeleza kuwa wapo vijana watano kutoka kampuni ya AGL Farm Ltd iliyoko shamba la Mkongo ambao wamewasilisha maombi, na kwamba wanawafahamu na wanafanya vizuri. Wanategemea kuwa vijana hao wanaweza kupata mkopo.

Akizungumzia mpango wa FAO, anasema umewaondoa vijana mitaani na kuwaelekeza kwenye kuwajenga, kuwapa elimu, ujuzi na mbinu za kilimo biashara cha kisasa na kufanikisha waweze kukopesheka ili kufikia malengo yao.

Vijana hao kutoka kata mbalimbali za wilaya hiyo wenye elimu ya kidato cha nne wanajifunza mbinu za kilimo bora shambani hapo kwa udhamini wa FAO kwa muda wa miezi miwili na wakiwa mashambani wanafanya kazi kwa vitendo kutoka kwa wenzao waliopata mafunzo nchini Israel.

Mkufunzi wa vijana hao ni muhitimu wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), Dickson Alex, anayesema aliamua kuingia kwenye ujasiriamali ili kubadilisha fikra za vijana wenzake wasomi kuwa kilimo siyo dhambi wala umaskini bali ni utajiri.

Anasema ana elimu bora na sifa za kuajiriwa lakini akaamua kuwekeza nguvu kwenye kilimo biashara akijua ipo siku kitamtoa kimaisha.

“Hii ni awamu ya tatu napokea vijana wanaotaka kuwa kama mimi kutoka maeneo mbalimbali, kwa sasa nina jumla ya vijana nane, watano ni wa kudumu na watatu ni wa muda. Nafanya nao kazi zote kwa vitendo au kwa mikono kwa muda wa miezi miwili. Nahamisha elimu na ujuzi niliyopata SUA na Israeli nawapa vijana ili kuwaonyesha na kuwaaminisha wengine kuhusu kilimo biashara,” anasema.

Dickson anasema kwa sasa wameshapata soko kubwa la bidhaa zao katika bwawa la kuzalisha umeme la Mwalimu Nyerere na hivi punde kuna soko jingine kubwa kutoka kwa watalii wanaotembelea hifadhi ya wanyama ya pori la Mwalimu Julius Nyerere -Selous.

“Kuna soko kubwa la mboga hapa kwetu. Bwawa la kuzalisha umeme la Mwalimu Nyerere peke yake linahitaji tani tano kwa wiki. Hii imetufanya tuongeze eneo la uzalishaji kutoka ekari 10 mpaka 20 ili kukidhi mahitaji hayo,” anasema Dickson.

Anafafanua kuwa walikuja kukagua mazao yanayotoka shambani kwetu, jinsi tunapambana kuhakikisha hatuwaangushi kwa sababu tunalima kwa kuzingatia ubora wanaotaka.

Nao baadhi ya wanufaika wa mpango huo wa FAO waliopo katika mradi huo, Juma Hemed na Salma Hussein, wanaelezea kufurahishwa na mpango huo na kuuita ni mkombozi kwa vijana hao ambao baada ya kumaliza elimu ya sekondari walikuwa hawana mbele wala nyuma.

“Mpango huu ni bora zaidi kuwahi kutokea katika maisha yetu na tunaahidi kujifunza kwa vitendo kadri tuwezavyo ili tukitoka hapa tukaanzishe mashamba yetu na tujikite katika kilimo biashara,” anasema Hemed.

“Kwanza tunaishukuru serikali Wilaya ya Rufiji kwa kutuleta hapa, tunawashukuru FAO na mkufunzi wetu kwa ushirikiano wanaotupa hapa. Tumeshaomba mkopo tunasubiria majibu tukifanikiwa tutapanua mradi wetu ili kulikamata soko lote la Bwawa la Mwalimu Nyerere,” anasema Salma.

Ofisa Mradi Mnyororo ya Thamani na Ajira kwa vijana kutoka FAO, Ajuaye Sigalla, anasema mpango huu una lengo la kuwavutia na kuwahamasisha vijana waingie katika uzalishaji kupitia kilimo biashara.

“Tunachokifanya ni kutambua kampuni zinazoongozwa na vijana za uzalishaji, au uchakataji au masoko au zinazofanya vyote. Huku ndiko hawa vijana wanakwenda kufanya kazi kwa vitendo,” anasema.

Anaongeza kuwa FAO haiwapi fedha vijana bali inatoa msaada kidogo kama vifaa na mahitaji mengine ili kuwezesha kazi ya kujifunza kwa vitendo iendelee.

“Kwa kufanya hivyo tunawasaidia vijana viongozi kuwapunguzia gharama za uendeshaji lakini kwa wapya wanapata fursa ya kujifunza kwa vitendo na kuongeza elimu na ujuzi. Wakitoka hapo si kama walivyokuja, wanakuwa ni watu wenye utaalamu. Tunafanya hivyo tukiwa na mategemeo makubwa kuwa wataenda kuendeleza kilimo biashara na kubadilisha maisha yao lakini pia kusambaza ualimu na ujuzi huo katika jamii walikotoka,” anasema.

Mpango huu wa FAO wa Youth Incubation Program katika mkoa wa Pwani pia unaendelea katika mikoa ya Dodoma, Singida na Arusha ambako vijana wanajishughulisha na viazi pamoja na maharagwe lishe wako kwenye uzalishaji.

TEKNOLOJIA

**NA MWANDISHI WETU**

# Ubunifu wa BOT waibua mageuzi ndani huduma za benki kongwe

## • TCB; tumekuja na yetu kipekee • Wizara Fedha; mageuzi ya mfano

TAKWIMU rasmi za Benki Kuu ya Tanzania (BOT), inatamka takribani miaka 16 tangu kuanza kupatikana kwa huduma za kibenki nchini kwa njia ya mtandao wa intaneti, pia malipo kufanyika kupitia mtandao huo.

Taarifa ya Benki Kuu inaonyesha huduma hizo zilianza kwa miamala chini ya 200,000, ikiwa na thamani ndogo ya fedha kwa mwaka mzima.

Huduma hiyo ya kidigitali, ni ya kielektroniki ambayo benki zinatumia kuwawezesha wateja kuhudumiwa kwa mtandao na ndani ya mageuzi hayo, ndani yake kati ya wanaoajumuisha ni Benki ya Biashara Tanzania (TCB), ambayo ikaamua kuwekeza nguvu zake.

Kushiriki zaidi kwa TCB katika maendeleo yake na uwekezaji unaofanywa na wadau wengine, pamoja na kusimamiwa kikamilifu na BoT, kumefanya huduma za kibenki kwa mtandao kuwa na matokeo chanya zaidi na yenye manufaa kibiashara na kiuchumi.

Takwimu rasmi za BoT zinaonyesha mchango wa intaneti kwenye huduma za benki, kunasaidia kuenea huduma jumuishi za kifedha na mchango wake katika kuifanya Tanzania kupunguza matumizi ya fedha taslimu kwenye uchumi.

Kwa sasa, huduma hii ya kidigitali inatajwa kuhusisha wastani wa miamala milioni moja kwa mwezi, ikiwa na thamani ya Sh. bilioni 10, ikilinganishwa na miamala 164,470 ya miaka 16 iliyopita, ilipoanzishwa.

Katika taarifa ya hivi karibuni, Benki Kuu inasema idadi ya miamala ya huduma za kibenki kwa mtandao iliongezeka hadi 969,126 mwezi Desemba mwaka jana, ikiwa tangu mwaka 2021 na thamani ya shughuli hizo ikawa ni Sh. trilioni 11.26.

"Nchini Tanzania, fedha taslimu ndio njia maarufu ya kufanya malipo. Hata hivyo, kuna njia nyingine mbalimbali za kufanya malipo kama vile hundi, malipo ya kielektroniki, malipo ya kadi, malipo kwa njia ya mtandao na malipo kwa njia ya simu," taarifa ya BoT inadokeza.

Hivi karibuni Benki ya Biashara ilifanyia maboresho makubwa katika mfumo wake wa intaneti za huduma za kibenki, inaufanya iwe shida zaidi na kutoa huduma kwa ufanisi mkubwa.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba (kushoto), akipongezana na Ofisa Mtendaji Mkuu wa TCB, Sabasaba Moshingi, baada ya kuzinduliwa huduma ya 'TCB Internet Banking', ambayo uboreshaji wake umefanywa na wataalamu wa ndani wa taasisi hiyo ya serikali. **PICHA: MTANDAO**

### WADAU WANENA

Meneja Mwandamizi Huduma za Kimtandao, Allen Manzi wa Benki ya Biashara, anafafanua maboresho waliyoyafanya ni uwekezaji wa ndani, ambao walijitegemea kwa kila kitu.

Mgeni rasmi katika uzinduzi wa huduma hiyo ya viwango vya kimataifa, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, anasema wazo la TCB kuja na ubunifu huo yenyewe, lina sifa ya kuigwa na taasisi zote za umma hasa benki za serikali.

> "Jambo hili linasaidia sana kuwajumuisha watu kwenye mifumo rasmi ya kifedha, kwa sababu ni utaratibu wa kihuduma unaomwezesha mteja kufanya malipo na kukidhi mahitaji yake ya kimiamala.

"Nimefurahi kusikia kuwa mifumo ya huduma hii ya kidigitali, pia imeunganishwa na mfumo wa MUSE ili kuzirahisishia taasisi za umma zinapofanya malipo kwa kuziondolea adha ya kwenda benki," anatamka mtendaji mkuu huyo wa Wizara ya Fedha na Mipango.

MUSE ni mfumo wa malipo wa serikali mahususi kwa ajili ya Serikali Mtandao ambao lengo lake kuu ni kuchochea matumiziya Teknoliojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kusaidia kuboresha utoaji wa huduma za umma.

"Mfumo mpya wa TCB wa huduma za kibenki kwa mtandao umeimarisha sana shughuli zetu za kibenki na kupunguza foleni za wateja kwenye matawi yetu sambamba na kuongezeka kwa miamala ya kidigitali kadri wateja wanavyoongezeka kuutumia," anaeleza Manzi na kufafanua:

"Jambo hili linasaidia sana kuwajumuisha watu kwenye mifumo rasmi ya kifedha, kwa sababu ni utaratibu wa kihuduma unaomwezesha mteja kufanya malipo na kukidhi mahitaji yake ya kimiamala."

"Hiyo ndiyo maana halisi ya huduma jumuishi za kifedha kwa mujibu wa Benki ya Dunia," anaeleza Manzi, akifafanua kwamba, kimsingi, malipo na hata kufanyika manunuzi kupitia intaneti ni suala linalohusu kupatikana urahisi na wepesi kwa huduma za kibenki na kifedha kwa ujumla.

Kwa mujibu wa Manzi, hadi sasa huduma za intaneti benki, zimeleta mapinduzi makubwa katika malipo ya kielektroniki nchini, inakubalika kwa wengi, hoja ambayo Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Tutuba, amefafanua.

Tutuba anaitafsiri kwamba ni jukwaa linalounganisha mifumo yote ya malipo kitaifa akiitaja kwa majina ya kitaalamu; GePG, TISS, TACH TIPS, SWIFT, EAPS, na SADC RTGS. Manzi anajisifu kwamba, mfumo wao wa malipo kidigitali umepokelewa vizuri sokoni na kuipandisha hadhi taasisi hiyo kongwe ya umma inavyowahudumia wananchi na uchumi wa taifa kwa ujumla.

Anataja mojawapo ya matokeo yake makubwa ni kuchangamkiwa na watumiaji wengi, Manzi akisema wengi wanavutiwa na uwezo wake wa kumfanya mtu kujiunga nayo yeye mwenyewe kidigitali. Kujaza makaratasi kwa ajili ya hilo ha kuhitajiki tena.

Hilo, analieleza kwamba, limechangia kuongezeka miamala inayohusisha mfumo wake kwa asilimia 43 kati ya mwaka jana na mwaka huu.

Kuhusu huduma za kibenki za TCB kwa njia ya mtandao wa intaneti ina utofauti wake na utaratibu wa awali, Manzi anaelezea:

"Kwanza kabisa ni rahisi kutumiwa na wateja na kwa wale wenye akaunti binafsi na zile za akiba, pia si kazi kubwa kwao kujiunga na huduma hii. Wateja wetu wakubwa wao hilo linafanyika kwa muda mfupi sana."

"Pili, ni mfumo salama ambao utaratibu wake wa maneno ya siri ya wateja si rahisi kudukuliwa kwa namna yoyote ile. Pia, una uwezo wa kukamilisha aina zote za malipo. Ikiwamo ya GePG, TISS, TT, malipo yanayohusisha viwango vikubwa vya malipo na kuhamisha fedha kutoka benki kwenda kwenye akaunti za simu za mkononi na vitu kama hivyo," anasema Manzi.

Anausifu mfumo kwamba una ufanisi, salama na upatikanaji wake ni popote na kila mahali, ukifanyika katika mazingira rafiki katika matumizi, watumiaji wakinufaika maradufu.

Vilevile, anataja faida ya kupatikana kwa nafuu, kwa wanaojiusisha na hasa biashara za nje ya nchi. Manzi anaendelea, kwamba TCB badi iko katika hatua za maboresho kupatikana kwa ufanisi maradufu.

"Kwa jinsi huduma hii ilivyochangamkiwa, tuna matumaini ya kufanya vizuri zaidi huku miamala ya kidijitali ikiongezeka kadri muda unavyoongezeka," Manzi anasema.

Benki Kuu inasema, ukuaji kwa matumizi ya mifumo ya kifedha ya kidigital kwenye miaka ya karibuni, kunachochewa zaidi na teknolojia ya simu za mkononi na kuendelea kufanya vizuri kwa uchumi wa taifa.

# Athari tabianchi si mafuriko, vimbunga pekee hata unyanyasaji kijinsia umo pia



Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi (wa tatu kushoto), akiwa pamoja na baadhi washiriki wa mafunzo ya kupinga ukatili wa kijinsia yaliyofanyika jijini Dar es Salaam. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

**INATOKA UK.13**

wengine kuambukizwa maradhi ya ngono na kwa ujumla kuwaharibia mipango na michakato ya maisha yote hayo yakiongeza umaskini, ugumu wa maisha na matatizo ambayo mzizi wake ni mabadiliko ya tabianchi.

Aidha, anasema bado tatizo la mfumo dume linaendelea kushika kasi kwa wanaume kujiona wao ndiyo wenye nguvu na uwezo katika maamuzi na uongozi kwa kutumia rasilimali ikiwamo kuuza mazao na kutumia pesa kwa manufaa yao pekee bila ya kuwashirikisha wanawake wanaolima pamoja mashamba au kuzalisha mali nyingine mfano ufugaji.

Hivyo anaitaka jamii kuacha tabia ya kupuuza maagizo na maelekezo wanayopewa kuhusu masuala mbalimbali yakiwamo ya kuboresha kilimo ili kujiepusha na masuala ya ukatili wa kijinsia na pengine wa kingono wanaofanya kwa kujua au hata kwa kutokujua.

Anawataka viongozi kuanzia ngazi ya wilaya, kata, vijiji na

> "Lengo kuu la mradi huo ni kuleta usawa katika maeneo matatu ambayo ni wanawake na uongozi na ngazi za kufanya maamuzi, ukatili wa kingono (SGBV) na kilimo na mabadiliko ya tabianchi.



Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA, Dk. Rose Reuben ambaye ni mwanahakati anayehimiza kuwapo juhudi zaidi kukomesha unyanyasaji watoto na wanawake kutokana na vyanzo mbalimbali yakiwamo mabadiliko ya tabianchi. **PICHA: TAMWA**

vitongoji sambamba na viongozi wa vituo vya taarifa na maarifa kutoa ushirikiano kwa waandishi wa habari ili kuelimisha jamii kuhusu kupinga ukatili wa kijinsia hasa ukatili wa kingono (SGBV).

Akizungumzia mradi wa RWCC Catherene anasema mradi huo unatekelezwa kwa miaka sita kuanzia mwaka 2021 hadi 2026 katika mataifa matatu ya Tanzania, Kenya na Ethiopia na kwamba hapa nchini unatekelezwa katika mikoa ya Manyara, Morogoro na Kilimanjaro.

Anasema lengo kuu la mradi huo ni kuleta usawa katika maeneo matatu ambayo ni wanawake na uongozi na ngazi za kufanya maamuzi, ukatili wa kingono (SGBV) na kilimo na mabadiliko ya tabianchi.

Dk. Rose Reuben, Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA), na mwezesha wa mafunzo hayo, yanayofanyika Dar es Salaam, anawataka wanahabari kuripoti kwa kina habari zinazohusu masuala ya kupinga ukatili wa kijinsia ili kuifanya jamii kuwa na uelewa mzuri na kuacha matendo hayo ambayo ni hatari hasa kwa watoto na kwa taifa.

Anaongeza kuwa iwapo kutakuwa na uelewa mzuri katika masuala ya jinsia jamii inaweza kuendelea kwa namna mbalimbali ikiwamo kukua kiuchumi sambamba na kutimiza malengo 17 ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

"Hata katika malengo ya maendeleo endelevu suala zima la jinsia ni jambo mtambuka na linaingia katika kila sekta kwa sababu ndiko kuna watu na linagusa wanawake na wanaume na kama kuna usawa wa jinsia tunaweza kutimiza malengo yote ya SDGs kuanzia la kwanza hadi la 17," anasema Dk. Rose.

Anakumbusha kuwa usawa wa kijinsia unalenga kufikia jitihada za kuleta usawa kati ya jinsi zote mbili na kuondokana na unyanyasaji wa aina mbalimbali uliokuwa unafanyika dhidi ya wanawake, watoto, wasichana na makundi mengine kwenye jamii, yanayotawala katika maisha ya kila siku.

Usawa wa kijinsia unahusiana na haki za binadamu, hasa za wanawake kuanzia maendeleo ya kiuchumi, kisiasa, kijamii, kielimu ambayo ni nyenzo ya kumaliza umaskini duniani hasa jamii ambamo wanawake hawana haki.

## WANENAVYO MALENGA

### KUFA NA TAI SHINGONI

ILI tusife haraka, maumivu yatushika,
Bora kufanya haraka, ya moyoni kututoka,
Kwa washauri kufika, ya kwetu kuyaanika,
Kufa na tai shingoni, twaweza kukuepuka.

Jambo gumu lakufika, kufanya kuhangaika,
Hadi moyo waumuka, na fikira zinachoka,
Kwa mtu lisipotoka, mwisho waweza pasuka,
Kufa na tai shingoni, twaweza kukuepuka.

Yaweza kufikirika, lako gumu kubebeka,
Kama vile lakufika, tangu nchi kuumbika,
Kumbe kama likisika, ni dogo la kubebeka,
Kufa na tai shingoni, twaweza kukuepuka.

Gonjwa la moyo kufika, shinikizo panda shuka,
Ni hayo umeyashika, moyo unashughulika,
Hadi pale inafika, yanashindwa vumilika,
Kufa na tai shingoni, twaweza kukuepuka.

Wanaume yasikika, wengi vifo huwashika,
Sababu yakiwafika, wabaki wasononeka,
Kwa wenza kuyaanika, aibu zinawashika,
Kufa na tai shingoni, twaweza kukuepuka.

Hili likieleweka, Kufichaficha kuchoka,
Pazuri tutapafika, shida nyingi kuondoka,
Mauti kufikafika, kwaweza sahaulika,
Kufa na tai shingoni, twaweza kukuepuka.

Wanawake twawacheka, kusema bila kuchoka,
Kumbe nyingi takataka, ambazo zinawafika,
Ndivyo zinahamishika, zisije zikawabaka,
Kufa na tai shingoni, twaweza kukuepuka.

Moyo mdogo hakika, amani yahitajika,
Mizigo ya kubebeka, kubeba yaleta shaka,
Kama haujapasuka, nyufa zaweza jengeka,
Kufa na tai shingoni, twaweza kukuepuka.

Kaka na dada amka, haya upate kushika,
Afya ni kutajirika, magonjwa kufukarika,
Yale ya kuepukika, bora yasijetushika,
Kufa na tai shingoni, twaweza kukuepuka.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**

ELIMU

NA REUBENI LUMBAGALA, DODOMA

SAMIA SCHOLARSHIPS

# Ni ukweli sasa kuwa kusoma, kufaulu sayansi inawezekana

• Wanasiasa, wazazi wafikishe ujumbe kona zote



Hali duni ya maisha inayokwamisha masomo inapungua baada ya serikali kubeba mzigo wa elimu ya msingi na sekondari, lakini pia imeanza kuwalipia gharama zote za vyuo vikuu watakaofanya vizuri kwenye kozi za sayansi. **PICHA: MTANDAO**

MAFANIKIO ya kitaaluma yanakwenda pamoja na mikakati madhubuti ili kufanikisha kutimiza malengo yaliyowekwa. Masomo ya sayansi kama Fizikia, Kemia, Baiolojia, Lishe, Kilimo na Hisabati hayasomwi kikamilifu kukiwa na hisia kuwa ni magumu au hulinganishwa na misemo kuwa ni fupa linalomshinda fisi.

Hivyo ni muhimu kuwekewa mikakati ili kuongeza ufaulu wa wanafunzi kuanzia elimu ya msingi hadi vyuo vya juu hasa kwa kuwa ipo dhana potofu miongoni mwa wanafunzi kuwa masomo ya sayansi na hisabati wengi hawayawezi kisa ni magumu.

Hisia hizo zimepelekea baadhi ya wanafunzi kuyachukia na kila mwaka kuathiri ufaulu wake kuanzia mitihani ya ndani ya shule, ngazi ya wilaya, mkoa, kanda hadi ngazi ya taifa.

Kutokana na hali hiyo, viongozi wa elimu katika ngazi mbalimbali, wamekuwa wakiweka mikakati ya kutoa motisha kwa wanafunzi watakaofanya vizuri katika masomo ya sayansi na hisabati ili kuongeza ufaulu, hatimaye kupata wataalamu wa fani mbalimbali za sayansi bila kusahau walimu wake ambao nao wanahamasishwa kwa namna tofauti.

Safari hii, Rais Samia Suluhu Hassan, ameonyesha moyo wa dhati kuinua sekta ya elimu hasa katika kuongeza chachu kwa wanafunzi ili kupenda na kufaulu masomo ya sayansi kwa kutoa ufadhili wa Samia Scholarships kwa wanafunzi watakaofaulu viwango vya juu kwenye sayansi katika mtihani wa kidato cha sita ili kuendelea vyuo vikuu katika fani hiyo.

Samia Scholarship itagharamia kwa asilimia 100 masomo ya vyuo vikuu vya Tanzania kwa wanafunzi ambao wamefaulu viwango vya juu na kupata udahili kwenye tiba, uhandisi, teknolojia na hisabati.

Kwa wanafunzi wa kike ili kupata ufadhili huu, anapaswa awe na ufaulu kwa daraja la kwanza kuanzia pointi 3 hadi 6 , wanaume wawe na daraja la kwanza kuanzia pointi 3 hadi 5 na kwa wenye mahitaji maalum wawe na ufaulu wa daraja la kwanza pointi 5 hadi 9.

Uhisani huo wa Rais utawezesha wanafunzi kupata ufadhili kwa kipindi cha kati ya miaka mitatu hadi mitano kulingana na programu wanayosoma chuoni.

Kuna mahitaji mengi yanayogharimu fedha nyingi ili kumwezesha mwanafunzi kusoma elimu ya juu, mathalani, ada, chakula na malazi, mafunzo kwa vitendo, vitabu, utafiti, bima ya afya, mahitaji maalum ya vitivo na vifaa saidizi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Samia Scholarship inagharamia mahitaji yote haya, hivyo mwanafunzi kulipiwa kila kitu, kazi kubwa kwa mwanafunzi ni kusoma kwa bidii ili kuendelea 'kufanya kweli' katika masomo yake ili kuwa sehemu ya wataalamu wa sayansi na teknolojia wa Tanzania.

Vilevile, mwanafunzi atapaswa kufaulu ufaulu wa juu usiopungua wastani wa alama zote za mitihani zikijumlishwa na kugawanywa zifikie 3.8 (3.8 GPA) ili kuendelea kuwa mnufaika wa ufadhili huu.

Akitangaza kufunguliwa kwa dirisha la maombi ya ufadhili wa Samia Scholarships, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda anasema uchambuzi huo wa wanufaika 640 wa umezingatia uwiano wa wasichana 244 sawa na asilimia 38 na wavulana 396 sawa na asilimia 62 na kwamba wanafunzi kutoka shule za serikali ni 396 sawa na asilimia 62 na shule binafsi ni 244 sawa na asilimia 38 ikijumuisha Tanzania nzima.

"Ndugu wanafunzi, ni wakati sasa wa kubadili mitizamo kuhusu masomo ya sayansi kwani wanufaika wa Samia Scholarship ni kielelezo kuwa inawezekana kufaulu masomo haya."

Cha muhimu ni kuwa na ndoto za kusoma fani za sayansi, kwa bidii, kuzingatia kikamilifu mafundisho ya walimu ndani na nje ya darasa bila kusahau kumtanguliza Mungu katika masomo na juhudi zote.

Ufadhili huo utawapunguzia mzigo wazazi na walezi ambao wanawajibika kulipia gharama za elimu za watoto wao na pengine wale ambao hawana uwezo.

Hivyo basi, wazazi na walezi wanayo nafasi ya kuongeza hamasa kwa watoto wao kupenda masomo ya sayansi ili kupata fursa hii inayotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan.

> Ndugu wanafunzi, ni wakati sasa wa kubadili mitizamo kuhusu masomo ya sayansi kwani wanufaika wa Samia Scholarship ni kielelezo kuwa inawezekana kufaulu masomo haya.

Kwa kuanzia katika mwaka wa masomo 2022/2023, serikali imetenga bilioni tatu kufadhili wanafunzi, Profesa Mkenda anasema na kuongeza: "Tutakapoingia mwaka wa pili inaweza kuwa shilingi bilioni sita na zitaendelea kuongezeka kulingana na uhitaji".

Serikali inafanya jitihada za kuongeza vitabu shuleni, kujenga na kukarabati maabara, kununua vifaa vyake na kuajiri walimu wa sayansi, ili kuongeza kasi ya wanafunzi kupenda na kufaulu masomo hayo.

Wanafunzi kwa upande wao wanao wajibu wa kusoma kwa bidii ili kufanya vizuri katika masomo yao na hatimaye kuitumikia nchi yao kwa kuwa sehemu ya wataalamu wa fani za sayansi kama vile uhandisi, tiba, hisabati na teknolojia kwa maendeleo endelevu.

***Mwandishi ni Mwalimu wa Sekondari ya Mlali iliyoko Kongwa mkoani Dodoma.***

***Maoni : 0620 800 462.***

# HABARI PICHANI



Wafanyabiashara wakiwa wameegesha mafurushi ya bidhaa zao jana, kabla ya kupanga kwenye meza katika mnada unaofanyika kila Jumamosi Loliondo, Kibaha mkoani Pwani. **PICHA: SABATO KASIKA**



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya KCB Tanzania Limited, Cosmas Kimario, akimpa zawadi mmoja wa wateja wa benki hiyo, jijini Dar es Salaam katika Wiki ya Huduma kwa Wateja iliyohitimishwa mwishoni mwa wiki. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**



Dereva wa bodaboda akipita katika barabara ya mabasi ya mwendokasi Kimara Baruti Dar es Salaam juzi, wakati Jeshi la Polisi limeshataja vyombo vya moto vinavyoruhusiwa kupita kwa dharura katika barabara hiyo. **PICHA: SABATO KASIKA**



Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete, akipata maelezo kwa Meneja wa Masoko wa Kampuni ya Global Land Solutions Ltd, Murtaza Adamjee, huku Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Zainuddin Adamjee akishuhudia katika maonyesho ya 3 ya uwekezaji na biashara yanayoendelea mkoani Pwani, Halmashauri ya Mji wa Kibaha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Ofisa Ardhi Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Selestin Liweje (kulia), akizungumza na wananchi wa Kata ya Majengo wilayani humo katika shughuli ya kugawa hati miliki 131 za viwanja kwa wananchi juzi katika viwanja vya Shule ya Msingi Mdote. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



## Wakurugenzi h'shauri waonywa matumizi fedha za serikali

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

KATIBU Tawala Mkoa wa Songwe, Happines Seneda, amewataka wakurugenzi wa halmashauri za mkoa huo, kuacha kutumia fedha za serikali kinyume na maelekezo ili zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa.

Aliyasema hayo wakati wa kikao cha kujadili afya ya msingi kwa jamii kilichowahusisha wadau mbalimbali wakiwamo wakuu wa idara, wakurugenzi, wakuu wa wilaya, maofisa tawala na makatibu.

Alisema serikali ilipeleka fedha kwa ajili ya utoaji wa elimu ya lishe katika halmashauri zote lakini zipo baadhi ya halmashauri ikiwamo Momba imetumia fedha hizo kinyume.

Alisema licha ya Mkoa wa Songwe kulima mazao lakini hali ya udumavu ipo juu na kwamba mikakati ya serikali iliwekwa ikiwamo utoaji wa elimu kuanzia ngazi za vijiji, kwamba fedha zilitolewa kuhakikisha hilo linafanikiwa.

"Momba mmefanya kitu cha ovyo, serikali ilileta fedha katika bajeti iliyopita kwa ajili ya kufanikisha elimu ya lishe inawafikia wananchi lakini hamkufanya hivyo na fedha Sh.milioni 90 mkazitumia kwa matumizi mengine mnayo yajua ninyi, mmekwamisha jitihada za serikali hilo lisijirudie,"alionya Seneda. Alisema mwaka 2022, Mkoa wa Songwe umepokea Sh.milioni 327 kwa ajili ya kuwezesha chanjo zote, kusisitiza kuwa fedha hizo zitumike kama zilivyoelekezwa na kwamba kinyume na hapo hatua kali za kisheria zitachukuliwa.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Waziri Kindamba, alisema ni aibu kwa mkoa unaolima mazao mengi lakini unaongoza kwa udumavu, jambo ambalo alisema halikubaliki na kwamba ipo haja wakuu wa wilaya, wakurugenzi na viongozi wengine wakiwamo wa dini kuhakikisha elimu ya lishe inawafikia wananchi.

Alisema chakula bora siyo chakula cha kujaza tumbo bali ni kile kinachozingatia makundi maalum ya vyakula ikiwamo matunda, mboga na kufanya mazoezi.

# Watanzania wahamasishwa unywaji zaidi wa kahawa

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

WATANZANIA wamehamasishwa unywaji wa kahawa ili kuongeza mnyororo wa thamani wa bidhaa hiyo ambao utawasaidia wafanyabiashara na wakulima kujiongezea kipato.

Wito huo umetolewa na Meneja wa Kituo cha Utafiti wa zao la Kahawa nchini (TaCRI), Nyanda za Juu Kusini, Dismas Pangalasi, wakati akizungumza na Nipashe kuhusu mwitikio wa wananchi kunywa kahawa.

Alisema ni asilimia saba tu ya wananchi wanaokunywa kahawa na kwamba idadi hiyo ni ndogo kuliko uzalishaji wenyewe.

"Pamoja na kinywaji cha kahawa kuwa kinywaji kinachotumiwa na watu wengi duniani baada ya maji, Tanzania ni asilimia saba tu ya kahawa ambayo huzalishwa hutumika nchini kama kinywaji

"Zipo faida nyingi za unywaji wa kahawa ikiwamo kuwakutanisha wadau mbalimbali ambao husaidia kuimarisha mnyororo wa thamani ambao humnufaisha mkulima pamoja na mfanyabiashara."

Akizungumzia unywaji wa kahawa, Mkuu wa Wilaya ya Ileje, Anna Gidarya alisema serikali inasisitiza kilimo biashara, hivyo aliwataka Watanzania kuachana na imani potofu zinazoelezwa kuwa kahawa ina madhara kiafya.

"Tukiimarisha soko la ndani kwa kunywa kahawa yetu, kahawa itakuwa na manufaa zaidi kwa sababu ushindani utaongezeka kati ya soko la ndani na soko la nje, hivyo kumsaidia zaidi mkulima wa Tanzania na kutengeneza ajira kwa vijana," alieleza Gidarya.

Aliongeza kuwa kahawa ni kinywaji kinachotumiwa zaidi duniani takwimu zinatuonyesha kuwa vikombe bilioni 2.7 hunywewa kila siku ni muhimu tukahamasishana kunywa ili kuongeza thamani ya zao hilo kwa kuwawezesha wafanyabiashara na wakulima kujiongezea kipato.

Gidarya aliwataka vijana na wanawake kuingia kwenye uzalishaji wa zao la kahawa ili kuondokana na umaskini, kwamba kwa sasa ni asilimia 18 tu ya vijana na wanawake wanaojishughulisha na uzalishaji kahawa mkoani humo.

Mkulima kutoka Kijiji cha Shaji, Lucy Shonza, aliiomba serikali kuongeza maofisa ugani kwenye maeneo yao ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo.



Mkuu wa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, Reuben Mfune (kushoto), akisaini mkataba wa afua za lishe unaolenga kupunguza udumavu jana kwenye ukumbi wa Mkapa. Anayeshuhudia ni Mkuu wa Mkoa, Juma Homera (kulia). **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wanafunzi kutokupewa chakula shuleni chanzo kushuka ufaulu

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

KUTOKUWAPO kwa chakula cha mchana kwenye shule za msingi na sekondari wilayani Songwe imetajwa kuwa ni moja ya sababu zinazochangia kupunguza ufaulu kwa wanafunzi.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Ofisa Elimu Shule za Msingi wilayani humo, Michael Nzunda, kueleza kuwa licha ya kutoa maelezo kwa wazazi na walezi lakini hakuna utekelezaji.

Alisema ajenda ya chakula shuleni ipo kwa muda mrefu, lakini hakuna mwitikio wa wazazi kutekeleza licha ya kutumia mikutano ya hadhara, vikao vya madiwani lakini bado hakuna mwitikio.

"Wilaya yetu imekuwa ikifanya vibaya kwenye mitihani mbalimbali ya kitaifa, miongoni mwa sababu zinazochangia ni kukosekana kwa chakula shuleni njia ya kukabiliana na hilo ni kuhimiza chakula lakini mwitikio ni mdogo tunaomba sana wazazi mtuunge mkono," alisema Nzunda.

Kupitia kikao cha kujadili vikwazo vinavyochangia wanafunzi kufanya vibaya kwenye mitihani yao, baadhi ya wadau wakaiomba halmashauri kutunga sheria ndogo ambayo itawabana wazazi na walezi kuchangia chakula kwa lazima.

Samwel Mwala, alisema rekodi zinaonesha kuwa shule nyingi zinazopika vyakula ndizo zinaongoza kwa ufaulu hivyo jukumu hilo lazima lisimamiwe wazazi wenyewe ili watoto wapate chakula cha asubuhi na mchana.

Mkuu wa wilaya hiyo, Simon Simalenga, alisema chakula kwa shule za msingi na sekondari ni lazima na kuangiza waratibu wa elimu pamoja na maofisa elimu kusimamia suala hilo.

Aidha, aliwataka watumishi wa wilaya hiyo suala la chakula kuwa ajenda ili kuongeza morali kwa wananchi kuchangia chakula shuleni kwa ajili ya kuongeza ufaulu kwa wanafunzi.

Mwalimu wa Shule ya Msingi Mkwajuni, Anna Samir, alisema ni ngumu kufikia malengo ya kuwawezesha wanafunzi kufanya vizuri kwenye masomo yao, hasa wanaotoka kwenye kaya maskini kutimiza ndoto zao endapo wazazi wanagoma kuchangia vyakula shuleni.

Hivi karibuni Kikao cha Kamati ya Lishe Mkoa wa Songwe, kiliazimia shule zote za msingi na sekondari kuanza kupanda bustani za mboga na matunda Ili kuimarisha lishe kwa watoto.





# JKT yaagizwa kuzalisha chakula kuipunguzia mzigo serikali

**Na Renatha Msungu,**
CHAMWINO

MKUU wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Jacob Mkunda amelitaka Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kuzalisha chakula kwa wingi ili kuipunguzia serikali gharama za chakula.

Alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki wakati JKT ikikabidhiwa zana za kilimo yakiwamo matrekta, mashine za kupandia na kuvunia katika hafla iliyofanyika makao makuu ya jeshi hilo.

Alisema JKT linapaswa kuanzisha viwanda vya kimkakati ili kuhakikisha wanazalisha chakula kwa wingi na kuimarisha usalama wa chakula.

Mkuu huyo alisema wanapaswa kuhakikisha wanafanya kilimo kwa malengo, ikiwamo upanuzi wa mashamba kwa kutumia teknolojia na utaalamu wa kilimo wanachofanya katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

“Mnahitajika kufanya upanuzi wa maeneo ya mashamba zana mnazo zidisheni kufanya kilimo chenye tija,”alisema Jenerali Mkunda.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo mkakati, Mifugo na Uvuvi, Brigedia Jenerali Hassan Mabena, alisema jeshi hilo limejipanga hadi kufikia 2025 wawe na uwezo wa kujitosheleza kwa chakula.

Brigedia Jenerali Mabena alisema wamejipanga kuhakikisha jeshi hilo linajitosheleza kwa chakula ili kuipunguzia gharama serikali ya chakula.

Alisema wanaishukuru Serikali na Wizara ya Ulinzi kutokana na kuwakabidhi bidhaa hizo ambazo wanaamini zitatumika vyema katika upanuzi wa kilimo.

“Tunashukuru kuongezewa zana za kilimo ndani ya JKT hii inazidi kuchochea hari ya kufanya kilimo chenye tija ndani ya JKT,” alisema Brigedia Jenerali Mabena.

Alisema lengo lao ni kuona JKT inazalisha chakula cha kutosha ndani ya jeshi hilo pamoja na kusambaza nje ya jeshi.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi, Dk. Faraji Mnyepe, alisema wizara hiyo itahakikisha JKT inaendelea kupata zana za kisasa na bora za kilimo ili waendelee kufanya kilimo chenye tija hapa nchini.

Dk.Mnyepe alisema uzalishaji wenye tija utasaidia kuzidi kuimarisha usalama wa chakula hapa nchini pamoja na upatikanaji wa chakula bora ndani ya nchi.



Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana (kushoto), akimkabidhi mkoba wenye nyaraka za vitendea kazi Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa Mfuko wa Misutu Tanzania, Prof. Shaban Chamshama (kulia), jijini Dodoma jana, (wa pili kulia) ni Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# ‘Wapuuzeni wanaotoa vitisho bima ya afya’

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

SERIKALI imewaomba wananchi kuunga mkono suala la bima ya afya kwa wote na kupuuza vitisho juu ya suala hilo kwa kuwa limefanyiwa kazi kwa zaidi ya miaka 10.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Prof. Abel Makubi, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza kwenye Kituo cha Televisheni cha Taifa (TBC) kuhusu Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote uliosomwa bungeni hivi karibuni.

Alisema muswada huo umebuniwa kwa takribani miaka 10 na sasa imefikishwa hatua ya kuingia bungeni ili kuweka mfumo imara wa wananchi kupata huduma ya afya.

“Wananchi wasitishwe na wala usiogope juu ya sheria hii, tunahitaji kila Mtanzania awe na bima ya afya na hata kwa wananchi wasio na uwezo, serikali imeweka mazingira ya kuwatambua na kuwapa kadi maalum za kupata huduma za matibabu, hivyo tuunge mkono suala hili ambalo ndiyo mkombozi mkubwa katika afya zetu,” alisema Prof. Makubi.

Alisema kuwapo kwa sheria hiyo wananchi wengi watakuwa na uhakika wa kupata huduma za matibabu wakati wanapozihitaji.

“Ili kila mwananchi aweze kushiriki shughuli za maendeleo ni lazima awe na uhakika wa afya yake kupitia uhakika wa kupata matibabu, lakini sheria hii itasaidia kuwaepusha wananchi kuingia kwenye janga la umaskini ambalo hutokana na gharama kubwa za matibabu hivyo jambo hili ni muhimu na tulipe kipaumbele,” alisisitiza Prof. Makubi.

Alieleza kuwa sheria hiyo inakwenda kuweka usawa katika kitita cha mafao kwa wananchi watakaojiunga na bima ya afya lakini kuwa na fursa ya wananchi wote kupata huduma katika vituo vyote vya kutolea huduma vya umma na binafsi kuanzia ngazi ya zahanati.

Hata hivyo, alisema sheria hiyo itaipa nguvu Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kuratibu na kudhibiti bima za afya kutoa huduma bora kwa wananchi.

“Uamuzi huu ni muhimu kwa kuwa asilimia 85 ya Watanzania walikuwa nje ya mfumo wa bima na kutokuwa na uhakika wa kupata huduma za afya, ilikuwa ni adha kubwa kwa wananchi,”alisema.

Alisema kuwa sheria itaweka viwango vya michango kulingana na hali halisi ya gharama za utoaji wa huduma za afya, kwamba viwango pendekezwa kwa sasa ni Sh. 340,000 kwa kaya ya watu sita.

## Vijiji vya Seluka, Wiyenzele vyakumbwa ukosefu wa maji

**Na Augusta Njoji,**
MPWAPWA

WANANCHI wa vijiji vya Seluka na Wiyenzele wilayani Mpwapwa, wanakabiliwa na ukosefu wa huduma ya majisafi kutokana na mradi wa maji uliyoko kushindwa kutoa maji hali inayohatarisha afya zao.

Wakieleza malalamiko yao kwa Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, mwishoni mwa wiki, wananchi hao walieleza kuwa wamekuwa wakipata matatizo ya ukosefu wa maji kwa muda mrefu.

Mkazi wa Seluka, Yona Kutala, alisema wananchi wa Seluka wanakabiliwa na kero ya maji hali inayosababisha kukosa hata ya kupigia mswaki.

“Mheshimiwa Waziri utaona kama vile wananchi wa Seluka wamenuna, wanashindwa kucheka kwasababu meno yao hayapo sawa, kupiga meno mswaki kunahitaji maji,”alisema.

Mkazi mwingine, Esther Mgonela, alisema wanawake ndiyo waathirika wakuu wa tatizo hilo kutokana na kushindwa kupika chakula kwa kukosa maji.

“Mwanaume akija akiuliza chakula kipo wapi unamwambia hakuna kwasababu ya shida ya maji hakuelewi na unaambulia kipigo,”alisema.

Mbunge wa Kibakwe na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene, alisema mradi wa maji Seluka ulikamilika na watu walikuwa na matumaini makubwa lakini huduma haipo kutokana na tatizo la ukosefu wa umeme.

Kufuatia hali hiyo, Waziri wa Maji, Aweso, alitoa siku 30 kwa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), kuhakikisha huduma ya maji inatolewa bila kuwapo na kisingizio chochote.

Alisema kama Meneja huyo atashindwa kuhakikisha huduma ya maji inapatikana kwenye eneo hilo atatafuta kazi ya kufanya. Awali, Meneja wa Wakala huo, Cyprian Warioba, alisema kutokana na tatizo la ukosefu wa umeme wa kuendesha mradi huo waliliomba Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kufikisha huduma kwenye eneo hilo.

Alisema; “Kuhusu matatizo ya huduma ya maji mtandao uliopo ni mdogo na kijiji kimetanuka, kutokana na ongezeko la watu”.

# Watakiwa kufanya mazoezi kujikinga na magonjwa

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI wa Kinga na Elimu ya Afya Zanzibar, Dk. Salim Slim, amesema ni vyema jamii kuweka mfumo madhubuti wa kufanya mazoezi ili kujikinga na maradhi ikiwamo magonjwa ya afya ya akili.

Alitoa rai hiyo juzi Kinazini Mjini Zanzibar baada ya kumalizika kwa matembezi maalum ya kuunga mkono Siku ya Afya ya Akili Duniani.

Alisema ili mtu awe na afya nzuri ni lazima awe na mfumo mzuri wa kufanya mazoezi na bila ya kufanya hivyo, mfumo wa damu utakua mzito na kusababisha kupata madhara ya kupoteza kumbukumbu.

"Ikiwa hatufanyi mazoezi katika maisha yetu angalau kwa dakika 20 kwa kila siku damu itaganda na kuweza kushindwa kufanya kazi vizuri baada ya hapo kinachofuata ni maradhi kutokana na kuganda kwa damu katika miili yetu," alisema Dk. Slim.

Alisema kuwa mfumo wa kufanya kazi kwa kutofanya mazoezi unaathiri mwenendo wa afya katika jamii, hivyo kila mtu anapaswa kuangalia hali ya maisha kwa kufanya mazoezi.

"Wafanyakazi wengi siku hizi wamejiachia sana, kila mtu anatumia usafiri sehemu ndogo usafiri uwe wa binafsi au daladala hii ni sababu kubwa inayosababisha watu kupata maradhi,"alisema.

Hata hivyo, aliwashukuru wadau wa afya kutoka Umoja wa Mataifa ( UN) kwa kuleta wazo la kuanzisha mazoezi kwani kufanya hivyo kunaboresha afya ya binadamu.

Daktari wa Dhamana wa Kitengo cha Magonjwa ya Akili, Hospitali ya Kidongo Chekundu, Khadija Abdulrahman, alisema kuwa mazoezi yana uhusiano mkubwa na afya ya akili katika maisha ya kila siku.

Alisema kuwa watu wengi katika jamii hasa wafanyakazi hukaa muda mrefu bila kufanya mazoezi, kati yao wanakua na msongo wa mawazo, hivyo kufanya mazoezi kutawasaidia kuondosha vichochezi vya magonjwa ya akili na mengine ikiwamo kisukari na shinikizo la damu.

# 'Serikali iko makini kuhusu upatikanaji chakula nchini'

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdullah, amesema serikali iko makini kupanga na kutekeleza mipango yake kwa kutilia maanani suala la ongezeko la idadi ya watu kwa kutatua changamoto ya upatikanaji na kujitosheleza kwa chakula nchini.

Aliyasema hayo jana wakati akisoma hotuba kwa niaba ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi katika ufunguzi wa maonesho ya Siku ya Chakula Duniani yaliyofanyika katika viwanja vya Chamanangwe, Mkoa wa Kaskazini, Pemba.

Alisema katika kutekeleza mipango hiyo serikali imeanzisha taasisi za utafiti wa kilimo na mifugo pamoja na wakala wa matrekta na zana nyingine za kilimo kwa lengo la kutatua changamoto zinazoikabili sekta hiyo na kubuni njia bora za uzalishaji kulingana na mazingira.

Aliwataka wananchi na wakulima kuchukua tahadhari katika uzalishaji wa mazao ya chakula na taarifa za hali ya hewa zinaonesha kuwapo kwa upungufu wa mvua za vuli.

Alisema kuwa mara nyingi nchi hupatwa na hali kama hiyo na kuwataka wakulima kupanda mazao yanayoweza kuhimili hali ya hewa na kutumia mbegu za mazao yanayoweza kukomaa kama muhogo, viazi vitamu, mtama na jamii ya kunde.

Aliwaasa wafugaji kufuga mifugo ambayo wanaweza kuihudumia kwa malisho na kuhifadhi sehemu zote za malisho kwa maslahi ya wanyama hao.

Aliwataka wananchi na wadau wengine kuacha kuvamia maeneo ya kilimo na misitu pamoja na ujenzi holela kwa visingizio vya uwekezaji na badala yake kufuata utaratibu wa ujenzi wa makazi kwa maslahi ya nchi.

"Maeneo yote ya kilimo na mifugo pamoja na misitu ni mali, hivyo ni vyema kuyatunza na kuyatumia kwa kuongeza tija na juhudi katika uzalishaji wa chakula ili kujikinga na balaa la njaa," alisema.

Pia alisema serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo itahakikisha inasimamia vyema sekta ya kilimo ili kuongeza uzalishaji wa chakula pamoja na kuwa karibu na wakulima na wafugaji kwa kuwapa huduma, nyenzo na utaalamu ili kuhakikisha nchi inazalisha chakula kingi na chenye kutosheleza pamoja na kuiweka nchi katika hali ya kuwa na uhakika wa chakula.

Alisisitiza umuhimu wa kuweka kipaumbele katika ulaji wa chakula bora chenye lishe na kuwataka wananchi kujenga utamaduni wa kula vyakula bora, ikiwamo unywaji wa maziwa hususan watoto walio chini ya miaka mitano ili kupata watu wenye afya, akili na utaalamu unaohitajika.

Naye Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, alisema wizara imejipanga kuhakikisha inaongeza ufanisi mzuri katika upatikanaji wa chakula na lishe bora kwa wananchi wote.

Shamata alisema kuwa wizara kupitia maonesho hayo itatoa elimu kwa wananchi wote kujifunza kulima kilimo cha kisasa na chenye tija kwa maslahi ya taifa.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Wizara ya hiyo, Seif Shabani Mwinyi, alisema maonesho hayo yamefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na umoja na ushirikiano uliopo baina ya serikali na mashirika binafsi.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akiwa pamoja na kamati maalum (kikosi kazi) ya kuchambua maoni ya washiriki wa mkutano wa wadau wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa, baada ya kumalizika kwa hafla ya kukabidhiwa ripoti ya maoni Ikulu Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# TAMWA yasikitishwa wanawake kuachwa kwenye uteuzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, kimesikitishwa na uteuzi uliofanyika hivi karibuni wa wajumbe saba wa Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Zanzibar ambao wote ni wanaume.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari, Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema, bodi hiyo itasimamia masuala ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi yakiwamo ya kutoa ushauri kwa serikali na sekta binafsi, kutoa elimu, mitaji, mikopo, kuunganisha taasisi, kushajihisha kufanyika kwa utafiti na kuweka mifumo ya ufuatiliaji na taarifa.

Alisema kuundwa kwa Mamlaka ya Uwezeshaji chini ya Sheria Namba 2 ya 2022 ya Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, kumetokana na azma ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi kuinua hali za uwezeshaji wa wananchi hasa wanawake ambao kwa miaka mingi wapo nyuma kiuchumi.


Alisema Mwenyekiti wa Bodi hiyo ameteuliwa na Rais na kufuatiwa uteuzi wa wajumbe wengine sita wote wanaume pia uliofanywa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga.

Alisema kuundwa kwa bodi hiyo ambayo haijazingatia uwapo wa wanawake kunaleta wasiwasi wa kufikiwa kwa malengo hayo ya uwezeshaji kwa wanawake ambao vikwazo vinavyowakabili ni vingi zaidi na vinahitaji uchambuzi wa kina na sauti za wanawake wenyewe ili kuvikwamua.

"Kwa mfano kutokana na historia na mwenendo wa kijamii, wanawake wengi hawakuweza kupata elimu rasmi, kuunda mitandao na kuwa na ujuzi wa kupatana, huku wengi wao wakiwa pia hawana umiliki wa mali isiyohamishika ambayo hutumika kama ni dhamana katika kupata mikopo,"alisema.

Alisema wanawake wanahitaji kufidiwa kwa muda mwingi wanaotumia kufanya majukumu ya nyumbani ambayo hayahusishi kipato cha fedha.

Hivyo alishauri mamlaka ya uteuzi kuangalia tena uteuzi huo ili kuziba pengo hilo la uwakilishi.





# Kijiji chaiangukia serikali kuomba ujenzi zahanati

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

KINAMAMA wa Kijiji cha Mwandutu wilayani Shinyanga, wameomba serikali kukamilisha kwa haraka ujenzi wa zahanati ya kijiji hicho, ili kuondokana na adha ya kujifungulia njiani.

Walieleza kilio hicho juzi wakati wa ziara ya Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko na kuiomba serikali iwakamilishie ujenzi wa zahanati hiyo.

Walisema wajawazito wanataabika wakati wa kujifungua hatua inayosababisha baadhi yao kujifungulia njiani.

Akiwasilisha kero hiyo kwa niaba ya kinamama wenzake, Batolo Nhule, alisema huduma ya afya inapokuwa karibu ni msaada mkubwa kwa wajawazito kujifungua salama, ndiyo maana wananchi wa kijiji hicho walihamasika kuanza ujenzi wa zahanati kwa nguvu zao, sasa wanaiomba serikali iwakamilishe na kuanza kutoa huduma.

Alieleza kuwa zahanati ya kijiji hicho cha Mwandutu ilianza kujengwa mwaka 2012 kwa nguvu za wananchi na mpaka sasa imeshapauliwa akiiomba serikali kuikamilisha kwa wakati ili waanze kupata huduma karibu yao.

Mhudumu wa Afya, Joyce Pambe, alisema ukosefu wa zahanati ni tatizo kubwa kijijini humo na wamekuwa wakitoa msaada wa kuzalisha wanawake wakiwa njiani na wengine majumbani ili kuokoa maisha yao, pamoja na kuwapatia pia elimu ya afya ya uzazi na uzazi wa mpango.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, aliwapongeza wananchi wa kijiji hicho kwa kujitoa kuanza ujenzi wa zahanati hiyo na kubainisha kuwa serikali itajitahidi kutenga fedha kwa ajili ya kuikamilisha ili kuwaepusha wajawazito kufuata huduma za afya mbali.



Baadhi ya wafanyabiashara wadogo maarufu machinga, wakiendelea na biashara zao katikati ya Jiji la Mwanza baada ya kuondolewa mjini na kutengewa maeneo ya pembezoni kwa ajili ya kufanyia biashara. **PICHA: VITUS**

# Wakulima Muleba walilia elimu ya maofisa ugani

**Na Lilian Lugakingira,**
MULEBA

BAADHI ya wakulima katika Wilaya ya Muleba, mkoani Kagera wameiomba serikali kuongeza idadi ya maofisa ugani vijijini, kuwapatia elimu ya mazao bora ya chakula na biashara ili kuboresha kilimo vijijini.

Waliyasema hayo juzi wakati wa ugawaji wa mbolea ya ruzuku kwa wananchi, wakisema kuwapo kwa maofisa ugani vijijini kutasaidia kuboresha kilimo ikiwa ni pamoja na kupokea elimu ya upandaji mazao mchanganyiko, tofauti na migomba na kahawa kama ilivyozoeleka.

Mkulima kutoka Kijiji cha Nshamba, Leonidas Kitambi, alisema uwapo wa maofisa ugani wa kutosha utawawezesha kulima kwa tija na kuinua wakulima kiuchumi kupitia kilimo.

Kitambi alisema, wakulima wanatumia nguvu nyingi kuzalisha lakini tija inakuwa ni finyu kutokana na upatikanaji wa pembejeo kuwa tatizo, pamoja na mbolea za madukani kuuzwa kwa gharama kubwa.

"Tunaishukuru serikali kwa kutuletea mbolea hii ambayo tunanunua mfuko mmoja kwa shilingi 70,000, tofauti na bei ya madukani ambayo ni kati ya shilingi 140,000 hadi 150,000 kwa mfuko hii itatusaidia kufanya kilimo chenye tija." alisema.

Mkulima Christopher Gabriel kutoka kitongoji cha Igabiro, aliiomba serikali kuhakikisha mbolea hiyo inawafikia wakulima mapema ili waitumie wakati wa kupanda na kukuzia lengo likiwa ni kupata mavuno mengi na kuepukana na baa la njaa.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Muleba, Greison Mwengu, alisema kwa sasa wamepokea mbolea ya awali ambayo ni tani 10, kwamba lengo ni kuletea tani 2,628 ambazo ndiyo mahitaji halisi ya wilaya hiyo.

"Niwaombe wakulima wote tujitokeze kwa wingi tufike hapa chama cha msingi cha TUKUTUKU, tununue mifuko ya mbolea kwa gharama nafuu yenye punguzo la serikali, maana manufaa yake ni makubwa katika kilimo," alisema.

Mkuu wa Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi katika wilaya hiyo, Charles Ntaki, alisema wamepewa malengo ya kusajili wakulima 59,000, lakini hadi sasa wamesajiliwa wakulima 7,065 wanaotarajia kupokea mbolea hiyo, huku wakulima wakiendelea kuhimizwa kujisajili.

"Wilaya yetu bado kuna kazi kubwa ya kusajili wakulima na kuwapandisha hadhi kwenye mfumo ili waweze kusomeka, tunaendelea kuwahamasisha wajitokeze maana mbolea hii ina uwezo wa kuhudumia mazao mbalimbali ikiwamo mahindi, mpunga, kahawa, migomba, mazao ya bustani na maparachichi," alisema.

# Ukosefu wataalamu lugha za alama mahakamani wakwamisha mashauri

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HAKIMU Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Kahama, Edmund Kente, amesema ukosefu wa wataalamu wa lugha za alama katika mahakama kunasababisha kuchelewa kumalizika kwa mashauri yanayohusu watu wenye ulemavu wa kusikia.

Amesema hali hiyo inailazimu mahakama kuwatumia watumishi au walimu wanaojua lugha hiyo kuendesha kesi.

Alibainisha hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari na kueleza wanavyosumbuka kuendesha mashauri hayo.

Aliiomba serikali kutatua tatizo hilo kwa kuwaajiri wataalamu wenye ujuzi wa lugha za alama katika kila mahakama na ikiwezekana wawekewe ofisi zao ili kuepusha usumbufu na ucheleweshaji wa mashauri ya namna hiyo.

Alisema wanapopata kesi zinazohusu watu wenye ulemavu wa kusikia katika mahakama, inawalazimu kuandika barua kwa wakurugenzi wa halmashauri kuomba walimu au watumishi ambao wamesomea lugha za alama kutafasiri wakati wa uendeshaji wa shauri na wakikosekana wanamuomba Msajili wa Mahakama.

Kente alisema wakati akiwa Hakimu Wilaya ya Magu, jijini Mwanza, kulitokea kesi ya ubakaji ya mtu mwenye ulemavu wa kusikia, aliandika barua kwa mkurugenzi ya kuomba mtumishi mwenye kujua kutafasiri lugha ya alama, alipatikana na kesi iliendeshwa na mhusika alikutwa na hatia na kufungwa miaka 30 jela.Alisema shauri la pili lilishindwa kumalizika kwa wakati baada ya mtumishi aliyepewa kutafasiri lugha wakati wa kuendesha shauri kutokuwa na uwezo mkubwa wa kutambua yanayozungumzwa na mwenye ulemavu hali ambayo ilifanya kuomba mwingine kwa Msajili wa Mahakama Kuu.

"Tunaomba serikali kuajiri watu ambao wamesomea lugha za alama katika mahakama zetu na ni vyema wakawa na ofisi ndani ya mahakama ili tunapopokea mashauri yanayohusu walemavu wa kusikia, tusihangaike kuwatafuta wakalimani kwa wakurugenzi wa halmashauri," alisema Kente.

Alisema Wilaya ya Kahama bado haijapata mashauri ambayo yanawahusu wenye ulemavu wa aina hiyo, watakapoyapata watalazimika kumwomba Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama, Anderson Msumba mtumishi anayefahamu lugha ya alama na kuendesha kesi.

Ofisa Elimu, Elimu Maalumu wa Manispaa hiyo, Agnes Ntalimbo, alisema idara yake ina walimu wanane wanaojua kuzungumza lugha ya alama kwa usahihi, hivyo inapotokea shauri wasisite kuwasiliana na uongozi ili kupata mwalimu wa kutafasiri na mteja wao akapata haki yake.

BURUDANI

# Cannon atimiza miaka 42, watoto 10

**LOS ANGELES, Marekani**

MCHEKESHAJI na rapa, Nick Cannon wa Marekani mwishoni mwa wiki alisherehekea kutimiza umri wake wa miaka 42, tangu kuzaliwa kwake, huku akipokea ujumbe kwa kumtakia afya njema kutoka kwa mama wa watoto wake 10, wakati huu akitarajia mtoto wa 11.

Cannon aliyetimiza umri huo Jumamosi, alimwagiwa salamu za heri kutoka kwa mama wa watoto wake wote.

"Najua unachukia siku yako ya kuzaliwa, lakini nitakuadhimisha kila mwaka milele," aliandika mwanamitindo, Bre Tiesi kwenye Instagram, ambaye amezaa naye mtoto wa kiume aliyepewa jina la Legendary.

"Asante kwa jambo bora zaidi ambalo limewahi kunipata, tunakupenda. Hongera kwa maisha ya upendo na kumbukumbu nilizopata kutoka kwako maishani," aliongeza.

Pia alipata ujumbe mtamu kutoka kwa Abby De La Rosa ambaye amezaa naye mapacha, Zillion na Zion wenye umri wa mwaka mmoja, huku pia akiwa mjamzito na wakitarajia mtoto mwingine ambaye sasa atakuwa ni wa 11.

Cannon pia alitumia ukurasa wake wa Instagram kuwashukuru mama wa watoto wake hao kwa kumtakia heri ya siku yake ya kuzaliwa na alifichua kwamba, alitumia siku nzima na mmoja wa watoto wake wakubwa, Monroe mwenye umri wa miaka 11, ambaye alizaa na mke wake wa zamani, Mariah Carey.

Katika video aliyoiweka kwenye Instagram, Monroe alionekana akiruka juu ya mpira akifanya mazoezi, huku Cannon akiwaambia wafuasi wake kwamba mwanawe huyo atakuwa mmoja wa wachezaji bora wa mpira wa kikapu duniani.

Watoto wa kwanza wa Cannon, mapacha ni Morocco na Monroe, walizaliwa Aprili 30, 2011 akizaa na mwimbaji Carey ambaye alimuoa kwa ndoa.

Baada ya kutengana kwake mwaka 2004 na Carey, alimchumbia mwanamitindo Brittany Bell, ambaye walizaa naye mtoto wa kiume, Golden mnamo Februari 21, 2017, akifuatiwa na binti Powerful Queen mnamo Desemba 2020.

Cannon alipata seti yake ya pili ya mapacha, Zion na Zillion aliozaa na De La Rosa mnamo Juni 2021. Cannon kisha alifichua mnamo Septemba 2022 kwamba amepata mtoto wa tisa aliyezaa na Lanisha Cole ambaye amempa jina la Walimwita Onyx.

Baadaye mwezi huo huo, Bell alijifungua mtoto wake wa tatu na Cannon aitwaye Rise Messiah ambaye ni wa 10.

Cannon pia alipata mtoto wa 11 wa kiume waliyempa jina la Zen aliyezaa na Alyssa Scott. Lakini mtoto huyo alifariki akiwa na umri wa miezi mitano tu kutokana na saratani ya ubongo.



# *Harmonize: Kuendesha lebo si mchezo*

**Na Mwandishi Wetu**

NYOTA wa muziki wa Bongo Fleva, Harmonize, amesema kazi ya kuendesha lebo ya muziki si rahisi na watu wasiichukulie poa.

Harmonize maarufu kama Konde Boy, ambaye jina lake halisi ni Rajab Abdul Kahal, amebainisha kuwa kuna watu wanapenda kumchukulia poa yeye na lebo yake, lakini ukweli ni kwamba amejitahidi sana.

Lebo yake ya Konde Boy ambayo mwezi huu imetimiza miaka minne tangu kuanzishwa kwake imewatoa wasanii kadhaa ambao wanatamba hivi sasa.

"Ukweli ni kwamba nimejitahidi na najitahidi kwa kadiri ya uwezo wangu kufanya mambo makubwa na kuwasaidia vijana wengine ili nao wasaidie familia zao.

"Watu wasinichukulie poa, najitahidi kufanya vitu kwa uwezo wangu wote ili kusaidia wengine, nao wasaidie familia zao,"aliandika Harmonize.

Lebo hiyo ya Harmonize imewatoa wasanii kama Ibraah na Anjella ambao kwa sasa wanatamba kwenye tasnia hiyo.




Canara Bank (Tanzania) Ltd.

(Together we can build a better life)

## PUBLICATION OF INTEREST RATES, FEES AND CHARGES

**PURSUANT TO REGULATION 11 OF THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS DISCLOSURE REGULATION, 2014 AND REGULATION 40(3)(a) OF THE FINANCIAL CONSUMER PROTECTION 2019.**

| | TZS | | USD | |
|---|---|---|---|---|
| **A. SAVINGS BANK** | | | | |
| 1. Monthly Maintanance Charges | | FREE | | FREE |
| 2. Non Maintanance of Minimum Balance | | FREE | | FREE |
| 3. A/C Statement Charges | | | | |
| a) Monthly | | FREE | | FREE |
| b) Interm | TZS | 4,300.00 | $ | 5.00 |
| 4. Cash Withdrawl Charges | | FREE | Up to 5000 | FREE |
| | | | Above 5000 | 0.26% |
| 5. Cash Deposit Charges | | FREE | | FREE |
| 6. Balance Confirmation certificate | TZS | 12,800.00 | $ | 6.00 |
| 7. A/c Closure charges | TZS | 12,800.00 | $ | 13.00 |
| 8. Activation of Dormat A/c | TZS | 5,100.00 | $ | 6.00 |
| **B. CURRENT ACCOUNT** | | | | |
| 1. Monthly Maintanance Charges | | FREE | | FREE |
| 2. Non Maintanance of Minimum Balance | | FREE | | FREE |
| 3. A/C Statement Charges a) Monthly | TZS | 4,300.00 | $ | 5.00 |
| b) Interm | Fixed TZS | 4,300.00 | Fixed | $5.00 |
| | plus For each page TZS | 500.00 | For each page | $1.00 |
| 4. Cash Withdrawl Charges | UPTO 25 MILLION | FREE | Upto 5000 | FREE |
| | ABOVE 25 MILLION | 0.11% | 5000 to 10,000 - | 0.26% |
| | | | Above 10,000 | 0.43% |
| 5. Cash Deposit Charges | UPTO 50 MIO | FREE | Upto 10,000 | FREE |
| | ABOVE 50 Million | 0.11% | > 10,000- | 0.26% |
| 5. Balance Confirmation certificate | TZS | 21,200.00 | | $13.00 |
| 6. Stop Payment Charges | TZS | 25,500.00 | | $13.00 |
| 7. Cheque Clearing Charges | | | | |
| a) Inward | TZS | 1,300.00 | | $1.00 |
| b) Outward | | FREE | | FREE |
| 8. Cheque Return Charges | | | | |
| a) Inward | TZS | 25,500.00 | | $13.00 |
| b) Outward | TZS | 25,500.00 | | $13.00 |
| 9. A/c closure charges | TZS | 21,200.00 | | $17.00 |
| **C. MOBILE BANKING CHARGES** | | | | |
| **1. Cash Withdrawal** | | | | |
| Upto 100,000 | TZS | 1,700.00 | | NA |
| 101,000 to 200,000 | TZS | 2,600.00 | | NA |
| 201,000 to 400,000 | TZS | 4,300.00 | | NA |
| 401,000 to 600,000 | TZS | 5,100.00 | | NA |
| 601,000 to 999,000 | TZS | 6,800.00 | | NA |
| **2. Funds Transfer/Mobile Wallet** | | | | |
| Upto 100,000 | TZS | 500.00 | | NA |
| 101,000 to 250,000 | TZS | 900.00 | | NA |
| 251,000 to 500,000 | TZS | 1,700.00 | | NA |
| 501,000 to 1,000,000 | TZS | 4,300.00 | | NA |
| 1,001,000 TO 10 Mn | TZS | 8,500.00 | | NA |
| **Mobile Banking Services** | | | | |
| A) Monthly Subscription Charges | TZS | 500.00 | | NA |
| B) PIN Request | TZS | 2,200.00 | | NA |
| **D. LOCKERS RENT YEARLY** | | | | |
| 1.SMALL | TZS | 296,700.00 | | NA |
| 2. MEDIUM | TZS | 508,500.00 | | NA |
| 3. BIG | TZS | 635,600.00 | | NA |

| E. REMITTANCES | TZS | | USD | |
|---|---|---|---|---|
| 1. TISS | TZS | 8,450.00 | EQUIVALLENT TO TZS 8450 | |
| **2. E Remittances** | | | | |
| Upto USD 1000 or Eq. TZS | TZS | 17,000.00 | $ | 9.00 |
| 1001 to 5000 | TZS | 20,400.00 | $ | 11.00 |
| 5001 to 10000 | TZS | 40,700.00 | $ | 22.00 |
| 10,001 and above | TZS | 84,800.00 | $ | 43.00 |
| **3. SWIFT** | | | | |
| **a) Swift Outward** | | | | |
| Upto 5,000 | | NA | $ | 39.00 |
| 5,001 to 10,000 | | NA | $ | 51.00 |
| above 10,000 | | NA | $ | 77.00 |
| **b) Swift Inward** | | | | |
| Upto 5,000 | | NA | $ | 11.00 |
| 5,001 to 10,000 | | NA | $ | 16.00 |
| above 10,000 | | NA | $ | 26.00 |
| **F. LOAN/ADVANCES RELATED CHARGES** | | | | |
| 1. Processing Charges | Upto 5 Mio - TZS | 21,200.00 | Upto 5,000 - | $85.00 |
| | 5Mio to 10 Mio - TZS | 169,500.00 | 5000 to 10,000 - | $170.00 |
| | 10 Mio to 25mio - TZS | 339,000.00 | Upto 20,000 - | $255.00 |
| | 25 mn to 500 mio - | 1.28% | 20,000 to 500,000 - | 1.28% |
| | >500mio--* (*minimum 7.5mio) | 1.06% | >500,000--* (*minimum 7,500) | 1.06% |
| 2. Documentation Charges | Upto 100 MILLION | FREE | Upto 50,000 FREE | !"#$%& |
| | >100 Mio (-Min 300,000) | 0.26% | >50,000 - (Min 150) | 0.26% |
| 3. Upfront fee on Term Loan | Upto 5Mio - TZS | 21,200.00 | Upto 20,000 - | $255.00 |
| | 5 Mio to 10 Mio - TZS | 169,500.00 | 20,000 to 500,000 - | 1.53% |
| | 10Mio 25mio - TZS | 381,400.00 | >500,000--* (*minimum 9000) | 1.28% |
| | 25 mn to 500 mio - | 1.53% | | |
| | >500mio--* (*minimum 9mio) | 1.28% | | |
| 4. Inspection Charges | Upto 100 Mio - TZS | 21,200.00 | Upto 50,000 | $22.00 |
| | >100 mio - TZS | 42,400.00 | >50,000 | $43.00 |
| 5.Credit Reference Report Charges from D&B Tanzania | TZS TZS | 101,700.00 | | $43.00 |
| 6.Pre-payment penalty | Calculated as %ge pre-paid amount in the case of takeover of liability by other | 1.70% | of pre-paid amount in the case of takeover of liability by other | 1.70% |
| **G. Guarantees (Local & International)** | | | | |
| Bonds & Guarantees | ( Min TZS 75,000) | 1.02% | | 1.02% |
| Bonds & Guarantees with 100 % Cash Margin | per quarter (Min TZS 75,000) | 0.43% | | 0.43% |
| **H. LETTER OF CREDIT** | | | | |
| **Import Letter of Credit (per qrtr of Part thereof)** | | | | |
| Opening commission | NA | | ( Min $ 200) | |
| LC amendment Commission | NA | | ( Min $50 max 350) | 1.02% |
| Swift charge for LC opening | NA | | | 0.34% |
| Swift charge for other message/amendments | NA | | | $34.00 |
| Extensions - Commissions | NA | | ( Min $200) | $34.00 |
| LC cancellation charges | NA | | ( Min $200) | 1.02% |
| Non payment of Bills on due date | NA | | Till Payment | 1.02% |
| **Export Letters of Credit (per quarter or part thereof)** | | | | |
| Advising commission | NA | | | $119.00 |
| Confirmation Commission | NA | | ( Min $150) | 0.43% |
| Negotiating bills under LC | NA | | (Min) $75+cuourier+int | 0.43% |
| Reimbursement claim paid | NA | | ( Min$75) | 0.43% |
| Extensions - Commissions | NA | | ( Min $200) | 1.02% |
| Collection of Export LC | NA | | (Min) $75+cuourier+int | 0.43% |
| Amendments | NA | | | $64.00 |

### OTHER DISCLOSURES(VIAMBATANISHI)

| | TZS | USD |
|---|---|---|
| 1. Base or Prime Lending Rate | 16 | 7 |
| 2. Maximum spread above Base or Prime Lending Rate | 5 | 5 |
| 3.Penal Interest | | |
| a. For non compliance on Terms of Saction | 3% p.a over regular rate of interest | |
| b. For Overdrawing/Excess drawing due to non payment of interest/installment/charges | 5% p.a over regular rate of interest | |
| 4. Deposit Rates | | |
| a. Current account | Nill | Nill |
| b. Savings bank deposit | 3.00% | 1.00% |

**i. Fixed Deposits of TZS**

| Amount in TZS | up to TZS 50 Million | Over TZS 50 Million | Above 100 Million |
|---|---|---|---|
| 30 -90days | 3.50% | 4.50% | 5.50% |
| 91-180days | 4.50% | 5.50% | 6.50% |
| 181-364 days | 5.50% | 7.00% | 7.50% |
| Above 1 year | 8.00% | 8.25% | 8.50% |

**ii. Fixed Deposits of USD**

| Amount in USD | up to USD 50,000 | Over USD 50,000 | Over USD 100,000 |
|---|---|---|---|
| 30 -90days | 1.50% | 2.25% | 2.50% |
| 91-180days | 2.00% | 2.75% | 3.25% |
| 181-364 days | 2.50% | 3.00% | 3.50% |
| Above 1 year | 3.00% | 3.50% | 4.00% |

| | | | |
|---|---|---|---|
| JOHN CHARLES | GM-OPERATIONS | SIGNED | 10-10-2022 |
| SALMA MRISHO | HEAD TREASURY AND TRADE FINANCE | SIGNED | 10-10-2022 |
| KAUSHENDRA TIWARI | GM-CREDIT | SIGNED | 10-10-2022 |

Canara Bank (T) Ltd, Head Office Dar Es Salaam Branch,Elia Complex P.O. Box 491, Dar Es Salaam, Tanzania , 2112532, www.canarabank.co.tz

217084302

# TAFF KUPELEKA SOKA WATU WENYE ULEMAVU MIKOANI

**Na Saada Akida**

RAIS wa Shirikisho la Mpira wa Miguu kwa Watu wenye Ulemavu nchini (TAFF), Peter Sarungi, amesema mwishoni mwa mwezi huu, kamati ya utendaji itakutana kwa ajili ya mchakato wa kuhakikisha kunakuwa na vyama vya mchezo huo katika mikoa yote Tanzania.

Akizungumza na gazeti hili jana, Sarungi alisema wanatakiwa kufanya uchanguzi wa TAFF kwa kuchagua viongozi wa juu mwishoni mwa mwaka huu na kwa mujibu wa katiba yao, wanatakiwa kupata wajumbe watakaopiga kura kutoka mikoa yote.

Alisema kikao hicho ni maalum kwa ajili ya kuangalia namna ya kuendeleza mchakato wao wa kuhamasisha kuwapo kwa vyama vya mikoa.

**"Huu mchakato ulianza mwanzoni, lakini tulisimama kwa sababu ya timu ya Taifa (Tembo Warriors), ilikuwa katika mashindano ya Kombe la Dunia, hilo tumemaliza na sasa tunarudi katika mchakato huo wa kuanzisha vyama na timu mikoani," alisema Sarungi.**

Alitaja mikoa ambayo walianza mchakato huo wa kuanzisha vyama na kupata wajumbe ni Morogoro, Dodoma, Mbeya, Iringa, Arusha, Pwani, Kagera na Mwanza.

"Tunaenda kuhamasisha mchezo huu ili kupata wajumbe mikoani pamoja na kupata timu katika mikoa hiyo lengo likiwa ni kucheza ligi kwa msimu mpya unaoanza Januari mwakani," alisema Sarungi.

Alisema michakato yote hiyo wanatarajia kuikamilisha haraka ili kuweza kuandaa timu ya taifa ya ushindani kwa ajili ya michuano ya Afrika inayotarajiwa kufanyika Januari, mwakani.

## *Gwambina yaona mwezi Championship*

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Gwambina FC juzi ilipata ushindi wake wa kwanza kwenye Ligi ya Championship baada ya kuichapa Copco mabao 3-0 kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza.

Kwenye mechi tatu zilizopita, timu hiyo ilipata sare moja na kupoteza mbili, hivyo ushindi huo umeweka hai matumaini ya kuisaka nafasi ya kurejea kwenye Ligi Kuu msimu ujao.

Timu hiyo ilicheza Ligi Kuu msimu wa 2020/21, lakini ikashuka daraja msimu huo huo.

Katika mchezo mwingine, ikiwa nyumbani Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, timu ya Green Warrios ilikiona cha moto ilipochabangwa mabao 2-1 dhidi ya Kitayosce.

Washindi hao walijifunga kupitia kwa Said Mbati, lakini walipata mabao yao mawili yaliyofungwa na Daniel William na Fabrice Ngoyi.

Kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, Pan African ililazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya African Sports.

Lilikuwa ni bao la kujifunga la Aidan Yesaya lililoipatia Pan African bao, huku la African Sport likiwekwa ndani ya kamba na Msonda Senda.

Ndanda FC ilikubali kipigo cha bao 1-0 nyumbani, Uwanja wa Nangwanda Sijaona dhidi ya Mashujaa, huku Biashara United ikionekana sasa imeamka, ikipata ushindi wa pili kwenye ligi hiyo ikifunga Pamba FC mabao 2-1, Uwanja wa Karume mjini Musama mkoani Mara.

Kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, wenyeji Ken-Gold walishindwa kuutumia vema uwanja wa nyumbani baada ya kukubali kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Fountain Gate ambayo imeonekana kuwa moja kati ya timu tishio msimu huu.

**TUMERUDI...**




Wachezaji wa Simba wakirejea nchini kutokea Angola jana, baada ya juzi kuibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Primeiro de Agosto, kwenye mechi ya mkondo wa kwanza ya Raundi ya Kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika. **PICHA: SIMBA**

## Masoud atimuliwa Dodoma Jiji FC

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Dodoma Jiji imetangaza kumfuta kazi Kocha Mkuu wa timu hiyo Masoud Djuma na benchi lake lote la ufundi, badala yake kikosi kitakuwa chini ya kocha wa timu za vijana, Omari Mohamed Omari.

Taarifa rasmi ya klabu hiyo iliyotolewa jana mchana na Idara ya Habari na Mawasiliano haikutaja sababu ya kuachana na kocha huyo, lakini timu hiyo imekuwa haina matokeo mazuri tangu kuanza kwa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

"Uongozi wa timu yetu umefikia makubaliano ya pande zote mbili kutoendelea na kocha mkuu wa klabu Masoud Djuma Irambona. Aidha, menejimenti ya Dodoma Jiji imefikia uamuzi wa kuvunja benchi lote la ufundi ili kupata wasaa wa kuliunda upya.

"Uongozi wa klabu unawashukuru kocha mkuu pamoja na benchi lote la ufundi kwa mchango wao mkubwa ndani ya klabu yetu na inawatakia kila la kheri katika majukumu yao mapya," ilieleza taarifa ya klabu hiyo na kuongeza.

"Kwa sasa klabu yetu itakuwa chini ya usimamozi wa kocha wa timu za vijana Omari Mohamed Omari."

## Taifa Jang'ombe, Black Sailor zalala tena

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Black Sailor na Taifa Jang'ombe zimeendelea kuandamwa na matokeo mabaya katika michezo ya Ligi Kuu Zanzibar inayoendelea visiwani hapo.

Katika mzunguko huu wa sita uliomalizika juzi, Taifa Jang'ombe ilipokea kichapo cha bao 1-0 dhidi ya Malindi na kuifanya timu hiyo kupoteza michezo minne mfululizo ikiendelea kubaki na alama mbili kwenye michezo sita waliyocheza.

Kwa upande wa timu ya Black Sailor nayo imepoteza mbele ya Maafande wa KVZ kwa kupachikwa bao 1-0 katika mechi iliyochezwa juzi kwenye Dimba la Amaan majira ya saa mbili usiku.

Kwa matokeo hayo, Black Sailor imeendelea kuburuza mkia katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ikiwa na alama moja huku akipoteza michezo mitano.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa ba Ofisa Habari wa Taifa Jang'ombe, Haji Kiduka, timu hiyo inaendelea kutafuta Kocha Mkuu na Msaidizi wake kabla ya Kumaliza mzunguko wa kwanza.

HABARI MICHEZO

ZISIKUPITE

### PINO ATAKIWA CHELSEA

KLABU ya Chelsea inamtaka kiungo wa kati wa Villarreal, Yeremy Pino mwenye umri wa miaka 19, kama mpango wa dharura huku kiungo wa kati wa England, Mason Mount mwenye miaka 23, akielekea katika miezi yake ya mwisho ya mkataba wake wa miezi 20. Kiungo wa kati wa AS Roma, Lorenzo Pellegrini mwenye umri wa miaka 27 ni chaguo lingine la 'Blues' hao. ***(Telegraph)***

### AKE AWINDWA INTER

INTER Milan ipo tayari kutoa dau la kumsajili kiungo wa Uholanzi, Ake mwenye umri wa miaka 27, ambaye pia ananyatiwa na Manchester City. ***(Ekrem Konur on Twitter)***

### JUTGLA AWANIWA ARSENAL

ARSENAL wameonyesha nia ya kutaka kumsajili mshambuliaji wa Club Bruges, Ferran Jutgla mwenye umri wa miaka 23. ***(Totofichajes)***

### LOPETEGUI KUSUBIRIWA WOLVES

KLABU ya Wolves huenda inasubiri zaidi kumfanya Julen Lopetegui kuwa kocha wao kwani raia huyo wa Hispania anashughulikia suala la kifamilia. ***(Daily Mail)***

### ZIYECH ATAKIWA MILAN

AC Milan wanaangalia uwezekano wa kumsajili winga wa Chelsea na Morocco, Hakim Ziyech mwenye umri wa miaka 29 Januari. ***(Mail)***

### DOKU AWINDWA LIVERPOOL

LIVERPOOL inaweza kumsajili mshambuliaji wa Rennes na Ubelgiji, Jeremy Doku mwenye umri wa miaka 21, Januari. ***(Calciomercato)***

### MARTINEZ KUZUIWA VILLA

KLABU ya Aston Villa haina nia ya kumruhusu mlinda mlango wa Argentina, Emiliano Martinez mwenye umri wa miaka 30 kuondoka Januari, huku Manchester United ikiwa miongoni mwa klabu zinazomwania. ***(Football Insider)***

### GAKPO BADO AWANIWA

KLABU za Manchester United, Southampton na Everton bado zinamwania mshambuliaji wa PSV Eindhoven na Uholanzi, Cody Gakpo mwenye umri wa miaka 23. ***(Football Transfer)***

### TRASSORD NA MKATABA MPYA

KLABU ya Brighton inapanga kufanya mazungumzo ya mkataba mpya na mshambuliaji wa Ubelgiji, Leandro Trossard, 27, na kiungo wa kati wa Argentina, Alexis Mac Allister mwenye umri wa miaka 23. ***(Athletic)***


### ADEL AGOMBEWA ENGLAND

LIVERPOOL wanafikiria kumnunua winga wa Misri na Pyramids, Ibrahim Adel Januari, 21, huku Arsenal, Brentford, Brighton na Nottingham Forest pia zikimwania mchezaji huyo. ***(90 Minutes)***

### CONTE AIKATAA JUVE

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Antonio Conte, 53, amepuuza tetesi zinazomhusisha na kurejea Juventus kuwa "zisizo na msingi". ***(Evening Standard)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO APIGA BAO LA 700 NGAZI YA KLABU

**LIVERPOOL,** England

Pia amefunga mabao 117 kwa timu yake ya taifa, huku kwa United pekee akifikisha 144...

CRISTIANO Ronaldo alifunga bao lake la 700 katika ngazi ya klabu wakati Manchester United ikitoka nyuma na kuwafunga Everton mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Goodison Park, Jumapili.

**Ronaldo alifikisha idadi hiyo ya mabao katika maisha yake ya soka ya kuvutia baada ya kuingia katika kipindi cha kwanza akichukua nafasi ya Anthony Martial aliyeumia, na kuhakikisha United inarejea katika njia ya ushindi kwenye Ligi Kuu England baada ya kipigo kibaya cha 'dabi' kutoka kwa Manchester City.**

Ronaldo hakuanza kwenye ziara hiyo ya United kule Merseyside, lakini jeraha la kipindi cha kwanza la Martial lilimfungulia njia ya kutengeneza rekodi nyingine.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37, ambaye amefunga mabao 117 kwa timu yake ya taifa, sasa amefikisha jumla ya mabao 144 aliyoifungia United katika vipindi viwili vya kukaa kwake Old Trafford.

Pia, amefunga jumla ya mabao 556 katika klabu za Sporting CP, Real Madrid na Juventus.

United walikuwa wameanza polepole pale Goodison Park na wakajikuta wakiwa nyuma kwa bao 1-0 lililofungwa na Alex Iwobi kwa shuti la umbali wa yadi 25.

Mnigeria huyo amefunga au kusaidia katika mechi tatu mfululizo za Ligi Kuu England kwa mara ya pili tu katika maisha yake ya soka (mara ya kwanza ikiwa ni Aprili 2016).

'Mashetani Wekundu' hao walisawazisha baada ya Antony kutumia pasi nzuri ya Martial na kumfunga golikipa, Jordan Pickford.

Na Antony ambaye ni raia wa Brazil akiwa mchezaji wa kwanza wa United kufunga katika kila mechi tatu za kwanza kwenye Ligi Kuu kwa klabu hiyo.

Ronaldo kisha akaihakikishia United ushindi na kuwa timu ya kwanza katika historia ya Ligi Kuu England kushinda mchezo wa 100 baada ya kutanguliwa kufungwa 1-0.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 367,

MECHI KALI

AC MILAN
VERSUS
CHELSEA

1 | 2.94
X | 3.28
2 | 2.30

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# DYBALA HATARINI KUKOSA KOMBE LA DUNIA QATAR

**ROME,** Italia

JOSE Mourinho anaamini kwamba, huenda Paulo Dybala hataichezea tena AS Roma mwaka huu baada ya raia huyo wa Argentina kuumia katika ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Lecce, Jumapili.

Hilo pia linamweka kwenye shaka kuichezea Argentina katika michuano ya Kombe la Dunia baadaye mwaka huu nchini Qatar.

Dybala alifunga bao la ushindi kwa mkwaju wa penalti baada ya Gabriel Strefezza kufuta bao la kwanza la Chris Smalling dakika ya sita, na kupata ushindi wa tatu mfululizo kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A.

Hata hivyo, fowadi huyo alianza kuchechemea na kushika paja lake la kushoto baada ya kufunga bao lake, na alionekana kutokwa na machozi kwenye benchi baada ya kutolewa nje.

Dybala amefunga mabao sita katika mechi 10 alizoichezea Roma msimu huu na ni hesabu ya juu ya timu (katika mashindano yote), lakini Mourinho sasa anaweza kumkosa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 kwa kipindi kirefu.

Alipoulizwa kuhusu hali ya Dybala baada ya ushindi huo, Mourinho aliiambia DAZN: "Nasema vibaya, lakini nafikiri vibaya sana.

"Mimi si daktari, lakini kwa uzoefu wangu, na baada ya kuzungumza na Paulo, kuna uwezekano kwamba hatutamuona mwaka huu."

Iwapo Dybala ataondolewa kwa muda mrefu, itakuwa pia pigo kwa Argentina kabla ya Kombe la Dunia, huku mshambuliaji huyo akiwa amecheza mechi 34 za kikosi hicho maarufu kwa jina la utani la Albiceleste.






# *Arteta: Arsenal ilistahili ushindi kwa Liverpool*

**LONDON,** England

MIKEL Arteta amesifu uchezaji wa timu yake katika ushindi wao 'uliostahili' dhidi ya Liverpool Jumapili, akisema kwamba Arsenal ilishinda 'kila kitu' siku hiyo.

Arsenal walikuwa kwenye kiwango kizuri pale kwenye dimba la Emirates kwa mabao ya Gabriel Martinelli na mawili kutoka kwa Bukayo Saka yaliyotosha kupata ushindi wa 3-2 na kuwafanya kurejea kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu England.

Akizungumza na Sky Sports baada ya mchezo huo, Arteta alisema kama ilivyotarajiwa, wachezaji walionyesha kiwango bora zaidi.

"Ni nzuri, haswa jinsi tulivyoshinda mchezo, jinsi tulivyocheza, mazingira ambayo tulitengeneza pia na nadhani sisi tulistahili kushinda mchezo.

"Tishio ambalo wanalo wakati wowote, wanaweza kukufunga na kutumia nafasi na walikuwa wazuri sana na nafasi walizopata. Lakini nadhani tulionyesha utulivu katika nyakati ngumu, ha wa kwa jinsi tulivyochez katika kipindi cha pili."

Alipoulizwa kuhus mchezaji bora wa mech hiyo, Martinelli, Arteta alis ma: "Yeye ni mdogo san na ni wazi unapoona maha alipokuwa mwaka mmo uliopita alipoanza dhi ya Brentford na alipo le maendeleo ni ya ajabu.

"Ana njaa ya mafanik hamu yake na jinsi anavy penda kucheza na kufany mazoezi, anakuwa bora ki siku."

,741,460

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 11/10/22 | 22:00 | Dinamo Zagreb vs RB Salzburg | 2.74 | 3.28 | 2.44 |
| 02. 11/10/22 | 22:00 | AC Milan vs Chelsea | 2.93 | 3.33 | 2.28 |
| 03. 12/10/22 | 17:15 | FC Andorra vs Burgos | 2.24 | 3.02 | 3.32 |
| 04. 12/10/22 | 22:00 | Racing Santander vs Zaragoza | 2.85 | 2.95 | 2.65 |
| 05. 13/10/22 | 03:45 | Corinthians vs Flamengo | 2.87 | 3.16 | 2.30 |
| 06. 13/10/22 | 19:45 | Betis vs Roma | 2.28 | 3.41 | 2.95 |
| 07. 13/10/22 | 19:45 | Union Saint Gilloise vs Sporting Braga | 2.34 | 3.35 | 2.90 |
| 08. 13/10/22 | 19:45 | Nantes vs SC Freiburg | 3.06 | 3.41 | 2.22 |
| 09. 13/10/22 | 19:45 | Slovan Bratislava vs FC Basel | 2.90 | 3.30 | 2.37 |
| 10. 13/10/22 | 19:45 | Djurgardens IF vs KAA Gent | 3.05 | 3.39 | 2.24 |
| 11. 13/10/22 | 22:00 | Trabzonspor vs Monaco | 3.14 | 3.39 | 2.24 |
| 12. 13/10/22 | 22:00 | Ferencvaros TC vs Red Star Belgrade | 2.23 | 3.40 | 3.05 |
| 13. 13/10/22 | 22:00 | Steaua Bucuresti vs Silkeborg | 2.70 | 3.25 | 2.55 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 11/10/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:00 | 4402 | Huda Hue vs QNK Quang Nam | 4.20 | 3.05 | 1.99 |
| 12:30 | 5721 | Cong Anh Nhan Dan vs BA Ria Vung Tau FC | 1.55 | 3.68 | 5.43 |
| 13:00 | 3957 | Dong Tam Long AN vs Binh Phuoc | 2.03 | 2.77 | 4.08 |
| 13:30 | 1326 | Incheon Utd vs Jeju Utd | 3.17 | 3.21 | 2.11 |
| 13:30 | 2304 | Jeonbuk Hyundai vs Gangwon | 1.62 | 3.65 | 4.76 |
| 14:00 | 1814 | Van Yerevan vs Lernayin Artsakh | 2.15 | 3.05 | 3.25 |
| 14:00 | 2906 | Shirak Gyumri vs Bkma Yerevan | 2.36 | 3.15 | 3.05 |
| 14:30 | 4131 | Sarawak vs Selangor FC | 3.50 | 3.84 | 1.81 |
| 14:45 | 1231 | Mes Shahr-e Babak vs Shams Azar Qazvin | 2.75 | 2.70 | 2.95 |
| 15:15 | 2653 | Negeri Sembilan vs Melaka | 1.22 | 5.65 | 9.75 |
| 15:15 | 4093 | Pahang FA vs Sabah | 2.02 | 3.74 | 2.96 |
| 15:45 | 3312 | AL Ain vs Jeddah Club | 2.12 | 2.87 | 3.56 |
| 16:00 | 1617 | Johor Darul Takzim vs Kedah | 1.19 | 6.80 | 13.00 |
| 16:00 | 2074 | Pars Jonoubi Jam vs Arman Gohar Sirjan | 2.41 | 2.67 | 3.21 |
| 16:00 | 2826 | DAR AL Dawa vs Al-Arabi | 2.26 | 3.07 | 3.02 |
| 16:00 | 4415 | Kuala Lumpur vs Terengganu | 2.52 | 3.25 | 2.52 |
| 16:00 | 5929 | FC Petaling Jaya City vs Penang | 1.73 | 3.85 | 4.30 |
| 16:00 | 5934 | Al-Jalil vs Kfarsoum | 1.48 | 4.10 | 5.47 |
| 16:15 | 5097 | Esteghlal Mollasani vs Khosheh Talaei | 2.42 | 2.80 | 3.35 |
| 17:00 | 3089 | Jamshedpur vs Delhi Dynamos FC | 1.37 | 4.59 | 6.64 |
| 18:15 | 2283 | Al Taawon vs Abha | 1.69 | 3.70 | 4.80 |
| 18:15 | 4622 | Dhamk vs Al Ittihad Jeddah | 4.51 | 3.56 | 1.76 |
| 19:00 | 5892 | Rayon Sports FC vs AS Kigali | 2.60 | 2.90 | 2.95 |
| 19:45 | 4255 | Copenhagen vs Manchester City | 16.02 | 7.25 | 1.14 |
| 19:45 | 5715 | Maccabi Haifa vs Juventus | 4.01 | 3.53 | 1.83 |
| 20:00 | 2740 | Jonkopings Sodra vs IK Brage | 2.37 | 3.43 | 2.88 |
| 20:00 | 5785 | Halmstads BK vs Orgryte IS | 1.54 | 4.24 | 5.65 |
| 20:30 | 5094 | AL Faiha vs Al-Ettifaq | 2.95 | 3.15 | 2.42 |
| 21:00 | 3115 | Doncaster vs Barnsley | 2.44 | 3.31 | 2.58 |
| 21:45 | 1134 | Charlton vs Exeter | 2.28 | 3.27 | 2.98 |
| 21:45 | 2563 | Whitby Town vs Hyde United FC | 2.97 | 3.36 | 2.14 |
| 21:45 | 3392 | Lancaster City vs Warrington Rylands 1906 FC | 2.39 | 3.55 | 2.70 |
| 21:45 | 3739 | Utd of Manchester vs Morpeth Town | 2.16 | 3.55 | 2.82 |
| 21:45 | 3765 | Kelty Hearts FC vs Queen of South | 2.63 | 3.32 | 2.48 |
| 21:45 | 4092 | Bonnyrigg Rose vs Annan Athletic | 1.86 | 3.45 | 3.69 |
| 21:45 | 4150 | Elgin City vs Albion Rovers | 1.83 | 3.45 | 3.79 |
| 21:45 | 4546 | Dundee Utd vs Hibernian | 3.59 | 3.34 | 2.01 |
| 21:45 | 4995 | Gillingham vs Colchester | 1.97 | 3.22 | 3.56 |
| 21:45 | 5033 | Atherton Collieries vs Belper Town | 1.69 | 3.64 | 4.27 |
| 21:45 | 5388 | York City vs Dagenham and Redbridge | 2.21 | 3.46 | 2.92 |
| 21:45 | 5541 | Wigan vs Blackburn | 2.57 | 3.16 | 2.67 |
| 21:45 | 5921 | Peterborough vs Forest Green | 1.46 | 4.38 | 5.97 |
| 21:45 | 5986 | MK Dons vs Bristol Rovers | 2.01 | 3.46 | 3.41 |
| 22:00 | 1104 | CA Fenix vs Deportivo Maldonado | 2.22 | 2.88 | 3.32 |
| 22:00 | 1355 | Dinamo Zagreb vs RB Salzburg | 2.73 | 3.23 | 2.47 |
| 22:00 | 1494 | AC Milan vs Chelsea | 2.94 | 3.28 | 2.30 |
| 22:00 | 1817 | Borussia Dortmund vs Sevilla FC | 1.50 | 4.26 | 5.54 |
| 22:00 | 4635 | Shakhtar Donetsk vs Real Madrid | 6.90 | 5.13 | 1.35 |
| 22:00 | 5735 | Paris St Germain vs Benfica | 1.42 | 4.80 | 5.91 |
| 22:00 | 5872 | Celtic vs RB Leipzig | 3.08 | 3.57 | 2.10 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



# KIPANGA YATOA SABABU SARE NA WATUNISIA CAF

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Msaidizi wa Kipanga FC ya visiwani Zanzibar, Khamis Hussan, amesema kutokuwa makini na ugeni wao kwenye mashindano ya kimataifa ni miongoni mwa sababu zilizochangia kuambulia matokeo ya sare tasa kwenye Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Club Africain ya Tunisia.

Kipanga ilishindwa kuutumia vema uwanja wake wa nyumbani baada ya kulazimishwa sare tasa katika Dimba la Amaan Jumamosi iliyopita, hivyo sasa itahitaji ushindi wowote ama sare ya mabao ili kusonga mbele kwenye michuano hiyo ya Afrika.

**Akizungumza na gazeti hili jana kutoka visiwani Zanzibar kocha huyo alisema wachezaji wake waliten- geneza nafasi nyingi lakini walishindwa kuzitumia.**

Kuelekea mchezo ujao wa marudiano nchini Tunisia, Hassan alisema kikosi chake kina majeruhi wawili, Hamad Fakhi ambaye aliumia kisigino na Mundhir Diara anayesumbuliwa na nyama za paja.

"Hao ndio majeruhi niliokuwa nao ambao waliumia Jumamosi, mpaka sasa wapo chini ya uangalizi wa daktari wakiendelea na matibabu," alisema Hassan.

Alisema jana waliendelea na mazoezi kuelekea mchezo wa marudiano na kwamba wanasubiri uongozi kuwapa ratiba kamili ya safari kuelekea nchini Tunisia kwa mechi ya mkondo wa pili itakayopigwa Jumapili wiki hii.

Alisema licha ya kupata sare hiyo wakiwa nyumbani, amerekebisha makosa aliyoyaona katika mchezo huo ili yasijitokeze tena kwenye mechi ijayo.

Alisema lengo lao ni kupambana kupata matokeo mazuri ili wasonge mbele na kuiwakilisha vema Zanzibar kupitia mashindano ya kimataifa.

TUMEWASHIKA...



Bukayo Saka akimpongeza Gabriel Martinelli kwa kumdandia mgongoni baada ya kuifungia timu yake bao la kwanza wakati wakishinda 3-2 dhidi ya Liverpool kwenye Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Emirates juzi. Mabao mengine mawili ya Arsenal yalifungwa na Saka. **PICHA: MTANDAO**

# *Chama atoa siri kushinda ugenini*

INATOKA UKURASA 32

ano.

Kwa mujibu wa Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema kikosi kimewasili jana alfajiri na wachezaji wameingia kambini kujiandaa na mchezo wa marudiano.

Alisema licha ya kupata ushindi ugenini wanaona bado hawajamaliza mechi, hivyo kuanza maandalizi ya mchezo wa marudiano mapema kwa ajili ya kuendelea kupata matokeo mazuri katika mechi ya marudiano.

"Licha ya kupata ushindi huu ugenini tunaona bado hatujamaliza mechi ndio maana maandalizi ya mchezo wa marudiano tunaanza mapema, tunahitaji kupata ushindi mnono nyumbani ili kufikia malengo yetu ya kucheza hatua ya makundi," alisema Ahmed na kutaja viingilio vya mechi hiyo kuwa ni mzunguko Sh. 3,000, machungwa Sh. 5,000, VIP C Sh. 10,000, VIP B, Sh. 15, 000 na VIP A Sh. 20,000.

Alisema wameweka viingilio rafiki ili kuwafanya mashabiki kujitokeza kwa wingi kuisapoti timu yao kufika hatua ya makundi kwa mara ya nne kwenye historia yao.

# Nabi aifungia kazi Al Hilal CAF

INATOKA UKURASA 32

iliyopita, kilimchagua Feisal baada ya kuonyesha kiwango kizuri kwa Septemba na kutoa mchango mkubwa kwa klabu yake ikiwa ni pamoja na kufunga mabao mawili.

Alisema Feisal aliwashinda Moses Phiri wa Simba na Reliants Lusajo wa Namungo FC huku kwa upande wa Janza akiwashinda Charles Mkwassa wa Ruvu Shooting na Thierry Hitimana wa KMC FC.

"Kamati ya tuzo imemchagua Meneja wa Uwanja wa Majaliwa, Lindi kuwa meneja bora wa uwanja kwa mwezi Septemba kutokana na kufanya vizuri katika menejimenti ya matukio ya mchezo pamoja na masuala yanayohusu miundombinu uwanjani," alisema Boimada.

Michezo
Jumanne Oktoba 11, 2022
Nipashe



Ronaldo apiga bao la 700 klabuni UKURASA 29

CHA KWANZA...



Kiungo fundi wa Simba, Clatous Chama, akiifungia timu yake bao la kwanza wakati ikishinda 3-1 dhidi ya Primeiro de Agosto ya Angola kwenye mechi ya mkondo wa kwanza ya Raundi ya Kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa 11 de Novembro juzi. **PICHA: SIMBA**

# Nabi aamua kuifungia kazi rasmi Al Hilal CAF

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, ameamua kuifungia kazi Al Hilal ya Sudan baada ya timu yake kuipigisha timu yake mazoezi mara mbili kwa siku, huku akieleza kuwa anatarajia kufanya kweli ugenini.

Awali, Yanga kabla ya kucheza mechi ya kwanza dhidi ya Al Hilal walikuwa wakifanya mazoezi mara moja kwa siku na baada ya kupoteza mechi hiyo, Nabi amewafungia kazi wachezaji wake kwa kuwapa program maalum kuelekea mchezo huo wa marudiano utakaopigwa Jumapili wiki hii jijini Khartoum, Sudan.

Kikosi cha Yanga kinatarajia kuondoka keshokutwa, Alhamisi kuelekea Khartoum, Sudan kwa ajili ya mchezo huo ambao wanahitaji kupata ushindi wowote ama sare ya kuanzia mabao mawili ili kutinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema amerejea uwanjani kwa ajili ya kufanyia kazi mapungufu yao kwa kuelekea kupambania matokeo chanya katika mechi hiyo ya marudiano.

Alisema wanaendelea na maandalizi kwa kufanya mazoezi mara mbili kwa siku ambapo asubuhi wanafanya saa mbili na nusu na jioni.

"Tumeona madhaifu yetu katika mechi yetu ya hapa nyumbani, sasa tumeyabeba hayo na kufanyia kazi kuhakikisha tunakisuka kikosi imara kumalizia dakika 90 zilizobakia," alisema Nabi.

Katika hatua nyingine Kiungo wa Yanga, Feisal Salum amechaguliwa kuwa mchezaji bora wa Septemba wa Ligi Kuu Bara huku Kocha wa Namungo FC, Honor Janza akichaguliwa kuwa kocha bora wa mwezi huo.

Kwa mujibu wa Ofisa Habari na Mawasiliano wa Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB), Kareem Boimada, Kikao cha Kamati ya Tuzo TFF, kilichokutana Dar es Salaam mwishoni mwa wiki

INAENDELEA UK. 31

# *Chama atoa siri kushinda ugenini*

## Mgunda asema kazi haijaisha mpaka iishe kwa Mkapa, kuiona kwa Mkapa buku tatu tu...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

WAKATI Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, akisema kazi waliyoianza nchini Angola ya kusaka nafasi ya kufuzu hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika haijaisha mpaka dakika 90 za pili zitakapomalizika katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumapili wiki hii, kiungo fundi na mtaalamu wa kupika mabao katika kikosi hicho, Clatous Chama, ametoa siri ya timu hiyo kushinda mechi zake za ugenini.

**Simba juzi iliibuka na ushindi wa mabao 3-1 ugenini nchini Angola dhidi ya Primeiro de Agosto, shukrani kwa Chama aliyeifungia bao la kwanza na kisha kupika mengine mawili kwa kuwamegea pasi za upendo Israel Mwenda na Moses Phiri.**

Akizungumzia mchezo huo, Chama alisema kabla ya mechi haijaanza aliwakusanya wachezaji wenzake na kuwaambia kwa nini wapo pale, na wasiangalie sana mechi za Ligi Kuu, kwani michuano hii ndiyo ya kuipa kipaumbele.

"Tunashinda ugenini kwa sasa kwa sababu Simba ni timu kubwa na yenye uzoefu kwenye mechi hizi, tumeshapata uzoefu na tunaijua (michuano hii), hivyo haitupi tabu. Nawaomba wanachama na mashabiki wafurahi na tutaungana nao kwenye mechi ya marudiano ili tukishinda na kuingia makundi tufurahi kwa pamoja," alisema Chama.

Kwa upande wa Mgunda yeye alisema mechi yao dhidi ya Primeiro de Agosto haijaisha na badala yake waunganishe nguvu za pamoja ili kuimaliza kazi Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

"Kazi haijaisha hadi iishe, tumeshapiga hatua mguu mmoja sasa bado kumalizia wa pili kuungana na mwenzake, akili zetu na mtazamo tunafikiria mechi ya marudiano, tumeshinda mabao matatu, lakini kuna mazuri nimeyaona tunaenda kuyaendeleza ili tufanye vizuri zaidi na mapungufu tunaenda kuyafanyia kazi ili kuweza kuyaondoa kabisa," alisema Mgunda.

Alisema mechi ilikuwa ngumi na si kama wengi walivyofikiria kwa sababu walicheza na timu ambayo ipo nyumbani.

"Mechi ya kwanza tumeimaliza bado mechi inayofuata, tumepata matokeo mazuri ugenini, tunakwenda kujipanga ili kuhakikisha mechi ijayo tunapata ushindi mzuri zaidi. Mechi ilikuwa ngumu kwa sababu tulicheza na timu ambayo ipo nyumbani kwao, walihitaji matokeo kwenye ardhi yao, ilihitaji nguvu za ziada kuweza kupata matokeo.

"Tuliwaheshimu kwa sababu wako nyumbani, tukapata goli la mapema na tukawapa fursa wao wacheze, lakini wacheze kwenye maeneo yao si karibuni na kwetu," alisema Mgunda na kuongeza.

"Tujitoe kwa ajili ya timu yetu kwa sababu ndege wafananao ndiyo huruka pamoja."

Simba ambayo ilirejea jana imeingia kambini tayari kwa mechi ya marudiano Jumapili itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa kuanzia saa 10:00 alasiri.

Mgunda alisema mchezo wa marudiano hautakuwa rahisi licha ya mtaji mzuri wa mabao na wanajipanga kuhakikisha wanashinda tena.

Alisema wamerejea nyumbani na kuanza maandalizi makubwa na kusahau matokeo waliyoyapata ugenini na kuhitaji kuanza upya katika mechi yao ya marudi-

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >